# UONGOZI UNAVYOJITOKEZA KATIKA FASIHI YA KISASA: UCHUNGUZI WA RIWAYA MPYA YA MIAKA YA 2000


**NA**

**NJENGA ALICE WANJIRU**


**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Kijamii, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ili Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili**


**Chuo Kikuu cha Moi**



**2021**

# UNGAMO

**Ungamo la Mtahiniwa**

Kazi hii ni yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine kwa minajili ya kutahiniwa kwa shahada yoyote.

Sahihi…………………………………………Tarehe……………………………

**Njenga Alice Wanjiru**

**SASS/PGK/02/10**

**Ungamo la Wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa ridhaa yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi…………………………………………Tarehe……………………………

**Prof. Issa Mwamzandi**
Idara ya Isimu, Fasihi na Mawasiliano,
Chuo Kikuu cha Kabianga,
Kericho, Kenya.

Sahihi…………………………………….. .Tarehe…………………………

**Bw. Kenga Mumbo**
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,
Chuo Kikuu cha Moi,
Eldoret, Kenya.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mume wangu Caleb Nyagar Akuku, watoto wangu William Akuku Nyagar na Laurayn Wairimu Nyagar na mama yangu Susan Wairimu.

## SHUKURANI

Kwanza namshukuru Mungu kwa kuendelea kunitunuku uhai na afya njema mimi pamoja na familia yangu. Pili nawashukuru kwa dhati wasimamizi wangu Prof. Issa Mwamzandi na Bw. Kenga Mumbo kwani ni kutokana na usimamizi na uelekezi wao nimefanikiwa kuifanya na kuikamilisha kazi hii. Namkumbuka Prof. Naomi Shitemi (Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi) ambaye alikuwa mmoja wa wasimamizi wangu wa kwanza. Sitasahau kuwashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, kwa kuendelea kunipevusha tangia shahada ya kwanza. Shukran za kipekee zimwendee Dkt Noordin Mwanakombo kwani ni kutokana na mijadala mikali darasani kuhusu riwaya mpya nilipata wazo la kufanya utafiti huu. Mola awabariki wote.

Naishukuru wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia kwa kufadhili masomo yangu. Sitawasahau wakubwa wangu - Mkurugenzi wa Habari Olewe Owiti, manaibu wake Peter Chepkwony na Joseph Kipkoech, na Mkuu wa Kaunti ya Uasin Gishu Bi. Immaculate Maima - ambao wote walinipa motisha na kunipa nafasi ya kuhudhuria mihadhara. Nawashukuru pia Leparleen Lenapeer ambaye alinipa motisha wa kurudi shuleni, Bi. Beatrice Omari ambaye alinishauri na kunishikiniza kuhusu kuendeleza masomo na pia Moses Marta, mkubwa wangu, ambaye pia aliniunga mkono kuhusiana na wazo hilo. Sitawasahau wanafunzi wenzangu Nyambura Mugeke na Caroline Milgo. Tulitembea nanyi katika safari hii.

# IKISIRI

Uongozi ni dhana muhimu sana katika jamii. Jamii zote ulimwenguni huwa na kiongozi wa aina fulani ambaye hutwikwa majukumu ya kuhakikisha kuwa watu wote walio chini yake wanapokea usawa kutokana na uongozi wake. Swala la uongozi limeshughulikiwa katika kazi za fasihi kwa namna tofauti tofauti. Utafiti huu uliangazia taswira ya uongozi inavyojitokeza katika fasihi ya kisasa kwa kuchunguza riwaya mpya za miaka ya 2000. Uliangazia mwelekeo mpya ambao unakisiwa umechukuliwa na baadhi ya waandishi wa riwaya mpya wanaoliona suala hili kwa mtazamo wa ndani nje. Madhumuni yafuatayo yalizingatiwa: Kufafanua taswira ya uongozi kama inavyosawiriwa na riwaya mbili mpya kwa kuangazia matatizo ya uongozi katika asasi za siasa na dini; Kutathmini mchango wa wananchi katika uongozi kwa mujibu wa riwaya zilizoteuliwa; na kuchunguza mtazamo wa ndani nje na mapendekezo yanayotolewa na riwaya kukabiliana na changamoto za uongozi. Riwaya za *Msimu wa Vipepeo* Wamitila (2007) na *Paradiso* Habwe (2010) ziliteuliwa. Data ilikusanywa kupitia usomaji makini wa riwaya zilizoteuliwa kwa kuzingatia mawazo ya waandishi yawe hasi au chanya kuhusu uongozi kwa kutumia uchambuzi wa yaliyomo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhistoria mpya. Data ilipangwa na kuchanganuliwa kimaelezo hivi kwamba mada zinazohusiana ziliwekwa na kuhusishwa kwa kijumla kama maoni ya waandishi kuhusu uongozi katika kipindi hiki maalum cha kihistoria. Utafiti huu umegundua kuwa uongozi bado ni changamoto katika asasi tofauti za kijamii na hasa katika siasa, serikali na dini ambazo zilishughulikiwa na riwaya zilizoteuliwa. Uongozi una athari za moja kwa moja katika maendeleo ya jamii na kwamba watawaliwa wanachangia tatizo hili. Waandishi wameonyesha kuwa ni lazima viongozi wayaangazie matatizo ya jamii kwa kushauriana na jamii badala ya kujiangazia wao binafsi. Pia, wananchi lazima wahakikishe kuwa viongozi wanawajibika kwa kujihusisha na masuala ya uongozi nchini. Katika dini, waandishi wanataka asasi hiyo iweze kujirekebisha kwa kuangazia maadili ya kidini ili jamii iwachukulie kwa dhati.

## ABSTRACT

In any society leadership is a very important concept. All communities globally are usually governed by a certain leader who is tasked with responsibilities of ensuring that everyone under his leadership enjoys fairness as a result of his/her rule. In literary works leardership has been viewed in diverse perspectives by different authors. The study analysed the leadership concept in various social institutions as depicted by writers of the new Swahili novel written since 2000. These authors view the problem as more of an inside than outside one as represented earlier on by preceding authors. The study was guided by the following objectives: to interogate leadership as depicted in the novels by focusing on leadership problems in political and religious institutions; to analyse the role of the led or the masses in leadership; and to investigate into the intrinsic-extrinsic concept and the novels' recommendations to dealing with leadership challenges. The novels *Msimu wa Vipepeo* by Wamitila (2007) and *Paradiso* by Habwe (2010) were selected for the study. Data was collected through critical reading of the selected novels focusing on the authors' views on leadership both positive and negative using content analysis guided by the tenets of new historicism. It was later analysed and arranged so that related topics were presented as the opinion of the writers on leadership during this specific historical period. The research has revealed that leadership continues to be a challenge in different institutions especially in politics, government and religion which were dealt with by the novels. It was further noted that leadership has a direct effect on the development of the society and that citizens are equally culpable in the quality of leadership that is offered to them by their leaders. The authors, in a way, recommend that leaders must address the community's problems through consultations with the masses. Citizens must hold their leaders into account by actively getting involved in their country's leadership. With regards to religion, the authors call for reforms that focus on religious ethics that will make the masses take the institution more seriously.

# YALIYOMO

UNGAMO ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKURANI ..... iv
IKISIRI ..... v
ABSTRACT ..... vi
YALIYOMO ..... vii
UFAFANUZI WA ISTILAHI ..... x
MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO ..... xii
**SURA YA KWANZA ..... 1**
**UTANGULIZI ..... 1**
1.1 Utangulizi ..... 1
1.2 Usuli wa Utafiti ..... 1
1.3 Suala la Utafiti ..... 4
1.4 Sababu za Kuteua Mada ya Utafiti ..... 5
1.5 Madhumuni ya Utafiti ..... 6
1.6 Nadharia Tete ..... 6
1.7 Misingi ya Nadharia ..... 6
1.8 Upeo wa Utafiti ..... 9
1.9 Yalioandikwa Kuhusu Mada ..... 10
1.10 Mbinu za Utafiti ..... 18
1.10.1 Mbinu ya Kithamano ..... 18
1.10.2 Uteuzi wa Sampuli Kimaksudi ..... 19
1.10.3 Mbinu za Ukusanyaji Data ..... 19
1.11 Uchanganuzi wa Data ..... 20
1.12 Uwasilishaji wa Data ..... 21
**SURA YA PILI ..... 22**
**HISTORIA FUPI YA WATUNZI NA KAZI ZAO ..... 22**
2.1 Utangulizi ..... 22
2.2 Historia Fupi Kuhusu John Habwe ..... 22
2.3 Historia Fupi ya K.W. Wamitila ..... 24
2.4 Dhana ya Nje Ndani ..... 26
2.5 Mtazamo wa Ndani Nje ..... 29

2.6 Dhana ya Uongozi ........ 33
2.7 Dhana ya Riwaya Mpya ........ 35
2.8 Hitimisho ........ 36
**SURA YA TATU ........ 38**
**SUALA LA UONGOZI KATIKA RIWAYA YA *MSIMU WA VIPEPEO* ........ 38**
3.1 Utangulizi ........ 38
3.2 Uongozi katika Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ........ 39
3.2.1 Ufisadi katika Uongozi ........ 39
3.2.2 Ukosefu wa Huduma za Kijamii ........ 46
3.2.3 Upendeleo katika Miradi ya Maendeleo ........ 51
3.2.4 Umaskini ........ 53
3.2.5 Kutegemea Misaada ........ 56
3.2.6 Ukiukaji wa Sheria ........ 58
3.2.7 Ufasiri wa Uongozi katika *Msimu wa Vipepeo* ........ 60
3.3 Wananchi na Uongozi ........ 60
3.3.1 Kutojali kwa Watawaliwa ........ 61
3.3.2 Wananchi na Ufisadi ........ 65
3.4 Suluhisho Lililopendekezwa ........ 66
3.4.1 Uaminifu ........ 67
3.4.2 Kiongozi Anayewapa Uwezo Anaowaongoza ........ 68
3.4.3 Kiongozi Mkakamavu ........ 69
3.5 Hitimisho ........ 70
**SURA YA NNE ........ 71**
**TASWIRA YA DINI KATIKA RIWAYA YA *PARADISO* ........ 71**
4.1 Utangulizi ........ 71
4.2 Umuhimu wa Dini ........ 71
4.3 Uongozi wa Dini ........ 72
4.3.1 Uongozi wa Kanisa na Siasa ........ 76
4.3.2 Unafiki Kanisani ........ 80
4.4 Uozo Kanisani ........ 85
4.4.1 Kuabudu Pesa ........ 85
4.4.2 Ubaguzi ........ 86
4.4.3 Uzinzi ........ 87
4.4.4 Biashara Haramu ........ 92

4.4.5 Ufisadi ........ 93
4.5 Mchango wa Wafuasi ........ 94
4.5.1 Miujiza ........ 94
4.6 Suluhu Lililopendekezwa ........ 96
4.6.1 Kiongozi Anayewajali Wengine ........ 96
4.6.2 Kiongozi Anayewachunga Anaowasimamia (Kondoo) ........ 97
4.6.3 Kiongozi Mfanyakazi ........ 98
4.6.4 Kiongozi Mwema huwa Tayari Siku Zote ........ 100
4.7 Hitimisho ........ 102
**SURA YA TANO ........ 104**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 104**
5.1 Utangulizi ........ 104
5.2 Muhtasari wa Utafiti ........ 104
5.3 Matokeo ya Utafiti ........ 106
5.4 Mchango wa Utafiti ........ 110
5.5 Hitimisho ........ 110
5.6 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye ........ 111
MAREJELEO ........ 112

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Danga** Katika utafiti huu, danga imetumika kumaanisha huduma, rasilmali na chochote kilicho bora nchini ambacho kinatumiwa na wachache walio mamlakani.

**Ndani Nje** Huu ni mtazamo unaokisiwa kuchukuliwa na waandishi wa riwaya mpya ambao wanayaangalia matatizo ya uongozi kwa kuangazia jamii yenyewe. Kwamba jamii inafaa kuuangazia udhaifu uliopo badala ya kulaumu athari kutoka nje kwa matatizo yanayoikumba.

**Nje Ndani** Mtazamo huu ulichukuliwa na waandishi wa hapo awali baada ya mataifa mengi barani Afrika kupata uhuru ambapo matatizo yalionekana kana kwamba yalitokana na ukoloni. Kwamba hata viongozi waliochukua hatamu za uongozi waliendelea kutumia mifumo iliyowachwa na wakoloni kuendeleza uongozi mbaya.

**Paradiso** Tunaangalia paradiso kuwa mahali pazuri ambapo kuna upendo, msamaha na kuwajali wengine. Ni mahali ambapo wanaoteseka wanaweza kukimbilia huku wakiwa na imani kwamba watapata usaidizi. Hata hiyvo katika riwaya ya *Paradiso*, tunashuhudia kinyume cha haya. Badala ya kuwa paradiso, kanisa ambayo inafaa kuwa paradiso hapa duniani imekuwa ni mahali pa fujo, vita, utengano na maovu mengine mengi.

**Riwaya Mpya** Dhana hii inarejelea upya wa mawazo ya waandishi wa riwaya ya kipindi cha miaka ya 2000 katika juhudi za kukabiliana na changamoto za uongozi. Katika kila kipindi cha kihistoria kuanzia kabla ya uhuru,

baada ya uhuru hadi sasa, waandishi wamekuwa wakitoa mapendekezo kuhusu tatizo la uongozi barani.

**Riwaya ya Kisasa** Hii ni riwaya ambayo imeandikwa kuanzia mwaka wa 2000.

**Uongozi** Utafiti huu unakisia kwamba uongozi bora lazima uwashirikishe watawala na watawaliwa. Kwamba kila kikundi kina nafasi yake katika uongozi na kwa hivyo jukumu la watawaliwa haliishi pindi tu wanapowachagua viongozi lakini wanafaa kuhakikisha kuwa viongozi wanawajibika kwa kila hatua katika uongozi wao.

# MAELEZO YA AKRONIMU NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AAT** | The African Association of Tanganyika |
| **ADC** | African Divine Church |
| **KANU** | Kenya African National Union |
| **NCCK** | National Council of Churches of Kenya |
| **TANU** | Tanganyika African National Union |
| **TY** | Tafsiri Yangu |
| **k.m** | Kwa mfano |
| **k.v.** | Kama Vile |
| **khj** | Kama hapo juu |
| **Mh** | Mhariri |
| **nk.** | Na Kadhalika |
| **uk.** | Ukurasa |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii imeangaazia usuli wa utafiti, suala la utafiti, sababu za kuteua mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, misingi ya nadharia, upeo wa utafiti, yalioandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Shabaan Robert ni mmoja wa waandishi maarufu wa Kiswahili waliokuwa wa kwanza kutumia fasihi kuangazia suala la uongozi. Maoni yake ya kisiasa na kijamii yalitokea wakati mmoja na malengo ya muungano wa kwanza wa umma wa waafrika – *The African Association of Tanganyika* (AAT) uliobadilika na kuwa chama cha kisiasa cha *Tanganyika African National Union* (TANU) ambacho kiliongoza nchi ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961. Huku akijihusisha na mawazo ya kijamii na ya kisiasa ya wasomi kuhusu maendeleo ya baada ya ukoloni, Shabaan Robert alieleza maazimio yao ya utu, ya kumaliza ukoloni na kujenga jamii iliyojikita katika haki na usawa. Tunaona mawazo yake katika riwaya ya *Adili na Nduguze* kuhusu jamii iliyo na usawa na huru kutoka kwa minyororo ya ukoloni na tamaduni zilizopitwa na wakati na ambazo zinamweka mtu kuwa msingi wa maendeleo ya nchi - yanafanana na mawazo makuu ya ujamaa. Kupitia haya ni dhahiri kwamba mwandishi huyu, kupitia kwa kazi zake za kifasihi, alihusika moja kwa moja na maendeleo ya kisiasa na ya kifalsafa ya nchi yake. Robert aliukashifu utawala wa kikoloni na kuonyesha mgogoro uliokuwepo baina ya wakoloni na Waafrika ingawa alifanya hivyo kwa kutumia tashtiti na mafumbo katika kazi zake. Kwa mujibu wa Mumbo (2018), Robert aliyafanya haya ili kuepuka rungu la dola.

Mbatia (2016) anasema kwamba "katika historia ya uandishi wa kinathari wa Kiswahili, *Lila na Fila* ni kazi ya kwanza ya kibunilizi yenye ujumbe wa kisiasa ulio wazi na inayotabiri majilio ya ujamaa. Tukio hili la kihistoria lilikuja kuwa mada kuu ya riwaya pevu katika miaka ya sabini" (uk. 109). Kwa hivyo tunaona kwamba riwaya ya Kiswahili imekuwa ikijihusisha na masuala ya uongozi barani tangu wakati wa ukoloni.

Kwa mujibu wa Wamitila (1997), riwaya za Kiswahili kwa muda ziliangazia masuala ya kijamii kama vile utovu wa nidhamu, maisha ya mijini, uchawi na kadhalika. Ni riwaya chache zilizoshughulikia masuala ya kisiasa akitaja riwaya kama vile *Kaburi bila Msalaba* na *Kikulacho ki Nguoni Mwako* ambazo ziliangazia vita vya MauMau vya uhuru. Hata hivyo riwaya zilizoandikwa miaka ya 1980 zilihusisha matatizo ya uongozi na yale yaliyokuwa yakiendelea katika jamii. Katika kipindi hiki tunapata riwaya ya *Mafuta* (Mkangi, 1984) iliyoangazia tofauti za kitabaka huku mwandishi akidhihaki uongozi wa Afrika na kuwatetea wanyonge walio wengi. Nayo riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini* inaangazia ufisadi ambapo wachache walio katika uongozi wanakula jasho la walio wengi.

Waandishi hawa wa riwaya mpya za Kiswahili, yaani riwaya zilizoandikwa kuanzia mwaka wa 2000, wanakisiwa kuchukua mwelekeo tofauti na waandishi wa hapo awali. Waandishi hawa, kando na kuangazia matatizo ya uongozi wa kisiasa, wanachukua mwelekeo mpya wa kuangazia asasi nyingine za kijamii kama inavyodhihirishwa na watafiti mbali mbali. Ngetich (2014) aliangazia udhalimu unaowafanywa na viongozi wa makanisa dhidi ya wafuasi kwa kurejelea riwaya ya *Paradiso.* Ngetich anaonyesha jinsi viongozi hao hutumia dini kuwahadaa wengine huku injili ikitumiwa kuwatapeli waumini ili wawatajirishe viongozi. Naye Yenjela (2017), akizungumzia kuhusu historia ya nchi ya Kenya kupitia kwa riwaya, ametafitia riwaya ya *Wimbo Mpya* ya Mbatia (2004) kuhusu mchango wa wapiganaji wa Mau Mau kwa uhuru wa nchi hii.

Wesonga, Ambuyo na Mzungu (2020) wametafitia masuala ya mazingira kwa kurejelea riwaya za *Tikitimaji* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Katika utafiti wao wanasema kuwa ingawa kwa miaka mingi masuala ya mazingira yamehusishwa na sayansi haswa katika kutoa takwimu kamilifu kuhusiana na masuala ya mazingira, fasihi inaendelea kuchukua dhima mpya katika jamii inayozidi kukua kiteknolojia. Sanja na Mukwhana (2015) wametafitia kuhusu mabadiliko yanayoendelea kushuhudiwa katika asasi ya ndoa kwa kurejelea riwaya ya *Paradiso* na ile ya *Kala Tufaha.*

Waandishi hawa ambao wana jukumu kubwa la kuielemisha na kuipa jamii mwelekeo wanazidi kutoa maoni yao kuhusu masuala mbali mbali yakiwemo ya uongozi kama mchango wao katika jamii. Kama anavyosema Khamis (2012, uk. 15):

> Kimaudhui, riwaya hii mpya ina mtazamo wa kuyaona matatizo yetu kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Nje inachukuliwa kuwa ni pembejeo tu la matatizo yote. Wakati mwingine, baadhi ya watunzi wa riwaya hii hujitoa kwa kiasi fulani katika kushughulikia matatizo ya ndani ya nchi na kutazama matatizo ya kidunia na kimataifa. Pengine haya yalishughulikiwa kwa kiasi na wanariwaya wa Kiswahili hapo zamani, lakini si kwa msisitizo na vuguvugu hili la sasa. Katika mifano yote ya riwaya hii mpya, unaziona na kuzisikia hasira kali za waandishi wake ambao wana tamaa kwamba watawakoleza wasomaji wao woga na hasira, wanapoikumbusha hadhira kitisho wanachokijua.

Anavyosema Khamis (2012) hapa ni kuwa waandishi wa riwaya mpya wanaitaka jamii iyaangalie upya matatizo haya ambayo yameendelea kuikumba tangu miaka ya ukoloni hadi sasa. Ni kana kwamba riwaya hizi zinadai kuwa miaka mingi baada ya mataifa haya kupata uhuru, ni muhimu yajiangazie kwa undani na kuona ni vipi wanajamii wanaweza kujikwamua na kutoa suluhu la matatizo yao. Zinavyodai, haitoshi tu kulaumu athari kutoka nje, yaani ile ya wakoloni, bali pia ni vyema jamii kujiangazia wenyewe (mtazamo wa ndani) kama njia moja ya kutoa suluhu kwa changamoto zinazoikumba. Katika kufanya hivi ni muhimu jamii ijitathmini yenyewe katika juhudi

za kujikomboa na kujikwamua, jambo linaloungwa mkono na Edi (2007, uk. 122) anaposema:

> Hatua ya kwanza katika ukombozi wa Afrika ni ile ya Afrika kujitathmini yenyewe, yaani iyaangalie matatizo yake kupitia kwa macho ya kiafrika na kuyaweka wazi kwani ilivyo sasa kitamaduni, kimaadili na kiroho bara hili limepoteza mwelekeo (TY).

Kama njia ya kujitathmini, riwaya mpya inaangazia sio tu uongozi wa kisiasa bali pia uongozi katika asasi nyingine za kijamii. Tofauti na tafiti nyingine, kazi hii imeangazia asasi ya dini sawia na ile ya kisiasa. Kazi hii imelinganisha uongozi ulivyo katika asasi hizi mbili ili kuona kama dini ambayo ni dhamira ya jamii inaweza kuegemewa kurekebisha asasi ya kisiasa.

### 1.3 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza suala la uongozi wa kisiasa na kidini barani Afrika hasa kwa kujikita katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa katika miaka ya 2000 hasa kwa kujikita katika riwaya mbili, *Msimu wa Vipepeo* ya Kyalo Wadi Wamitila (2007) na *Paradiso* ya John Habwe (2010). Aidha, utafiti ulihakiki namna uongozi unavyojitokeza katika riwaya hizi. Suala la uongozi limeshughulikiwa na waandishi wengi wa riwaya. Hata hivyo, nyingi za kazi zilizoandikwa baada ya uhuru wa nchi mbalimbali ziliona ukoloni na ukoloni mamboleo ulioendelezwa na viongozi waliochukua hatamu baada ya ukoloni kama chanzo cha uongozi mbaya na ambao umeendelea kuliathiri bara la Afrika hadi sasa.

Hata hivyo baadhi ya waandishi wa riwaya mpya wamechukua mwelekeo tofauti kuhusu tatizo hili. Tofauti na riwaya za hapo awali zilizoliona suala hili kwa mtazamo wa “nje-ndani”, inadaiwa kwamba riwaya za sasa zimechukua mwelekeo mpya wa kuliangalia suala la uongozi kwa mtazamo wa “ndani-nje”. Waandishi hawa wanaona

kuwa ni muhimu kwa jamii kujitathmini kwa undani ili kupata suluhu ya tatizo hili linaoendelea kuiathiri.

Utafiti huu basi unaangazia suala hili kutoka kwa mtazamo huo wa ndani nje na uliazimia kuchunguza misingi na mihimili hiyo ya mtazamo wa "ndani nje" na namna unavyoathiri suala la uongozi katika mataifa ya Afrika.

### 1.4 Sababu za Kuteua Mada ya Utafiti

Mada hii ya utafiti iliteuliwa kwa sababu kadhaa. Kufikia sasa, kutokana na kudurusu kwa mtafiti kuhusu suala hili la uongozi, ingawa watafiti kama Ngetich (2014), Sanja na Mukhwana (2015), Gromov (2014), na Yenjela (2017) wamezungumzia suala la dini na riwaya za kiafrika, hakukuwa na kazi ama utafiti wowote wa fasihi ambao unaangazia suala la uongozi wa kisiasa na kidini kwa kurejelea riwaya zilizoandikwa miaka ya 2000 kwa mtazamo wa "ndani-nje. Sababu ya pili ni kuangazia namna uongozi wa kisiasa ulivyo, miaka mingi baada ya kupata uhuru, ili kuona jinsi unavyochangia kuimarika au kudhoofika kwa jamii kama inavyobainika katika riwaya mpya ya miaka ya 2000.

Aidha, demokrasia ni mojawapo ya ustaarabu unaotumiwa katika nchi mbali mbali katika uongozi ambapo wananchi hupewa nafasi ya kuwachagua watu ambao watawawakilisha. Kutokana na haya ni wazi kwamba viongozi huchaguliwa na wananchi na kwa hivyo ni muhimu kuangalia jinsi wanavyoshiriki katika mchakato huu wa uongozi.

Sababu nyingine muhimu ni kuangazia jinsi watunzi wa riwaya wanavyosawiri uhalisia wa nchi zao. Pia, utafiti uliangazia asasi ya dini ili kutathmini mchango wake katika suala la uongozi, hususani tunapoiegemeza na mtazamo huo wa "ndani-nje.". Dini imepewa wajibu mkubwa katika jamii kwani ndio dhamiri ya jamii na kwa hivyo,

inategemewa kutoa mwongozo kuhusu mambo mbali mbali na hasa pale viongozi wanapopoteza mwelekeo. Kwa hivyo ni muhimu kuichunguza ili kuona kama inaweza kuutekeleza wajibu huu.

## 1.5 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

i. Kufafanua taswira ya uongozi barani Afrika kwa kuchunguza matatizo katika asasi ya dini na siasa kama inavyodhihirika katika riwaya zilizoteuliwa za *Msimu wa Vipepeo* na *Paradiso*.

ii. Kutathmini mchango wa wananchi katika uongozi kwa mujibu wa riwaya zilizoteuliwa.

iii. Kuchunguza mtazamo wa ndani nje na mapendekezo yanayotolewa katika riwaya teule kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto za uongozi.

## 1.6 Nadharia Tete

i. Uongozi ni changamoto kuu inayokabili asasi za kisiasa na kidini katika jamii za kiafrika.

ii. Wananchi wanaotawaliwa wamechangia uongozi duni katika jamii.

iii. Riwaya mpya zimejikita katika mtazamo wa ndani nje kukabiliana na changamoto za uongozi mbaya.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhistoria mpya. Nadharia ya uhistoria mpya iliasisiwa miaka ya 1980 na kushika nguvu katika miaka ya 1990 kupitia kwa kazi za mtalaam Stephen Greenblatt. Tofauti na uhakiki wa historia ambao ulijikita katika kuangalia jinsi matini inavyoakisi wakati ilipoandikwa, nadharia hii hutathmini jinsi

matini inavyoathiriwa na wakati mahsusi ilipoandikwa. Habib (2005) anasema kuwa wananadharia hawa, huona kazi za kifasihi kuwa zao la hali zilizoandikiwa kuliko zilivyo zao la fikra za mwandishi. Wananadharia wa uhistoria mpya huona kazi za fasihi kama zinazoleta uwiano badala ya kuiga matendo ya binadamu, na kutokana na haya wanaziona kazi za fasihi kama zinazounda badala ya kuakisi kipindi maalum. Kutokana na haya, riwaya zilizoteuliwa ziliangaziwa kwa jinsi waandishi wanavyojitahidi katika kuunda jamii mpya sio tu katika siasa bali pia katika dini.

Nadharia hii hushughulikia maana katika matini kwa kuangalia kazi hiyo kupitia kwa mfumo wa mawazo yaliyoko katika kipindi fulani cha kihistoria. Kwa mujibu wa nadharia hii, historia si upangaji wa matukio tu bali ni maelezo changamano ya uhalisia wa ubinadamu na mabadiliko ya mawazo yanayoaminiwa. Huenda kazi za kifasihi zitueleze au zisitueleze ukweli wa ulimwengu lakini zitatuambia kuhusu jinsi watu wanavyofikiria katika kipindi fulani. Kwa mfano, kazi maalum ya kifasihi ina uwezo wa kueleza mawazo kuhusu mpangilio wa jamii, dhuluma, miiko na mengineyo mengi katika jamii husika. Kwa mujibu huu, riwaya zilizoshughulikiwa zilichunguzwa kuona jinsi zilivyoangazia suala la uongozi kwa mtazamo mpya yaani ule wa ndani nje kama lilivyozungumziwa na mwandishi Khamis (2012). Mwandishi huyu anasema kuwa kwa muda mrefu, riwaya ziliangalia suala la uongozi mbaya kama lililohusisha athari kutoka nje. Riwaya mpya katika kazi hii zikiwakilishwa na *Msimu wa Vipepeo* na *Paradiso* zilitumiwa kuangazia mabadiliko ambayo yanaangazia udhaifu uliomo katika jamii hasa katika asasi muhimu za dini na siasa. Hali ilivyo katika asasi ya siasa iliangaziwa ambapo tulichunguza vitendo vya viongozi na jinsi vinaathiri jamii. Kwa upande wake, dini ambayo inafaa kuirekebisha jamii ilichunguzwa kuona ikiwa inazingatia maadili katika uongozi wake.

Wanauhistoria mpya hujishughulisha na jukumu la kisiasa la fasihi na pia dhana ya mamlaka. Wanajishughulisha na itikadi au uumbaji wa kijamii ambao umo katika kila kipindi cha kihistoria. Wananadharia hawa husisitiza kwamba itikadi hujitokeza katika kazi za kifasihi na diskosi. Pia, wao hujikita katika uhusiano ulioko kati ya matini na muktadha ilimoandikiwa. Wanavyodai kazi ya kifasihi zina maana nyingi, kila maana ikiathiriwa na pia kuathiri muktadha wa kijamii ilimoandikiwa. Nadharia hii inaendelea kusema kwamba matini hazitokani na ombwe tupu bali huzalishwa kutoka kwa hali maalum za kihistoria na kijamii. Inaendelea kwamba ikiwa tunataka kuelewa jinsi fasihi na matini nyingine zinavyoathiriana katika kipindi maalum cha kihistoria, basi ni lazima tuziangazie matini zote kwa makini. Kwa utaratibu huo, riwaya zilizoteuliwa zilihusishwa pia na matini nyinginezo, za kifasihi na zisizokuwa za kifasihi, zilizoandikwa nyakati hizo pia ili kujenga nudhumu nzima ya uhistoria wa kipindi hicho. Matini nyinginezo zinazozungumzia hoja sawa na zile zilizomo ndani ya riwaya mbili za utafiti zilijumuishwa kama sehemu moja ya uhistoria mpya uliomo ndani ya riwaya za *Msimu wa Vipepeo* na *Paradiso*.

Nadharia hii imetumika kubaini ni nani anayepewa mamlaka katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* na ile ya *Paradiso* na jinsi anavyotumia mamlaka hayo. Mamlaka yanahusiana kwa karibu na uongozi na kwa hivyo tuliangalia jinsi aliye na mamlaka katika ngazi mbali mbali za jamii anayatumia ama kuimarisha au kukandamiza asasi hiyo anayoiwakilisha. Nadharia hii pia ina uhusiano wa karibu na nadharia ya Umarx kwa vile huwa inaangazia mahusiano katika jamii hususani mivutano ya kitabaka baina ya wenye nyenzo za kuzalisha mali na wasio nazo katika kazi za kifasihi. Hata hivyo tofauti na nadharia ya Umarx, nadharia ya uhistoria mpya huangazia jinsi mamlaka yalivyo katika jamii. Nadharia hii hulenga kuelewa kazi za kifasihi kwa kuangazia

muktadha wake wa kihistoria na pia kuelewa historia ya kitamaduni na kiakili kupitia kwa fasihi.

Kutokana na haya, nadharia hii iliufaa utafiti huu katika kuelewa mabadiliko yanayoendelea kujitokeza katika riwaya mbili za utafiti. Jamii yoyote ile huwa inashuhudia mabadiliko katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Kwa vile mwandishi huathiriwa na jamii anapoitunga kazi yake, basi taswira za mabadiliko haya sharti zijitokeze katika kazi zake. Kwa hivyo katika kazi zilizoteuliwa nadharia hii ilitumiwa kuchanganua na kuchunguza mabadiliko yaliyoko na jinsi yanavyosawiriwa na waandishi husika. Pia ilitumiwa katika uchanganuzi wa data kubainisha changamoto za uongozi katika ngazi za kisiasa na kidini.

**1.8 Upeo wa Utafiti**

Utafiti huu ulichunguza suala la uongozi katika jamii kwa kuangazia asasi ya siasa na dini. Kazi hii ilijikita katika kuchambua riwaya za *Msimu wa Vipepeo* (K. W. Wamitila) na *Paradiso* (John Habwe). Katika kuzichambua asasi hizi, tuliangazia suala la uongozi uwe ni uongozi bora au mbovu linavyojitokeza katika asasi hizi hasa kwa kuzingatia mtazamo wa ndani nje. Kando na kuangalia matatizo yanayotokana na uongozi mbaya, kazi hii pia iliangalia suluhu linalopendekezwa na waandishi katika kukabiliana na matatizo yaliyoko katika jamii. Riwaya hizi zote zimeandikwa katika miaka ya 2000 na hivyo basi zinasaili kipindi hiki maalum cha kihistoria. Vile vile, utafiti huu ulifanyika kwa maktaba ambapo mtafiti alizuru maktaba ya Margret Thatcher katika Chuo kikuu cha Moi, maktaba ya Jomo Kenyatta Memorial Chuo Kikuu cha Nairobi na pia maktaba ya kitaifa (National Library Services) mjini Eldoret. Pia mtafiti alitoa makala mengi yaliyoandikwa kuhusu suala la utafiti kutoka kwa mtandao.

**1.9 Yalioandikwa Kuhusu Mada**

Katika sehemu hii, mtafiti aliangalia riwaya kadhaa na tafiti mbali mbali za riwaya na jinsi ambavyo zimeangazia suala hili la uongozi barani Afrika. Hii ni kwa sababu ingawa waandishi wanaandika kuhusu matatizo ya nchi zao binafsi, matatizo haya yanafanana, kwani nyingi za nchi hizi zilipitia tajriba sawa chini ya wakoloni na vile vile baada ya uhuru.

Mwanzoni, fasihi ya Afrika ilikuwa chombo cha kusherehekea umaarufu wa historia ya Afrika, baadaye ilitumiwa kupigana vita dhidi ya ukoloni, kwa sasa inatumiwa kama silaha ya kuonyesha kutoridhika kwa mataifa ya kiafrika baada ya ukoloni (Kehinde, 2005). Baada ya kupata uhuru, fasihi iliangazia masuala ya kijamii kama vile dini, maadili na hata mapenzi miongoni mwa mengine. Kwa mujibu wa Mulokozi (2012), hizi ndizo dhamira zilizoandikiwa zaidi na waandishi wa riwaya za Kiswahili katika miaka ya 1960 na mwanzo wa miaka ya 1970. Hata hivyo, kutokana na kudorora kwa uchumi katika miaka ya 1970 na 1980, kulizuka waandishi ambao walianza kuangazia masuala ya kupoteza imani kwa viongozi ambao walichukua mahala pa wakoloni na kuendelea kuwanyanyasa waliotawaliwa. Mulokozi (2012) anazitaja riwaya kama vile *Ubeberu Utashindwa, Mzalendo,* na *Kaburi bila Msalaba* miongoni mwa zingine. Hata hivyo wengi wa waandishi wa riwaya hizi walilaumu wakoloni kama sababu ya kuendelea kudorora kwa nchi za Kiafrika. Kwa kiwango kikubwa, huu ndio mtazamo uliochukuliwa na waandishi na wahakiki wa awali ambao waliyaona matatizo ya serikali huru za Kiafrika yakitokana na ukoloni na ukoloni mamboleo.

Waandishi wa riwaya barani Afrika wameendelea kupigana na suala hili ijapokuwa mielekeo ambayo wamechukua imeendelea kubadilika katika vipindi tofauti vya kihistoria. Waandishi wengi wameandika kuhusu kunyanyaswa kwa wachochole kwanza na wakoloni na baadaye wakoloni mamboleo, yaani na viongozi waliochukua

mahala pa wakoloni baada ya mataifa haya kupata uhuru. Wananchi wamepoteza matumaini na viongozi hawa ambao mwanzoni walionekana kama ambao watawainua kutoka kwa minyonyoro ya wabeberu lakini hili halikuwa (Olowonmi, 2008; Pantengouh, 2005; Kehinde, 2005; Ntarangwi, 2007).

Akizungumzia kuhusu umuhimu wa mwandishi, Nyamndi (2006) anasema kuwa mwandishi sio tu mwalimu kwa kuzingatia maana asilia ya neno hili bali pia ni mtabiri wa jamii yake ambaye hutambua na kusisitiza udhaifu wa jamii yake. Anaendelea kutoa rai yake kuwa tangu kuandikwa kwa riwaya maarufu ya Things *Fall Apart* (Chinua Achebe), msimamo ambao umetawala uandishi ni kuwa shida za bara la Afrika zinatokana na ukoloni. Kazi hii inaonyesha mkondo ambao umetawala uandishi wa riwaya nyingi tangu mataifa mbali mbali ya Afrika kupata uhuru. Pia inazungumzia kuhusu jukumu la mwandishi la kutambua udhaifu wa jamii yake kuitabiria na kuielimisha jamii yake majukumu ambayo yanadhihirishwa na kazi zilizoteuliwa.

Naye Dasylva (2003) anasisitiza umuhimu wa jukumu hili la mwandishi akisema kuwa mwandishi anaweza kuwa kigeugeu kulingana na mtazamo wake na muktadha wa utunzi wa kazi yake au utambuzi. Kiakademia, yeye ni mtaalam katika nyanja maalum ya maarifa. Lakini la muhimu zaidi ni kuwa mwandishi ni mwanajamii anayeshiriki yale yanayoendelea katika jamii yake. Kwa hivyo mwandishi ni msanii wa kweli kwani wakati wote anabuni kazi zinazojibu maswali nyeti yanayoikabili jamii yake kwa wakati uliopo. Dasylva akimnukuu Novikov anasema:

> Dunia iko sawa kabisa na jinsi alivyoisaili katika kazi yake. Mwandishi anamsihi msomaji auone ulimwengu na kuamua matukio kama mwandishi anavyoyaona na kwa kutumia ukweli wake. Katika kazi yake, mwandishi humshawishi msomaji na ubora wa mafikirio na taswira yake na hutaka kuathiri fikra na hisia za msomaji (Novikov, 1982, uk. 12). (TY).

Olowonmi (2008) anasema kuwa hamu ya mwandishi barani Afrika ya kuwa na uongozi bora unaozingatia demokrasia haitingisiki. Anaongeza kwamba kiini cha kuelezea kukosa matumaini ni ile hamu ya kuwa na viongozi ambao watakuwa na uadilifu na watakaoongoza serikali inayowashughulikia wengi. Hili linaonyeshwa na matumizi ya taswira za uongozi mbaya, kutengwa na kuwepo kwa wananchi waliopoteza imani. Anasema kuwa kati ya tanzu za fasihi, riwaya imejitokeza kama chombo muhimu cha kuzishughulikia changamoto zinazohusiana na uongozi barani. Utanzu huu unampa mwandishi uhuru wa kuyaelezea mambo kwa njia iliyo na uhalisia wa hali ya juu.

Kehinde (2008) anakubaliana na haya akidai kwamba tofauti na waandishi wa magharibi, waandishi wa bara la Afrika ni wasanii ambao wamejitolea kwa jamii. Waandishi hawa wakati wote wamekuwa wakiangazia suala linaloendelea kusumbua la ukosefu wa uongozi bora wa kisiasa katika mataifa yao binafsi. Waandishi hawa wanaonyesha kwamba njozi za uhuru katika nchi hizi zimetoweka na badala yake wananchi wamekosa matumaini. Kwamba nia ya viongozi ilikuwa tu kuchukua nafasi zilizowachwa na wakoloni bila kuunda upya miundo ya kisiasa, kijamii na kitamaduni iliyoachwa na wakoloni.

Pöysä (2011) anakubaliana na mtazamo huu kuhusu waandishi wa kiafrika akisema kuwa riwaya za kiafrika huangazia mataifa huku wahusika wakiwakilisha nguvu za kijamii. Anasema kuwa katika riwaya za usasa baadaye, jukumu la wahusika wakuu linaangaziwa. Anaendelea kuwa katika riwaya za kiafrika ule ubinafsi ulioko katika riwaya za kimagharibi haupo na kwamba riwaya hizi zina uhusiano wa karibu na yale yanayoendelea katika jamii za waandishi. Toni ya kisiasa inayoshuhudiwa katika riwaya hizi inahusiana na jukumu la mwandishi. Waandishi wengi wanajishughulisha na yanayoendelea katika jamii zao na huchukua jukumu la kijamii. Anasema kwamba

mnamo mwaka wa 1965, mwandishi maarufu Chinua Achebe aliandika kwamba "mwandishi hawezi kujiepusha kutoka kwa jukumu la kuelimisha na ufufuo ambalo lazima lifanywe. Jameson (1986, uk. 81) anasema kuwa waandishi kama vile mwandishi wa Kenya Ngugi wa Thiong'o na mwenzake wa Senegal Sembene Ousmane wakiandika baada ya uhuru wa nchi zao:

> Wana hamu ya mabadiliko ya ufufuo wa kijamii ambao bado haujapata mawakala wa kuuendeleza. Anaendelea kuwa tatizo hili linasababishwa wakati unyanyasaji unatokana na jamii – kwamba hapo awali, adui yaani mkoloni aliwakilishwa kwa urahisi kwani alizungumza lugha tofauti, alikuwa na sura tofauti na alikuwa na nafasi maalum katika jamii. Kwa hivyo waandishi hawa wanaona kuwa ni jukumu lao kuzifahamisha jamii zao na/au kuwapa maoni mbadala kuhusu hali zao (TY).

Kazi hii inazua suala muhimu katika fasihi, lile la wahusika. Kwamba katika kazi za kifasihi, mwandishi hutumia wahusika kuendeleza wazo lake na wakati mwingi anatumia wahusika walio na sifa za kawaida za binadamu na kwa hivyo inakuwa rahisi kwa hadhira kujihusisha nao.

Suala jingine ambalo limeangaziwa na waandishi na linaloathiri mataifa ya kiafrika ni lile la tabaka. Katika utafiti wake wa riwaya ya Meja Mwangi, Kehinde (2004) anasema Kenya ya baada ya uhuru inakumbwa na tatizo tofauti, lile la utabaka ambalo limeibua ufa mkubwa kati ya wenye mali na wachochole. Kenya ya sasa inashuhudia sio tu kukatizwa tamaa kwa maskini waliotumai kuwa na maisha bora baada ya uhuru lakini pia kuzidi kutumbukia katika umaskini na kunyanyaswa. Anaendelea kusema kuwa matarajio ya watu hayakutimia. Hali ya kisiasa na kijamii imejaa ukosefu wa matumaini. Aidha, Tarmakin (1978:314) anasema uhuru ambao ulipatikana kwa mateso mengi umegeuka na kuwa laana kwa sababu:

> Wakenya wengi walio katika tabaka la chini wanaishi katika hali ya umaskini…maisha na umasikini wa wanaoishi mijini yanaendelea kutatizwa na hali mbaya ya mahala pa kuishi na ukosefu wa huduma. Unyonge wa maskini nchini Kenya unaonyeshwa na maisha ya

> ubadhirifu ya mabwanyenye…hali ya kijamii na kiuchumi ya walio wengi ni ya kukatisha tamaa (TY).

Huu ndio uhalisia unaoshuhudiwa katika jamii za kiafrika ambapo wenye mali wanaendelea kutajirika huku wengi ambao hawana wakiendelea kuzama katika lindi la umaskini. Tunapata kwamba wengi wa hao walio na mali si kwamba walifanya kazi bali ni viongozi na walio katika mamlaka ambapo wanatumia nyadhfa zao kupora mali ya wananchi.

Olowonmi, Olayiwola na Olukayode (2009) wanasema kuwa mwandishi wa riwaya amechangia vilivyo katika maendeleo ya kitaifa kwa kazi zake. Ingawa wakati mwingi maoni yake na sauti yake zinakinzana na zile za mwanasiasa, kujitolea kwake kwa jamii yake kunaendelea kumpa msukumo. Anatumia usanii wake wa hali ya juu kuwatetea wasio na sauti katika jamii, yaani maskini. Wataalam hawa wanadai kuwa nyingi za matini za baada ya ukoloni ni motifu za uchungu na umaskini. Wakati mwingi mwandishi wa riwaya anatathmini ufafanuzi wa kikoloni ulioumba jamii inayoitwa taifa la Afrika. Kwa kuvuka mipaka ya vizazi vya waandishi wa kiafrika, riwaya inakuwa ishara ya kijamii inayoakisi matatizo ya jamii yake na ile ya ulimwengu kwa jumla. Katika kuangazia juu ya mchango wa mwandishi wa riwaya kuhusu matatizo yanayozuia maendeleo katika bara la Afrika, mwandishi wa riwaya zaidi ya mwandishi mwingine yeyote, amezamia katika kukashifu ufisadi, ukosefu wa maadili ya kibinafsi na udhaifu wa utawala. Kwa kufanya hivi, anatimiza changamoto alizowekewa na Achebe, kama anavyonukuliwa na Olorunleke (1999: 118) anapomwona mwandishi kama:

> Binadamu asiye wa kawaida ambaye lazima aelewe hata yale mambo madogo kuhusu ukiukaji wa haki katika mahusiano ya kibinadamu na pia kama Soyinka anapomwona mwandishi kama aliye na nguvu za kutabiri na pia anayerekodi “Desturi na matukio ya jamii yake na pia kama sauti ilio na maono katika wakati wake”. (TY).

Mawazo haya yanaonyesha umuhimu wa mwandishi katika jamii ambapo anatumia ujuzi wake kisanaa kuangazia sio tu matatizo ya jamii yake bali pia kutoa suluhu. Kama mwanajamii anashuhudia yanayoendelea na vile vile anaumia sawa na wananchi wengine na hivyo basi anaandika kama mchango wake kwa jamii.

Edi (2007), akiandika kuhusu riwaya ya *Osiris Rising* ya mwandishi Ayi Kweyi Armah, anasema kuwa kwa kuangazia matukio ya wahusika wakuu, ni wazi kwamba hatua ya kwanza na ambayo haiwezi kuepukika katika ukombozi ni "Afrika kujitathmini yenyewe". Utathmini huu unamaanisha kuwa bara la Afrika lijitazame kwa macho yake yenyewe na kwa mujibu wa hisia zake na tajriba zake za kila siku na kwa kutumia vifaa vya kiafrika. Ama kweli haitoshi tu kwa Waafrika kulihakiki bara hili ili maoni yao yawe ya kiafrika. Vifaa vya kuhakiki lazima viwe vya kiafrika. Katika kufanya hivi, maovu yanayotawala jamii za kiafrika za baada ya uhuru yatawekwa wazi. Kati ya maovu haya ni wizi, ufisadi, usaliti, mapendeleo, uharibifu wa mali ya umma, kudhoofika kwa mfumo wa elimu na mengineyo. Katika riwaya hii ni wazi kwamba ingawa bara la Afrika liko katika nafasi yake kijiografia, kitamaduni, kimaadili na kiroho, bara hili limepoteza mwelekeo. Kazi hii inaonyesha mwelekeo mpya wanaochukua waandishi wa riwaya mbili za utafiti katika kushugulikia matatizo ya bara hili. Huu ni mwelekeo wa kujitathmini na kuirai jamii iweze kutafuta suluhu badala ya kila saa kulaumu masuala ya nje.

Gromov (2014) anasema waandishi wengi wa Kiswahili katika kazi zao wanatabiri maafa makubwa ya siku za usoni-dunia kabla na baada ya kuangamia kwa ulimwengu, unaozongwa na mamlaka za kiimla, baa la njaa na umaskini.  Hata hivyo katika kazi zao wanatoa maoni yao kuhusu uwezekano wa kuwaokoa binadamu, na hivyo kuwapa wasomaji onyo kali la siku za usoni na vile vile matumaini ya siku hizo. Kazi hii inaangazia riwaya ya kisasa na mtazamo wa waandishi na suluhu wanayotoa. Kwa

waandishi, ingawa hali ni mbaya, kuna matumaini kwamba ikiwa jamii itazingatia inayoandikiwa na waandishi basi itaweza kujinusuru.

Oha (2007) anasema kuwa haja ya kuiweka wazi hali ya kuhuzunisha katika bara la Afrika imekuwa katika mawazo ya waandishi wa kisasa katika bara hili. Sauti zinazolalamikia uongozi mbaya kwa njia mbali mbali zinaongezeka. Hata hivyo, uhalisia huu unakera zaidi na waandishi wanaendelea kuuandikia. Akimnukuu Mutiso (1974), Oha (2007) anadai kuwa siasa katika fasihi ni jambo zuri kwa sababu fasihi bora katika Afrika ya kisasa hunuia "kutabiri dhana kuu za kisiasa na kijamii zitakazotumika kuelimisha vizazi vya kisasa na hata vijavyo". Siasa kwa hivyo inakuwa kifaa cha lazima katika ujenzi wa bunilizi za kisasa za Afrika. Izebaye (1979) anakubaliana na Oha akisema, "riwaya ya kiafrika imeathiriwa kwa njia ya moja kwa moja na siasa, hasa katika maelezo yake kuhusu mabadiliko kutoka kwa kutawaliwa kitamaduni hadi tashtiti za miaka ya baada ya uhuru" (uk. 23). Mwandishi huyu anadhihirisha mchango mkubwa wa riwaya katika kuangazia suala hili la uongozi na hasa katika kuelimisha jamii kwa kuipa njia mbalimbali za kukabiliana na hali hii katika vipindi tofauti vya kihistoria.

Akitafitia riwaya za mwandishi Armah, Kakraba (2011) anasema kuwa kando na ujumi wake, ni riwaya ambazo zimeundwa kuwa vifaa vya upinzani na uhuru. Zinalenga kupigana na kile Armah anachokiona kama kukiukwa kwa haki, mapendeleo na ukatili ambao umetendwa kwa miaka mingi na wageni na pia waafrika dhidi ya waafrika. Kwa hakika, uhuru katika fasihi huwapa watu, jamii na bara hili changamoto za kutambua kilicho kizuri katika urithi wao na kuwazuzua kutafuta suluhu kwa matatizo yao. Kazi hii inaonyesha kubadilika kwa uandishi wa riwaya ambapo waandishi wanaanza kuyaangazia matatizo ya ndani kwa kuangazia ndani kuliko nje. Hata hivyo tofauti na

kazi hii ni kwamba utafiti huu umeangazia zaidi asasi mahsusi za jamii na pia masuala yanayoiathiri.

Olali (2008) anaeleza jitihada za wananchi kupigana na maovu katika jamii kama vile ufisadi. Mwandishi anatuonyesha hali ilivyo chini ya uongozi wa Maotad ambapo ufisadi, umaskini, uporaji wa mali miongoni mwa mengine ndio hali ya kawaida. Ili kupigana na hali hii, viongozi wa vyama mbali mbali pamoja na wananchi kupitia kwa Mzee Twajua wanafanikiwa kuwashawishi wananchi kuing'oa serikali ya Maotad. Na, kwa hivyo, tunaona mchango mkubwa kati ya viongozi na wananchi katika kusuluhisha matatizo ya nchi. Hata hivyo, mwandishi anatuambia kuwa suala la ufisadi bado linaendelea licha ya kuwa na viongozi wapya. Kutokana na haya, ni wazi kwamba kubadilisha viongozi peke yake hakutoshi na kwa hivyo ni muhimu kuwa na mabadiliko ya kimsingi miongoni mwa jamii ili kukabiliana na tatizo la uongozi.

Kwa mujibu wa kazi zilizoangaziwa, ni wazi kwamba suala la uongozi limeendelea kuwa kero katika nchi za kiafrika. Licha ya kuwa waandishi kupitia kwa fasihi na hasa riwaya wamekuwa wakitekeleza wajibu wao wa kukashifu maovu yanayoathiri jamii yanayosababishwa na uongozi, suala hili bado linaendelea. Wananchi katika bara hili bado wanaendelea kuishi katika umaskini uliokithiri. Waandishi wa riwaya mpya kwa sasa wamechukua mwelekeo mpya ambao utafiti huu uliangazia na kuchunguza maoni yao kuhusu njia za kukabiliana na suala hili. Asasi ya dini imeangaziwa kwa kuwa inafaa kusimamia ukweli, amani na utangamano, umoja na kuwatetea maskini na wote wanaodhulumiwa katika jamii miongoni mwa mengine. Hivyo basi ni muhimu kuichambua na kuona kama kweli wanatekeleza hayo au wamechotwa na ulimbikizaji wa mali na kutafuta mamlaka hivi kwamba jamii inabaki bila mtetezi.

### 1.10 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inaangazia maelezo kuhusu mbinu za utafiti na mbinu ambayo imetumika katika utafiti huu. Vile vile tutaangalia uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

#### 1.10.1 Mbinu ya Kithamano

Goddard na Melville (2005) wanasema kuwa kuna aina mbili kuu za utafiti, utafiti ule wa kitakwimu na wa kithamano. Ule wa kitakwimu unahusisha idadi na takwimu na unafaa zaidi katika tafiti za maabara. Yaani utafiti wa kitakwimu unatumia mbinu zinazohusishwa na tafiti zinazoshirikisha idadi na takwimu ili kubaini ukweli katika hali maalum. Kutokana na takwimu zinazotokana na aina hii ya utafiti, makisio fulani na maamuzi ya jumla yanaafikiwa. Manufaa mawili ya aina hii ya utafiti ni kuwa unahakikisha kuwa utafiti ni yakinifu na maamuzi yanaweza kuthibitishwa. Hata hivyo aina hii ya utafiti haiwezi kutumiwa kutathmini matukio maalum ya kitamaduni.

Mbinu ya utafiti wa kithamano inahusisha kufasiri matukio na hali ambayo ina umuhimu katika utamaduni. Matukio haya hayawezi kuelezwa na kueleweka kikamilifu kwa kutumia aina ya utafiti unaotumia idadi na takwimu kwa sababu maana yake inapatikana katika ishara. Mbinu hii hutumika kutafuta maana ya ishara na mawazo ya kijumla hutolewa kueleza jinsi jamii inavyouona ulimwengu. Utafiti wa kithamano unafaa katika uchambuzi wa matini za kifasihi. Hii ndio aina iliyotumika katika utafiti huu unaohusisha kutafuta maana kutoka kwa waandishi wa matini zilizochaguliwa. Kwa vile utafiti huu unahusu maoni ya waandishi kuhusu uongozi, basi utafiti wa kithamano ulifaa zaidi. Pia utafiti huu ulijikita katika kufasiri matukio, wahusika na maana kama inavyojitokeza katika matini husika. Kwa vile fasihi huakisi jamii, basi

yanayoandikwa huwa ni mambo yanayotendeka katika jamii iliyoandikiwa na waandishi katika kipindi maalum cha wakati.

### 1.10.2 Uteuzi wa Sampuli Kimaksudi

Utafiti huu uliteuwa kimaksudi riwaya mbili za *Msimu wa Vipepeo* (2007) na *Paradiso* (2010). Uteuzi huu ulifanywa baada ya kusoma riwaya kadhaa zilizoandikwa katika miaka ya 2000 na waandishi mbalimbali zikiwemo za *Wimbo Mpya* (Mbatia, 2000), *Msururu wa Usaliti* (Mbatia, 2010), *Mafamba* (Olali, 2008), *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003), *Safari ya Lamu* (Habwe, 2011), *Maisha Kitendawili* (Habwe, 2000), *Cheche za Moto* (Habwe, 2008), *Fumbo la Maisha* (Habwe, 2009), *Dharau ya Ini* (Wamitila, 2008) na *Musaleo* (Wamitila, 2004).

Uteuzi wa kimaksudi wa riwaya ya *Paradiso* unatokana na kuangazia asasi ya dini kwa undani huku ile ya *Msimu wa Vipepeo* ikizungumzia asasi ya kisiasa katika kipindi hiki maalum cha kihistoria. Mwandishi katika riwaya hii anazungumzia kipindi maalum yaani miaka 39 tangu nchi kupata uhuru. Kwa hivyo mtafiti alikusanya data kithamano ambayo inagusia suala hili na jinsi ambavyo limeshughulikiwa na waandishi. Data iliyokusanywa inahusiana na uongozi kwa kuzingatia vipengele vya siasa na dini.

### 1.10.3 Mbinu za Ukusanyaji Data

Riwaya mbili, yaani *Msimu wa Vipepeo* na *Paradiso,* zilitumika katika kupata data ya utafiti huu kwani zimezungumzia hali ya uongozi wa kisiasa na kidini. Kutoka kwa riwaya hizi, mtafiti alipata mawazo ya waandishi kuhusu uongozi ulivyo katika jamii na mapendekezo yao kutokana na suluhu wanazotoa. Katika kufanya hivi, mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Mckee (2001) anasema matini ni kitu ambacho kutoka kwake tunapata maana. Anaendelea kusema kwamba uchambuzi wa matini ni njia

ambayo watafiti hutumia kupata habari kuhusu jinsi wanadamu wanajaribu kuuelewa ulimwengu wao.

Katika uchambuzi wa matini, mbinu kuu iliyoitumika ni ile ya uchambuzi wa yaliyomo. Krippendorff (2004) anaeleza kuwa uchambuzi huu ni mbinu ya kufasiri inayotumiwa kuchunguza data, makala yaliyochapishwa picha au matini za sauti ili kuelewa maana yake kwa watu, yale inayowezesha au kuzuia na jinsi habari inayotokana na haya hutumiwa. Haya ni maswali ambayo wanasayansi asilia hawawezi kujibu na pia kuyapata kutokana na mbinu wanazotumia.

Mbinu hii huhusisha kusoma matini zilizoteuliwa ili kutambua mada husika. Haya yanafanywa kwa kuchambua maana wazi na fiche za mwandishi, wahusika na mandhari. Kupitia kwa haya, tunapata maoni ya waandishi kuhusu uongozi ulivyo na jinsi unavyoathiri jamii kichanya au kihasi.

**1.11 Uchanganuzi wa Data**

Kwa kutumia mbinu hii, tuliweza kusoma na kuchambua masuala yote yanayohusu uongozi katika jamii kwa kuzingatia siasa na dini. Ukiongozwa na nadharia ya uhistoria mpya, utafiti huu uliangazia sio tu viongozi bali pia wanaotawaliwa wawe katika siasa au dini ili kuona mchango wao.

Nadharia ya uhistoria mpya inasema kwamba kazi za fasihi ni zao la wakati zilipoandikwa kuliko ilivyo zao la fikra ya mwandishi. Kwa kuzingatia haya mtafiti aliweza kuchambua hali ilivyo katika siasa na dini. Katika kufanya hivi utafiti huu uliweza kuangalia jinsi uongozi mbaya unavyoendelea kuathiri nchi kutokana na utumizi mbaya wa rasilmali, unyanyasaji na ufisadi miongoni mwa mengine. Vile vile, utafiti huu uliangazia uongozi bora na manufaa yake kwa nchi.

Kigezo kingine katika nadharia hii ni kile cha kulinganisha kazi za kifasihi na zile zisizo za kifasihi. Kupitia kwa haya mtafiti ameweza kuweka kazi zinazoshughulikiwa katika muktadha wa kihistoria jambo ambalo linasisitizwa na nadharia ya uhistoria mpya. Hili liliweza kuthibitisha kwamba yale waandishi wanayoyaandikia ndiyo yanayoendelea katika nchi.

Nadharia hii inazungumza kuhusu dhana ya mamlaka ambapo inaangalia nani amepewa mamlaka katika kazi za fasihi. Mtafiti aliweza kuangalia wahusika ambao wamepewa mamlaka katika asasi ya dini na ile ya uongozi na jinsi wanavyotumia mamlaka yale. Hii ni kwa sababu dhana ya mamlaka inahusiana kwa karibu na uongozi na kwa hivyo matumizi yake yana athari kwa jamii.

Pia jinsi mwandishi anavyoathiriwa na jamii anapoandika kazi yake ndivyo vivyo hivyo anavyolenga kuiathiri jamii kwa mawazo yake. Kama nadharia ya uhistoria mpya inavyosema fasihi huwa inashiriki katika kuunda jamii upya badala ya kuakisi jamii. Kwa kuzingatia haya, utafiti huu uliweza kuangazia mawazo ya waandishi katika kuunda jamii mpya.

### 1.12 Uwasilishaji wa Data

Baada ya kukusanya data, mtafiti alizipitia kwa makini huku akichunguza zile mada zinazohusiana na kuzipanga na kuhusisha kwa kijumla kama maoni ya waandishi kuhusu mada zinazoshughulikiwa yaani, uongozi katika asasi ya siasa na dini.

Tasnifu hii imepangwa kwa kuzingatia mada kuu zilizozungumziwa na riwaya, mada hizo ndizo zilizorejelewa mno katika riwaya zilizhoshughulikiwa. Aidha, mada ndogo ndogo pia zimezungumziwa mintarafu ya suala la uongozi wa kisiasa na kidini.

# SURA YA PILI

# HISTORIA FUPI YA WATUNZI NA KAZI ZAO

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, kazi hii imeangazia historia ya waandishi John Habwe na Kyalo Wamitila ambao wameandika riwaya zilizoshughulikiwa katika kazi hii. Kwa mujibu wa nadharia ya uhistoria mpya, ambayo iliuongoza utafiti huu, matini hazitokani na ombwe tupu bali huzalishwa katika hali maalum ya kihistoria. Kwa hivyo, katika kuangazia historia ya waandishi tunapata ithibati kwamba waandishi hawa ni wanajamii na kwamba wameishi katika kipindi hiki maalum cha kihistoria. Kutokana na haya wameweza kuathiriwa na yale yanayoendelea katika jamii na kwa kutumia kipawa chao kama waandishi wanatimiza jukumu waliopewa na jamii yaani kutambua tatizo lililopo na pia kama nadharia ya uhistoria mpya inavyosema kuunda jamii mpya kwa kutoa suluhu.

Pia mtafiti ameangalia dhana ya nje ndani ambayo kwa muda ilitumiwa kuangalia hali ya uongozi katika bara ya Afrika. Katika kuiangazia dhana hii, tunaangalia ni nini hasa kinachoashiriwa tunapozungumzia dhana hii ambayo inakisiwa kuchukuliwa na waandishi wa kisasa katika kuangazia tatizo la uongozi. Hatimaye, tunaangalia dhana ya uongozi ambayo ni dhana kuu iliyoshughulikiwa katika utafiti huu.

## 2.2 Historia Fupi Kuhusu John Habwe

John Habwe, ambaye ni Profesa wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, alizaliwa mwaka wa 1962 katika eneo la Emuhaya katika uliokuwa Mkoa wa Magharibi na kukulia huko. Alisomea shule ya msingi ya Ebukhaya na kisha shule ya Sekondari ya Ebwali kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Baadaye, alihudhuria shule ya upili ya Kaptet (sasa Tengecha High School) kwa masomo yake ya kidato cha tano na sita. Ni wakati akiwa katika shule ya sekondari alipoanza kuipenda sana lugha ya Kiswahili na

akasoma vitabu, magazeti na majarida mengi ya Kiswahili katika juhudi za kujiendeleza. Walimu wake pia walikipenda sana Kiswahili chake na kumhamasisha kukikuza. Habwe alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi ambako alipata shahada yake ya kwanza ya B.A Kiswahili mwaka wa 1984. Aliendelea na masomo yake na kusomea shahada ya Uzamili na kufuzu mwaka wa 1988 ambapo aliandika tasnifu yake juu ya *Amali Mtagusano wa Maana na Jamii ya Wamvita*. Alifundisha kwa muda katika chuo hicho hicho kuanzia 1995 hadi 1999 huku akisomea shahada ya Uzamifu.

Kwa mujibu wake, amebobea katika sarufi na fasihi ya Kiswahili. Mwandishi huyu anasema aliathiriwa pakubwa na wahadhiri wake kama vile Prof Mohammed Bakari, Prof Mohammed H. Abdulaziz ambaye alikuwa mhadhiri katika Chuo kikuu cha Nairobi na marehemu wawili ambao hatawasahau – Prof Jay Kitsao na Bw Kadenge Kazungu. Anasema kwamba mengi anayoyafanya ni kama walivyokuwa wanafanya. Mmoja wa wanafunzi aliowafunza akiwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi ni mtaalam wa fasihi na mwandishi maarufu Prof. Kyalo Wamitila. Baadhi ya vitabu alivyoandika ni pamoja na *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili* na *Mizungu ya Manabii*, *Darubini ya Kiswahili*, *Darubini ya Utunzi*, *Maumbile si Huja*, *Maisha Kitendawili*, *Paradiso*, *Cheche za Moto, Fumbo la Maisha, Safari ya Lamu, Ayubu Mashakani, Safina na Kima wa Ajabu, Kovu la Moyoni,* na *Sifia Mzimu*.

Uandishi wake umeathiriwa na waandishi maarufu wa ughaibuni na pia Afrika Mashariki kama vile waandishi wa Kiingereza Leo Toistory na wa Kiswahili Prof Said Ahmed Mohammed na Prof Euphrase Kezilahabi. Habwe anasema uandishi wao ulimvutia toka akiwa masomoni na hata wa leo haujakoma kumvutia. Anasema wao ni magwiji watajika wa sanaa ya kubuni. Na kila mara anapoandika huwa analenga kuvifikia viwango vyao ama hata kupita. Riwaya ya *Paradiso* ambayo inashughulikiwa katika utafiti huu ni moja ya riwaya zake. Riwaya zake nyingi ameziandika wakati nchi

ya Kenya ilikuwa inashuhudia misukosuko ya kisiasa na unafiki wa kidini. Km, riwaya ya Kovu la Moyoni iliangazia machafuko ya baada ya uchaguzi huku riwaya ya Paradiso ikiandikwa wakati asasi ya dini inaendelea kutumika kama kitega uchumi.

## 2.3 Historia Fupi ya K.W. Wamitila

Kyallo Wadi Wamitila alizaliwa mjini Machakos nchini Kenya mwaka wa 1966. Alisomea shule ya upili ya Machakos kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne na shule ya upili ya Lenana kidato cha tano na sita mwaka wa 1984 hadi 1985. Baadaye alijiunga na chuo kikuu cha Nairobi kwa masomo yake ya shahada ya kwanza na ya uzamili. Anaishi mjini Nairobi ambako yeye ni Profesa Mwandamizi wa Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Ni mwaandishi maarufu sio tu wa vitabu vya riwaya, diwani, tamthilia bali pia ameandika vitabu vya kiakademia vya fasihi. Baadhi ya riwaya alizoandika ni *Nguvu ya Sala, Bina-Adamu, Musaleo, Yatima* na *Dharau ya Ini na Msimu wa Vipepeo.* Tamthilia alizoandika ni *Wingu la Kupita, Pango* na *Sumu ya Bafe*. Diwani zake ni *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (Mh), *Tamthilia ya Maisha* (mashairi) (Mh) na *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine* (Mh).

Vitabu vingine alivyoandika ni vya kitaaluma kama vile; *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake, Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia, Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi, Kamusi ya Ushairi, Kamusi ya Methali, Kamusi ya Misemo na Nahau, Kamusi ya Tashbihi, Vitendawili, Milio na Mishanga, Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi* na *Archetypal Criticism of Kiswahili Poetry.*

Wamitila ametuzwa mara nyingi kutokana na kazi zake. Ameshinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta mara tatu kutokana na riwaya zake: *Nguvu za Sala* (2001) na *Musaleo* (2005). Riwaya inayoangaziwa katika utafiti huu, *Msimu wa Vipepeo,* pia ilishinda Tuzo hiyo hiyo katika mwaka wa 2007. Katika mwaka wa 2006, alituzwa na TUKI kwa kuwa

msomi bora wa Fasihi ya Kiswahili, Afrika Mashariki. Ni mwandishi ambaye amechangia pakubwa katika uendelezaji kiakademia wa ufunzaji wa fasihi. Katika riwaya zake, mwandishi huyu huangazia maswala ya kijamii na pia siasa.

Mucee, King'ei na Wafula (2018) wanasema kuwa Wamitila aliyesomea shahada yake ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Bayreuth nchini Ujerumani anaongozwa na imani kuwa nchi za kiafrika na ulimwengu wa tatu zinaendelea kunufaisha nchi za kimagharibi. Wanaendelea kusema Wamitila anaamini kwamba masuala kama vile utandawazi hayakuletwa kuwanufaisha Waafrika bali kutajirisha nchi za kimagharibi. Tunaona haya katika kazi iliyoshughulikiwa kwani Wamitila anairai jamii iweze kutoa suluhu ya matatizo yao badala ya kutegemea nchi za kimagharibi.

Wamitila huenda aliathiriwa katika uandishi wake na wakati alipokaa Ujerumani kwani katika mahojiano kati yake kuhusu riwaya ya *Bina-Adamu,* anasema kuwa uandishi wowote ule ni sifa ya kitawasifu. Anaendelea kusema kuwa alifika Ujerumani na kwa kiasi lazima uzoefu wake kuhusu historia ya huko na mambo mengine yalihusika hapa na pale katika uandishi wake hasa wa riwaya ya *Bina-Adamu* aliyoiandikia huko ingawa, kulingana naye, ni kwa kiasi kidogo sana. Anasema kuwa lengo la kuandika riwaya hiyo ilikuwa ni kuukosoa mfumo wa ubepari kwa jumla. Tunaona mwandishi huyu akiendelea kuukemea mfumo huu ambapo wachache wanamiliki rasilmali za nchi na njia za kutega uchumi katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* iliyoshughulikiwa katika kazi hii.

Wamitila anasema kuwa riwaya ya mwandishi yeyote yule haina budi kuakisi mazingira yake, siasa za nchi yake na mambo yanayomhusu. Na kwa hivyo tunaona kuwa aliathiriwa na jamii yake alipooandika riwaya yake ya *Msimu wa Vipepeo*. Haya yanadhihirisha yanayoshikiliwa na nadharia ya uhistoria mpya kwamba mwandishi

huathiriwa na jamii katika kazi yake na kwamba kila matini ni diskosi ya uhalisia uliopo.

## 2.4 Dhana ya Nje Ndani

Hii ni dhana ambayo inashughulikia matatizo ya uongozi kwa kuangazia nje zaidi kuliko ndani. Kwa kuzingatia dhana hii, tunaangalia masuala kama ukoloni, ukoloni mambo leo na uongozi kama mambo ambayo yameendelea kusababisha kutoendelea kwa jamii. Kwa muda mrefu, mataifa mengi ya Afrika yalikuwa chini ya uongozi wa wakoloni ambao walikuja na kusababisha mabadiliko makubwa katika mifumo ya maisha ya Waafrika. Rodney (1973) anaelezea jinsi wananchi katika nchi hizi walivyoteseka chini ya utawala wa mkoloni. Waafrika walinyang’anywa mashamba yao na kulazimishwa kukuza mazao ambayo hayakuwafaidi. Hii ni kwa sababu mazao hayo yaliuzwa na wakoloni huku wakilazimishwa kulipa kodi. Walinyang’anywa pia uhuru na hata utamaduni wao ukapotoshwa na wakoloni. Rodney anaendelea kusema kuwa rasilmali za Afrika zilitumiwa kuendeleza nchi za kigeni ambazo zilitawala nchi za Afrika na hivyo basi kushiriki katika kulemazwa kwa maendeleo barani.

Hali hii iliyoelezewa na Rodney inathibitishwa na riwaya ya *Kaburi bila Msalaba* iliyoandikwa na Kareithi (1969). Katika riwaya hii, tunashuhudia jinsi waafrika walivyonyang’anywa mashamba yao na kuachwa bila nyenzo za kuzalisha mali. Wakienda mijini kutafuta ajira wanafukuzwa kwa vile hawana pasi huku wakilazimishwa kulipa kodi kwa serikali ya mkoloni. Haya yaliwafanya waafrika kama vile mhusika mkuu Meja Blue kuwaongoza wengine kupigania uhuru. Kama Kehinde (2005) anavyotuambia, waandishi katika kipindi hiki walitumia fasihi kupigana na vita dhidi ya ukoloni. Mwandishi maarufu Shaban Robert pia alikuwa miongoni mwa waandishi walioshiriki katika kupigana na ukoloni kupitia kwa fasihi.

Nadharia ya uhistoria mpya inasema kwamba matini huzalishwa kutokana na hali halisi ya jamii katika kipindi maalum cha kihistoria. Na kwa hiyvo wakati huo, matatizo ya bara hili kwa mujibu wa waandishi yalitokana na ukoloni. Ukoloni hapa ukawa ndio dhana ya nje ambayo ilisababisha matatizo ya ndani barani. Kama anavyosema Olowonmi (2008), tangu kuandikwa kwa riwaya ya Achebe, *Things Fall Apart*, msimamo ambao ulitawala uandishi ni kwamba matatizo yanayolikumba bara la Afrika yalitokana na ustaarabu ulioletwa na nchi za kimagharibi.

Baada ya kupata uhuru, waafrika wengi walijawa na matumaini kwamba hali sasa ingebadilika na kwamba wangepata matunda ya uhuru waliopigania. Hii ni kwa sababu walipata viongozi ambao walikuwa ni waafrika wenzao. La kuvutia zaidi ni kwamba kwa kutumia demokrasia, ambayo ni mojawapo wa mifumo ya utawala iliyoletwa na ukoloni, waliweza kushiriki katika uchaguzi wa viongozi wao. Kutokana na matumaini haya makubwa, waandishi pia walipumua na wakazamia katika kuandikia masuala ya kijamii kama vile mapenzi, maadili na dini. Hata hivyo, Mulokozi (2012) na Wamitila (1997) wanasema kwamba hili lilibadilika katika miaka ya 1970 na 1980 kutokana na kuendelea kudhoofika kwa uchumi.

Katika kipindi hiki, kukazuka mwelekeo mpya wa kuangalia upya tatizo la uongozi kwa kuwaangazia viongozi waliochukua hatamu za uongozi baada ya wakoloni. Waandishi wakaanza kuangazia dhamira kama vile ufisadi, unyanyasaji wa wanyonge na viongozi waliowachagua. Wamitila (1997) anataja riwaya kama vile *Mafuta* iliyoangazia tofauti za kitabaka huku mwandishi akidhihaki uongozi na kuwatetea wayonge walio wengi. Wataalam mbali mbali wakiwemo Olowonmi (2008) na Ntarangwi (2007) wanatuambia kwamba wananchi walikosa matumaini na viongozi waliowachagua baada ya matarajio yao kukosa kutimia. Baada ya kupoteza mashamba yao kwa wakoloni na hata kupoteza maisha wakiyapigania, kuna wengi waliotarajia kwamba watarudishiwa mashamba

hayo. Rodney (1973) alielezea jinsi rasilmali za nchi za Afrika zilitumika kuendeleza mataifa ya magharibi. Na kwa hivyo ilikuwa ni matarajio ya wengi kwamba baada ya kujitawala rasilmali hizo zitatumika kuendeleza nchi mbali mbali. Lakini hili halikuwa na badala yake, viongozi waliochukua mahali pa ukoloni waliendeleza sera zilizoachwa na wakoloni na hivyo basi kuendelea kuwanyanyasa waafrika wenzao.

Wataalam wengi waliona kuwa ukoloni ulizalisha ukoloni mambo leo. Kwa mujibu wa Rodney (1973), mifumo ya ukoloni ilihakikisha kwamba nchi za kiafrika ziliendelea kutegemea mataifa ya magharibi kwa maendeleo yao. Kufikia hadi sasa, uchumi wa mataifa mengi umeendelea kutegemea mataifa ya kimagharibi ambapo mengi ya mazao yanauzwa yakiwa hayajaongezwa thamani. Hii inamaanisha kwamba yanauzwa kwa bei ya chini. Mazao hayo hayo hatimaye yanarudishwa humu barani yakiwa yameongezwa thamani na kuuzwa kwa bei ya juu ambapo ni wachache wanaoweza kumudu. Pia, mengi ya mataifa ya Afrika yameendelea kutegemea teknolojia kutoka nchi za nje ambayo wananunua kwa bei ya juu bila kusahau mikopo inayotolewa na mataifa ya kigeni ambayo inaendelea kulipwa kwa riba ya juu.

Kutokana na haya, maisha ya wanyonge yameendelea kuzama katika umaskini huku viongozi wao wakijilimbikizia mali na kuishi maisha ya ubwanyenye. Baada ya kuchukua usukani, serikali ya Rais wa kwanza nchini Kenya, Mzee Jomo Kenyatta ilianzisha sera ya kuwapa waafrika nafasi zilizoachwa na wazungu katika serikali. Amutabi (2009) na Odhiambo-Mbai (2003) wanasema kwamba Rais Kenyatta alirithi mfumo wa serikali jinsi ulivyokuwa chini ya wakoloni ambapo ulitumiwa kuchunga maslahi ya wakoloni walio wachache. Tunaona kuwa lililobadilika ni watu tu waliochukua nafasi hizo kwani waliendelea kutumia mamlaka ya kiserikali kuchunga maslahi ya wachache waliokuwa uongozini. Kwa kuwa hawakujali maslahi ya wananchi walio wengi, walishiriki ufisadi na uporaji wa mali ya umma ili kujitajirisha

pasi na kujali hali ya wananchi. Kutokana na haya, tatizo la kitabaka katika jamii likaendelea kuongezeka ambapo walio na mali waliendelea kutajirika huku maskini wakizidi kuwa maskini.

Mwelekeo huu kama ule wa hapo awali wa kuangazia ukoloni uliendelea kuchukua mtazamo wa nje ndani. Hii ni kwa sababu vidole vya lawama vilinyoshewa viongozi walio mamlakani na ukoloni mamboleo. Lakini licha ya haya matatizo yalioangaziwa tangu ukoloni bado yanaendelea kukithiri na hivyo basi waandishi wa kipindi hiki wamechukua mwelekeo mpya wa ndani nje.

### 2.5 Mtazamo wa Ndani Nje

Khamis (2012) anautaja mtazamo wa ndani nje kuwa mwelekeo unaoyaona matatizo ya bara la Afrika kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Nje, kwa mujibu wa msomi huyu, inachukuliwa kuwa ni pembejeo tu la matatizo yote. Kulingana na mtazamo huu, matatizo ya uongozi, umaskini, ufisadi na mengineo bado yapo. Hata hivyo, miaka mingi baada ya kupata uhuru, ni wazo la waandishi kwamba hatuwezi kuendelea kusingizia ukoloni kwa matatizo yanayaoendelea kukumba bara hili. Pia ingawa viongozi bado wanaendelea kuwanyanyasa wanaotawaliwa, ni muhimu kuiangalia jamii kwa undani ili kuangalia mchango wa kila mmoja katika tatizo hili la uongozi.

Watalaam katika kipindi hiki cha kihistoria wanasema kwamba wakati umefika kwa Afrika kuanza kujitathmini yenyewe. Edi (2007) anasema kuwa ni lazima bara hili liweze kujihakiki na kuweka matatizo yake wazi. Hapa, mtalaam huyu anataja maovu kama vile ufisadi, usaliti, uharibifu wa mali ya umma miongoni mwa mengine. Mawazo yake yanaungwa mkono na Kakraba (2011) akisema kwamba riwaya huwapa watu, jamii na bara hili changamoto za kutambua kilicho kizuri katika urithi wao na kuwazuzua kutafuta suluhu kwa matatizo yao. Hapa tunaona kubadilika kwa mtazamo

ambapo waandishi wanaitaka jamii iweze kujisaka na kutafuta suluhu za matatizo yanayoendelea kuikumba.

Katika riwaya ya *Wimbo Mpya,* Mbatiah (2004) anairudisha hadhira yake wakati nchi ilipopata uhuru. Kulingana na riwaya hii, ni kana kwamba mwandishi anasema hapo ndipo watu wangeanza kuimba wimbo mpya, wimbo ambao wananchi wenyewe kwa kushirikiana na serikali wangeanzisha miradi ya maendeleo. Katika kazi hii, mwandishi anasema kuwa wale waliobahatika kupata elimu wanafaa kuwa mstari wa mbele kuwahamasisha wengine na hivyo basi kuwawezesha wananchi kuchukua hatma ya maisha na nchi mikononi mwao. Ndio maana tunamwona Mariamu ambaye ni mwalimu akirudi kijijini baada ya kupewa talaka na mumewe. Anafaulu kuwaleta wanakijiji pamoja katika kuchangia mradi wa shule. Katika riwaya hii, tunaona kila kikundi kikitekeleza wajibu wake na kwa pamoja nchi inashuhudia maendeleo. Haya yanawiana na mawazo ya Masango (2002) anaposema kwamba Waafrika walishirikiana, wakategemeana kuzingatia vipawa mbali mbali miongoni mwao na kwa pamoja wakaweza kutimiza matarajio yao.

Mbatia anaendeleza wazo hili katika riwaya yake nyingine *Msururu wa Usaliti* (2010). Katika riwaya hii, mwandishi anaonyesha jinsi wananchi wamekuwa wakisalitiwa na viongozi waliowachagua. Tunapata kisa cha mbunge Mbogo ambaye anatumia mali ya chama cha ushirika kujilimbikizia mali. Hatimaye, anatumia mali hiyo hiyo kupata kiti cha ubunge ingawa hana elimu yoyote. Na kwa hivyo mwandishi anawataka walio na elimu kama vile wahusika Kage na Mutua kuendeleza vita vya ukombozi katika nchi zao. Ingawa elimu inachangia pakubwa katika kutatua matatizo ya jamii, ni wazi kwamba hivi sasa mataifa mengi barani Afrika, Kenya ikiwa miongoni mwao, yana viongozi ambao wana elimu; wengi wao wakiwa ni wanataaluma katika nyanja mbali

mbali. Lakini tunaona uongozi ukiendelea kudhoofika huku wakiendelea kupora mali ya nchi.

Kipindi cha miaka ya 1990 kilishuhudia mabadiliko makubwa barani Afrika kutokana na kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya kisiasa. Hili lilitokana na uongozi duni uliokuwa unaendelea kushuhudiwa katika nchi nyingi. Hata hivyo, Olali (2008) anasema kuwa licha ya kuwepo kwa vyama vingi hali ya maisha imebaki kuwa ile ile. Mataifa ya Kiafrika bado yanaendelea kushuhudia ufisadi, umaskini na uporaji wa mali na walio mamlakani. Olali anatuambia kwamba kubadilisha mifumo ya uongozi au hata viongozi wenyewe hakutoshi. Na kwa hivyo waandishi wanapendekeza kuwepo kwa mabadiliko ya kimsingi ili kushuhudia mabadiliko ya kudumu. Huu ni mtazamo wa ndani nje ambapo waandishi wanaitaka jamii iweze kujitathmini kwani suluhu haitatoka kwa viongozi peke yao lakini kutokana na jamii.

Kazi hizi zinaonyesha mtazamo mpya unaochukuliwa na waandishi wa kisasa kwamba suluhu la matatizo barani limo miongoni mwa wenyeji na wala sio nje. Kwa kuzingatia msimamo huu wa ndani nje, waandishi katika kipindi hiki wanaangazia asasi nyingine za jamii. Kati ya asasi hizo ni ile ya dini ambayo ina wajibu mkubwa katika kurekebisha jamii. Hii ni asasi ambayo inafaa kudumisha maadili ambayo yameadimika katika jamii. Masango (2002) anasema kabla ya kuja kwa dini ya kikristo, sherehe za kidini katika jamii ziliongozwa na viongozi waliokuwa na mamlaka makuu. Uongozi wao ulikuwa wa kufaa na ulioponya roho za watu. Hekima yao katika uongozi na kuwasaidia wanavijiji ilianzisha mahusiano mapya kati ya viongozi na wanaoongozwa. Anaendelea kusema kuwa viongozi hawa ndio walioweka urithi wa kidini katika jamii.

Ni wazi kwamba asasi ya dini ilipewa hadhi kuu katika jamii kutokana na majukumu iliyopewa na jamii. Hii ni kando na ilivyo sasa ambapo uozo umejaa katika asasi hii hivi

kwamba inaendelea kupoteza heshima yake katika jamii. Viongozi wa dini kama tunavyoambiwa na waandishi hawana tofauti na wale wa kisiasa kwani ufisadi, ubinafsi, tamaa ya pesa, na utengano unashuhudiwa makanisani. Na kwa hivyo ni wazo la waandishi kwamba asasi hii inafaa kujirekebisha ili iwe baadhi ya asasi zitakazoleta maadili na uwiano unaohitajika katika jamii.

Akinukuliwa na Masango, Mbiti (1977) anasema kuwa viongozi wa dini waliunda imani za kidini, walisherehekea sherehe za kidini, matambiko, walikariri methali na visaasili ambavyo vilikuwa na maana ya kidini. Pia waliunda sheria na tamaduni ambazo zililinda maisha na mtu binafsi na yale ya jamii au wanakijiji. Yaani walielekeza maisha na utoaji wa huduma kwa wanakijiji. Pia waliwajibikia kijiji/ jamii yote. Ikiwa kiongozi alikosa mwelekeo au kuwa na utovu wa nidhamu, wanakijiji hawakumshughulikia. Huu ndio baadhi ya urithi ambao watalaam wanazungumzia wanapowataka waafrika kuangalia chochote kizuri au cha manufaa katika urithi wao kama njia ya kukabiliana na changamoto katika jamii. Tunaona kwamba wanakijiji wenyewe kutokana na uelekezi waliopata kutoka kwa viongozi wao wa kidini walikashifu viongozi wabaya. Hili linakinzana na yanayoendelea hivi sasa ambapo viongozi wanaotenda kinyume cha maadili ndio wanaopata umaarufu katika jamii.

Mtazamo huu wa ndani nje una umuhimu mkubwa katika kazi hii, ni kiini hasa cha utafiti huu unaoangalia mwelekeo mpya uliochukuliwa na waandishi katika kipindi hiki cha kihistoria. Waandishi, kama Mulokozi (2012) anavyotuambia, wanaonyesha hasira yao kwa yale yanayoendelea kutendeka ambapo licha ya kuwa na uhuru kwa miongo kadhaa, hali ya wananchi kiuchumi na kijamii inaendelea kuzorota. Ni wazo la waandishi kwamba mataifa barani yana kila kinachohitajika kuwa sawa na mataifa mengine nje ya bara hili. Na kwa hivyo wanaitaka jamii iweze kujisaka na kuangalia kilicho kizuri katika urithi wao ili iweze kutoa suluhu kwa matatizo yake.

**2.6 Dhana ya Uongozi**

Uongozi ni dhana ngumu na ambayo ina maana kadhaa kadiri inavyoeleweka na kufafanuliwa na watalaam tofauti tofauti. Masango (2002) anasema kiongozi ni mtu anayewaathiri watu binafsi au vikundi miongoni mwa jamii au kijiji. Kiongozi huwasaidia anaowaongoza kuwa na lengo, halafu anawaelekeza kupitia kwa mfanyiko mzima wa uongozi, huku akiipa jamii nafasi yake katika mfanyiko huo. Kwa mujibu wa haya, anayeongoza na anayeongozwa kila mmoja ana nafasi yake katika mfanyiko huu wa uongozi. Ni wazi kwamba kiongozi ana jukumu kubwa la kuipa jamii anayoiongoza lengo na mwelekeo lakini pia ni lazima aihusishe jamii hiyo katika kutimiza lengo hilo. Anaendelea kusema kuwa tunahitaji viongozi watakaosaidia bara la Afrika kuwa na uvumbuzi. Njia ya pekee inayowezesha viongozi wa Afrika kuwajibika ni kuangazia matatizo yanayowaathiri wafuasi wao. Kiongozi anawajibika wakati anaangazia mahitaji na masuala ya wale anatamani kuwaongoza.

Akizungumzia dhana ya mamlaka na ambayo inahusiana kwa karibu na uongozi, Focault (1982) anasema kuwa kumekuwa na mivutano ya kijamii aina tatu katika vipindi tofauti vya kihistoria; mivutano dhidi ya utawala, dhuluma inayowatenga watu kutoka kwa wanachozalisha na dhidi ya mtu binafsi na wenzake. Hata hivyo kufikia karne ya 16, kumekuwa na mfumo mpya wa mamlaka ya kisiasa unaowakilishwa na serikali. Mamlaka hii ya serikali inaonekana kuwa haijali watu binafsi bali huangazia maslahi ya wachache. Hili ndilo tatizo la uongozi linaloshughulikiwa katika kazi hii ambapo waliopewa nyadhfa katika taasisi mbali mbali wanatumia mamlaka waliyonayo kuwagandamiza wengine.

Katika muktadha wa kiafrika, ilikuwa ni kawaida kwamba uongozi wa kitaifa barani katika kipindi cha baada ya uhuru ulikuwa wa “Mtu Mkubwa”. Katika aina hii ya uongozi, uamuzi wa ugawaji wa rasilmali, uwezo na mamlaka ulikuwa (na bado kwa

kiasi kidogo) unamilikiwa na rais. Pale ambapo malengo yalishirikisha wengine, viongozi wa serikali kwa kiwango kikubwa walihusisha kikundi kilichodhibitiwa na wakuu wa kisiasa (Gardner, 1990).

Hali hii ndio imeendelea katika bara hili ambapo wananchi hawahusishwi vilivyo katika maendeleo huku viongozi wakiendelea kuamua ni vipi rasilmali za umma zitatumika na hata miradi ya maendeleo itakayotolewa kwa wananchi. Tunaona hali ambapo mwananchi anayetozwa ushuru kufadhili miradi ya umma hana mchango wowote kuhusu jinsi ushuru huo unavyotumiwa.

Hili linathibitishwa na Kwaka (2011, uk 236) akisema kwamba tangu uhuru, utawala na usimamizi wa masuala ya umma ulipotoka hivi kwamba viongozi katika kila ngazi nchini waliwajibika tu kwao wenyewe au kwa vyama vyao vya kisiasa. Wananchi walitengwa na hawakuhusishwa kamwe katika maamuzi kwa mambo yaliyowahusu. Tunaambiwa kwamba la kushangaza, katika mataifa ya Afrika, siasa huwa ndio kitovu cha mamlaka na kwamba huwa inachukua kiasi kikubwa cha rasilmali kutoka kwa jamii. Kwa mujibu wa Afegbua na Adejuwon (2012), kitengo hiki cha siasa hutumia rasilmali hizo kujifaidi huku wanasiasa wakiwa hawana ari ya kuinua maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Mawazo ya Lumumba (2011, uk 38) kuhusu uongozi yanatupa hali ya kuhuzunisha kuhusu uongozi nchini Kenya. Anasema kuwa hapa nchini, kiongozi huchukuliwa kuwa yeyote aliye mamlakani bila kujali jinsi anavyotumia mamlaka hayo. Anaendelea kusema kule tu kuwa na nafasi inayoashiria uongozi huchukuliwa kuwa ni uongozi. Hili linaashiria kwamba wananchi hawajali sifa za anayechukua mamlaka. Pia kiongozi huyo yuko huru kutumia mamlaka yale kwa njia yoyote atakayo huku wananchi

wakiangalia tu. Hili linaeleza ni kwa nini tunapata viongozi wanaoshiriki ufisadi, wanaeneza siasa za chuki na maovu mengine wakiendelea kuchaguliwa.

Uongozi bora ni ule unaoonyesha usimamizi bora wa rasilmali za umma na hata za kibinafsi kwa manufaa ya wote. Lakini kwa mujibu wa kazi zilizoteuliwa tunaona viongozi wakifanya kinyume na haya kwani kando na kutokuwa na lengo lolote, wanaitumia jamii kwa maslahi yao ya kibinafsi.

Kwa hivyo uongozi unaathiri, una lengo, unawajibika na kuwashirikisha watawala na watawaliwa katika kila hatua. Kwamba hata baada ya uchaguzi, ni muhimu viongozi kuwashauri wananchi kuhusu matatizo yanayowakumba na jinsi wanavyoweza kuyatatua kwa pamoja. Vile vile wananchi wana jukumu kubwa katika uongozi. Lazima wajishughulishe na yanayoendelea katika uongozi kwa mfano, wajue fedha zilizotengewa miradi mbali mbali, kama miradi hiyo ilitekelezwa na pia kuhoji walio mamlakani. Katiba ya nchi ibara ya 118 (b) inasisitiza kushirikishwa kwa umma, ni muhimu wananchi watilie hili maanani.

## 2.7 Dhana ya Riwaya Mpya

Akizungumzia riwaya mpya, Wamitila (2003, uk. 185) anaeleza kuwa "dhana hii hutumiwa kuirejelea riwaya iliyozuka Ufaransa katika miaka ya 1950 na huakisi matumizi ya mbinu za kiubunifu za uandishi wa riwaya. Waandishi wa mkondo huu huwa na nia ya kuziasi kaida za kijadi za uandishi wa riwaya pamoja na kuyapinga baadhi ya mawazo waliyo nayo wasomaji kuhusu fasili hasa ya neno riwaya. Kazi hii ilichukua maelezo ya Matz (2004) kuhusu riwaya ya kisasa. Kwa mujibu wa mtaalam huyu, "riwaya huwa ya kisasa kila wakati kwa vile inaangazia maisha ya kisasa na, kama neno 'kisasa' linavyoashiria, huwa kila wakati inaangazia kitu kipya" (Matz, 2004, uk.1). Katika riwaya ya kisasa, mwandishi hutumia uhalisia kama jukwaa ambapo

yeye hutoa maoni ya kijamii na kisiasa. Mwandishi hutumia masuala ya kisasa yanayoathiri jamii lakini, badala ya kuwauliza watafute suluhisho za nje, hutumia bunilizi kwa kuirai jamii ijichunguze kama njia ya kushughulikia changamoto za kisasa (Hooti na Omrani, 2011).

Matz (2004, uk.7) anaendelea kusema kwamba, “riwaya ya kisasa inamaanisha bunilizi inayojaribu kitu kipya, katika kipindi hiki cha usasa, kutafakari, kufahamu, au hata kukomboa maisha ya kisasa. Katika kazi hii, tunapozungumza kuhusu riwaya mpya, tunarejelea riwaya ambazo zimeandikwa katika kipindi hiki cha kihistoria yaani miaka ya 2000 kwa vile zinaandika kuhusu changamoto zinazoikabili jamii na vile vile kutoa suluhu. Kwa hivyo, riwaya mbili zilizoshughulikiwa - *Paradiso* na *Msimu wa Vipepeo* - ni riwaya mpya kwani zinayaangazia matatizo ya kipindi hiki cha kihistoria na kutoa suluhu ambazo zitasaidia kukabiliana na changamoto za uongozi.

Riwaya mpya pia inaakisi mazingira yake. Katika juhudi za kukabiliana na masuala ya kisasa yanayoathiri watu binafsi, na kufanya hivyo kutoka pembezoni, riwaya mpya inakuwa zao la na pia huzalisha mazingira yake. Uandishi wa aina hii, ingawa ulitokana na hali za ukoloni na baada ya ukoloni, unaibuka kama wito wa kujitambua na unakiuka kanuni za awali za uandishi. Riwaya mpya hutambua na kupendekeza suluhisho za changamoto za 'kisasa'.

### 2.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumeelezea kuwa Habwe na Wamitila ni wanajamii na kwa hivyo kama wanajamii wengine wanaathiriwa na yanayoendelea katika jamii. Haya ni mambo kama ufisadi, ubadhirifu wa viongozi ambao umewaacha wananchi wengi wakiwa maskini na pia kutoajibika kwa viongozi na wananchi katika uongozi. Vile vile suala lingine ambalo limeiathiri jamii na ambalo limeangaziwa na waandishi ni unafiki katika dini

ambapo asasi hii imegeuzwa na kuwa asasi ya kibiashara na wakuu wa dini badala ya kukoleza imani na maadili. Hili limefanya asasi hii kukosa heshima na hadhi yake katika jamii. Pia mtazamo wa nje ndani umeangazia na kulinganishwa na ule wa ndani nje ambao ndio kiini cha utafiti huu. Hatimaye, tumeangalia fasili ya uongozi

# SURA YA TATU

# SUALA LA UONGOZI KATIKA RIWAYA YA *MSIMU WA VIPEPEO*

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaangazia suala la uongozi kama linavyojitokeza katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*. Inazamia masuala muhimu yanayoathiri uongozi nchini kama vile ufisadi, ukosefu wa huduma za kijamii, maonevu, umaskini, kutegemea misaada na ukiukaji wa sheria. Kwa kuongozwa na mtazamo wa ndani nje, sura hii pia inachanganua namna wananchi wanavyoshiriki mchakato wa uongozi. Vile vile sura hii inaangazia suluhu inayotolewa na mwandishi kukabiliana na tatizo hili la uongozi.

Changamoto maalum zinazozungumziwa na riwaya hii ya *Msimu wa Vipepeo* zikiwemo ufisadi, umaskini, maonevu ya kijamii yanayoathiri jamii au eneo fulani, ukosefu wa umoja wa kitaifa na utangamano, ukiukaji wa sheria na ukosefu wa utoaji wa huduma za kijamii zimeangaziwa. Aidha nchi inayorejelewa riwayani imetumiwa kuwakilisha nchi mbali mbali barani Afrika.

Kwa kuongozwa na fikra ya nadharia ya Uhistoria Mpya, sura hii pia inaangazia matini changizi zisizokuwa za kifasihi ili kuelewa muktadha wa riwaya ya *Msimu wa Vipepeo,* hususan namna riwaya hii inavyojengwa kiamudhui na matini hizo. Yerli (2017) anasema kuwa Uhistoria Mpya ni usomaji wa makini wa matini zisizo za kifasihi za kipindi maalum ili kuelewa kazi za kifasihi. Anaendelea kusema kuwa wananadharia ya Uhistoria Mpya hutumia makala yasiyo ya kifasihi kama vile makala ya kisheria, bunge, ya kidini na hata magazeti miongoni mwa mengine katika kuhakiki kazi za kifasihi. Sura hii inabainisha kuwa kazi ya kifasihi huathiriwa na muktadha wa kisiasa, kitamaduni, kidini na hata kijamii. Kwa kuzingatia nadharia hii na yale yaliyomo katika riwaya tunaona, kwa mfano, kuwa hali ya ubadhirifu serikalini inayozungumziwa na mwandishi ni hali halisi.

### 3.2 Uongozi katika Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*

#### 3.2.1 Ufisadi katika Uongozi

Kwa mujibu wa Mojdegani (2016), mhistoria Mpya hulenga kuitafsili kazi ya kifasihi kwa kueleza miundo ya mamlaka ya kijamii na jinsi mamlaka yalivyodhihirishwa katika matini. Anaendelea kusema kwamba nadharia hii huangalia "migogoro" ili kutambua ni kikundi kipi ambacho kina mamlaka katika jamii. Kwa hivyo, kwa kuzingatia haya tunaangalia ni kikundi kipi kilichopewa mamlaka katika riwaya hii na jinsi kinavyoyatumia mamlaka hayo "miaka isiyopungua thelathini na tisa tangu uhuru" (uk. 246).

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mwandishi amewapa viongozi wakuu wa kisiasa na serikali mamlaka. Hata hivyo anatupatia taswira ya viongozi ambao hawatumii mamlaka hayo kuwahudumia wananchi bali wanayatumia kujifaidi kupitia njia za ufisadi. Lumumba (2011) na Treisman (2000) wanakubaliana kwamba ufisadi ni matumizi ya afisi ya umma kwa lengo la kujinufaisha kibinafsi. Haya ndio mambo yanayotendeka uongozini kama Afegbua na Adejuwon (2012) wanavyotueleza, hapa barani Afrika ambapo mali yaliyomo hutawaliwa na wanasiasa wachache walio mamlakani. Waziri Mkurutu, katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, anawakilisha kikundi cha viongozi wenye mamlaka katika jamii. Kutokana na mamlaka hayo, wananchi wanawategemea ili kusuluhuhisha baadhi ya matatizo yanayowakumba. Hata hivyo, tunaona kuwa kikundi hiki cha viongozi kina matarajio mengine ambayo yanakinzana na yale ya wanaotawaliwa. Wamitila anasema kuwa baada ya kutangazwa kwa baraza la mawaziri, wananchi wana matumaini makubwa kuwa matatizo yao ambayo yamewasonga kwa muda yatapewa kipao mbele na viongozi wao wapya.

> Kiongozi wa nchi alikuwa ameteua baraza lake la mawaziri ambalo lazima lilipaswa kuhakikisha matatizo mengi, likiwepo hili la maji, yamesuluhishwa. "Oyee!" watu wachache waliokuwa pale

> walishangilia walipotambua kuwa shida yao imefikia ukingoni (uk. 13).

Hata hivyo, riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inatuambia kuwa viongozi wana matarajio mengine bali sio kuyatatua masuala ya wananchi. Pindi tu Mkurutu anapopata wadhfa huo anaingilia suala la ufisadi. Ni kiongozi ambaye hana subira ya kutumia mshahara anaopata kujijenga na badala yake anatumia njia za mkato na hila. Kwake yeye uongozi unampa nafasi ya kutumia mamlaka yanayotokana na afisi ile ili kujifaidi. Nyumba aliyonunua waziri huyo ilitokana na:

> … kuwepo kwake pale kulitegemea mwanasiasa mmoja ambaye alibamizwa kwenye kingo za mto wa uhalisi na mawimbi ya uchaguzi huo. Ninachotaka tu ni kupata hela ya kulipia huo mkopo kisha niende zangu mashambani! Hii Kitambaasie inione kisogo; naenda kula managu na terere, spaghetti na divai nakuachieni nyie! alisema mkurugenzi huyo. Mkurutu, akivuta tabasamu, moyo unampapa, akampa milioni kumi na moja aliyohitaji, pesa alizozipata baada ya kumsaidia mfanyibiashara mmoja kupata zabuni wizarani (uk. 20).

Wakati rais Kamaliza Rungu-rungu-ya-Kioga anapofanya mabadiliko katika serikali yake, Waziri Mkurutu anahamishwa kutoka Wizara ya Utalii hadi ile ya afya. Hii ni wizara ambayo ina umuhimu mkubwa kwa nchi kutokana na huduma muhimu inayotoa na kwa hivyo anayeisimamia ana jukumu kubwa kuona kuwa hali katika sekta ya afya inaimarika. Hata hivyo, Mkurutu hakuifurahia nyadhfa hii mpya kwa kuwa:

> Nafasi hii mpya ilimnyima Waziri Mkurutu fursa muhimu ya kusafiri nje, kwa kisingizio cha majukumu ya wizara yake. Alihisi kuwa kashushwa hadhi ingawa kahamishiwa wizara muhimu sana katika nchi yake inayougua kila aina ya maradhi (uk. 153).

Hali hii ni sawa na ile Kiai, akinukuliwa na Mutula, Muna na Koma (2013), anarejelea anaposema kwamba ufisadi ulikuwa jambo la kawaida kwa wanasiasa na wakuu serikalini. Hili linaeleza ni kwa nini walikuwa wanang’ang’ania nafasi za uwaziri ambazo walitumia kujipatia mamlaka. Na kwa hivyo waliokuwa katika mamlaka walichangia pakubwa katika wizi wa mali ya umma ili kuendeleza maslahi yao ya kisiasa. Walitumia afisi zao kuiba mali ya umma bila uwazi wowote. Anaendelea

kusema kuwa mamlaka makubwa yaliyopewa afisi ya rais katika katiba ya zamani yalifanya afisi hiyo kuwa kitovu cha ufisadi. Asasi zilizoundwa kuangalia matumizi mabaya ya mamlaka hazikuwa na mamlaka yoyote. Asasi kama vile idara ya mahakama na bunge zilibaki tu kupitisha matakwa ya rais hata yale yaliyokuwa na athari hasi kwa nchi. Naye Hope (2014) anasema hali ya ufisadi nchini ilifikia wakati ambapo hakukuwa na tofauti kati ya maslahi ya umma na yale ya kibinafsi huku maafisa wa serikali wakiendelea kuiba kutoka kwa hazina kuu ya serikali na asasi zingine za serikali.

Hali hii inawiana na yanayosimuliwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambapo Waziri Mkurutu anatumia nafasi ya uwaziri kuiba fedha zilizotengewa Wizara ya Afya ili kujitajirisha. Mwandishi anatupa taswira ya kuhuzunisha katika hospitali za umma ambapo wengi wa wananchi wanatafuta matibabu jambo ambalo lingemfanya Waziri Mkurutu kutia juhudi kuona kwamba hali hiyo inaimarishwa. Lakini kwa Waziri Mkurutu, hili ni jambo linalomchukiza na kwa hivyo hana nia ya kuibadilisha hali hii. Kwake yeye, haya ni majukumu tu anayoyatekeleza kwa vile hawezi kuyakwepa. Mwandishi ansema:

> Waziri Mkurutu hakupenda kazi ya kuandamana na wageni kwenye hospitali za kitaifa na kuwaonyesha shughuli za huko. Harufu ya dawa za hospitalini ilimtia kipalizi puani; sura ya magwanda ya wagonjwa ilimsinya na sura za wagonjwa wenyewe kumletea hisia za mtu anayekimbizwa na jinamizi. Alikerwa na miguno yao vitandani pamoja na vilio vya kuyalilia maisha. Waziri alichukizwa hata na mandhari zenyewe hospitalini. Lakini hakuweza kuyakwepa majukumu yake ya kiwaziri (uk. 172).

Licha ya kuwa waziri alisinywa na hayo yote, alifurahia kutumia rasilmali ambazo zingeweza kuibadilisha hali hii. Katika riwaya hii, Wamitila anaonyesha kuwa kuna rasilmali ambazo kama zingetumiwa kwa njia inayofaa, zinaweza kubadilisha hali ya nchi. Mwandishi anatuambia kwamba serikali inanunua dawa ambazo zinafaa kupewa wagonjwa hospitalini. Hata hivyo, badala ya dawa zile kuwafikia wagonjwa, waziri

anatumia mamlaka yake kuanzisha biashara ya kuziuza huku akihakikisha kuwa madaktari wanawaelekeza wagonjwa wao wanunue dawa kwa duka la waziri. Kwa hivyo tunaona hali ambapo fedha ambazo zingeimarisha hali ya nchi zinabaki kwa wachache walio katika mamlaka na ambao wanazitumia jinsi watakavyo.

> Alishaanza biashara ya uuzaji wa madawa, na kwa kufuata ushauri wa Fabio, akalitumia jina la ndugu aliyekuwa mfanyikazi katika kiwanda kimoja cha sukari nchini. Walishawasiliana na madaktari wengi jijini kuhakikisha kuwa watu walipendekezwa wakanunue dawa pale (uk. 161).

Pia katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo,* Waziri Fumo anashinda zabuni ya kutoa tarakilishi kwa serikali licha ya kuwa hakutuma ombi wakati kampuni zingine zilikuwa zinatuma maombi (uk. 110). Jambo linaloudhi ni kwamba licha ya kupewa hiyo zabuni kinyume cha sheria, anatoa tu tarakilishi tatu ilhali fedha zimelipwa. Pia kwa kuwa anajua anachokifanya, anamwamuru meneja kutia sahihi na hivyo basi kujiondoa lawamani. Tunampata waziri huyu akiwanyanyasa wanaofanya kazi chini yake kwa kuwatumia kulipia makosa yake. Ni wazi kwamba meneja hangekataa agizo la waziri na hata anashindwa jinsi atajitetea kwa makosa ambayo yeye hakuyafanya. Meneja huyo anaishia kufutwa kazi kwa makosa ya waziri.

Mwandishi anatuambia kuwa wakurugenzi ambao wanateuliwa na mawaziri kusimamia mashirika mbali mbali wanachukua nafasi hizo sio kwa azma ya kutoa huduma bali kwa kutaka kuchunga maslahi ya mawaziri waliowateua na hasa kuwaficha wanapotekeleza uovu. Vile vile wanawanyanyasa wadogo wao ambapo wanatekeleza ufisadi lakini wadogo ndio wanaoulipia kwani pesa zao zinatwaliwa kulipia uovu uliotendwa na waziri na hata kufutwa kazi.

> Mkurugenzi wa shirika (ambaye kwa kawaida aliteuliwa na waziri-baada ya mahojiano) aliwaita mameneja wote. Bwana Chacha hatuwezi kumlaumu waziri kwa kukosekana kwa tarakilishi za shirika. Waziri sio meneja wa shirika! Hivi tumpigie simu na kumwambia kuwa hakuyakagua makatoni ya tarakilishi? Huo sio

> uwajibikaji kabisa!" Meneja akajaribu kujitetea; hata waliomfahamu kwa karibu sana kama Kanda walimtetea. Lakini haikusaidia kitu. Huo ndio uliokuwa mwisho wake; akafutwa na robo tatu ya marupurupu yake kutwaliwa na shirika kufidia gharama za tarakilishi hizo (uk. 111).

Haya yanawiana na anayosema Akech (2011), kwamba rais, mawaziri wa serikali na wafanyi kazi wakuu serikalini huwa wanatumia sheria kuwatisha wadogo wao kutekeleza amri kinyume cha sheria kwa sababu ya ukosefu wa taratibu za uwajibikaji. Anasema kuwa wafanyi kazi wa chini hujipata wakishiriki ufisadi kinyume na mapenzi yao. Mwandishi wa riwaya hii anaendelea kusema kwamba ufisadi haumo tu kwa mawaziri bali unaanzia kwa kiongozi wa nchi mwenyewe. Hili linaonyesha jinsi ilivyo vigumu kupigana nao kwa sababu ikiwa rais mwenyewe anaendeleza ufisadi, basi inakuwa rahisi kwa walio chini yake kutenda vivyo hivyo licha ya pingamizi kutoka kwa wachache.

> Alikumbuka jinsi walivyomsaidia jamaa yake rais ambaye alikuwa na zabuni ya kuuza tarakilishi kwenye wizara ya serikali; zabuni ambayo katika kikao cha baraza la mawaziri ilipingwa sana na mawaziri kadha wakiongozwa na Waziri wa Elimu na Taaluma (uk. 268).

Mwandishi anatupatia taswira ya viongozi ambao wanafurahia mamlaka wanayopewa si kwa sababu wanayajali maslahi ya umma lakini kwa sababu zao wenyewe. Kutokana na haya, hawana roho ya utu ya kujaribu kusuluhisha matatizo ya umma lakini wanataka tu kujifaidi. Hii ni sifa moja ya uongozi mbaya ambapo viongozi wanaangazia maslahi yao wenyewe badala ya wale wanaowaongoza.

Shirika la *Transparency International* linasema kuna aina mbili za ufisadi, ufisadi wa kisiasa na ule wa kirasimu. Kwa mujibu wa shirika hilo, ufisadi wa kisiasa hutekelezwa katika viwango vya juu vya mamlaka. Ufisadi huu huhusisha wanasiasa, mawaziri wa serikali, wafanyi kazi wakuu serikalini na wakuu wengine ambao wameteuliwa, kuchaguliwa au kupewa nyadhfa za umma. Ufisadi huu unahusisha matumizi mabaya

ya afisi na wale wanaotunga sheria na ugawaji wa rasilmali katika jamii. Unaweza kuhusisha kuunda sheria kwa manufaa ya mawakala wa sekta ya kibinafsi ili wapate hongo, kutoa zabuni za umma kwa makampuni maalum au ufujaji wa pesa kutoka hazina kuu ya serikali.

Ufisadi wa kirasimu hutokea wakati wa kutekeleza sera za umma na huhusisha wafanyi kazi, warasimu na maafisa wa utawala. Ufisadi huu huwa ni kati ya warasimu na mawakala wa kibinafsi. Mawakala kama hao huenda wakaitisha malipo ya ziada ili kutoa huduma za serikali; au kulipia hongo ili kuruhusu vitendo vinavyokiuka sheria na taratibu. Aina zote mbili za ufisadi zimejitokeza katika riwaya hii kama ambavyo tumeona hapo awali. Haya yanadhihirisha yanayoshikiliwa na nadharia wa uhistoria mpya kwamba itikadi zinazobaini fasihi lazima zitafitiwe na kuhakikiwa kwa njia za kijamii, kisiasa na kiuchumi za kipindi kinachozungumziwa (Balkaya, 2014).

Ufisadi wa urasimu unajitokeza katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambapo Waziri Mkurutu na mwanasheria Fabio Mkalla wanashirikiana na Gertuso Berlusconi (GB) kuwanyang’anya wakazi wa Kisiwandeo rasilmali yao. Mkalla anatumia mamlaka yake kama mkuu wa sheria na tajriba yake kuvunja sheria za nchi. Tunaona kuwa badala ya kutetea umma, viongozi hawa wanashughulikia maslahi yao kwa kukiuka sheria na taratibu zilizowekwa. Hii ni rasilmali ambayo wakazi wangetumia kujiimarisha kiuchumi lakini badala yake viongozi hao wanachangia kuwanyanyasa kiuchumi. Kupitia ushirikiano wake na viongozi hao, GB anawakataza wananchi kuvua samaki kwa kuwa ile bahari ambayo ni mali ya umma imegeuka na kuwa rasilmali ya kibinafsi.

> Palikuwa na kigaro cha watu waliokuwa wakiongea kwa kuhamasika sana - wakifyoa; wakilaani na wakilalamika. Walikuwa wakaazi wa pale ambao walikuwa wanalalamikia kuwa GB alikuwa akiwanyima nafasi ya kuwavua samaki baharini kwa kudai kuwa ni sehemu ya ardhi yake. Kwamba sehemu ya bahari iliyokuwa mbele ya jumba lake ilikuwa mali yake; maji, samaki na viumbe vyote walioishi pale.

> Fabio na waziri walitazamana kabla ya kuchepuka na kuelekea hotelini (uk. 66).

Bhat (2014) anasema kuwa nia kuu ya nadharia ya uhistoria mpya ni kuangalia kazi ya kifasihi kwa kuzingatia usuli wake kihistoria na kuangazia hali ya kijamii na kiutamaduni. Wananadharia hii huchambua matini kwa kushirikisha katika tathmini matini za kifasihi na zisizo za kifasihi ambazo huenda zilimwathiri mwandishi wakati wa kuandika kazi yake. Na hivyo basi ni muhimu kufahamu uhusiano kati ya matini, hali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Anasema kuwa kila matini ni diskosi inayoashiria hali halisi.

Kwa kuzingatia haya, tunaangalia makala yake Khamis (2018) kuhusu kampuni moja ya kutoka nje inayoitwa Dominion ambayo ilipewa fursa ya kuwekeza katika kaunti ya Siaya. Kando na uvuvi, kampuni ya Dominion ilinuia kuwekeza katika ukulima wa pamba na mpunga na pia kujenga mitambo ya kusagia. Ili kufanya hivi, ilijenga bwawa ambalo wataalam wa mazingira walisema litasababisha mafuriko ambayo yangetatiza maisha ya wakazi. Kampuni hii ilibinafsisha ziwa, barabara, wakazi wakazuiwa kufika shuleni, sokoni na hata vituo vya afya na kufanya maisha ya wakazi kuwa magumu. Hapa tunaona viongozi ambao haja yao kuu ni kuwafurahisha wawekezaji na kuwasahau wananchi ambao kando na kuwapa mamlaka walio nayo kupitia kwa kura, wanajitajirisha kwa kodi wanazolipa.

Kwa kuzingatia haya tunachunguza utawala na dhuluma zinazotendewa wananchi katika kipindi hiki cha kihistora. Kwamba kuna viongozi ambao wamechaguliwa na wananchi ili waweze kutatua changamoto zinazowakabili. Wanalipwa kutokana na kodi inayotozwa wananchi lakini wanawadhulumu kwa kuwanyang’anya njia zao za kujipatia riziki. Wamitila anatoa picha ya viongozi ambao wanajali maslahi ya wageni zaidi huku wakiwapuuza wenyeji. Gertusso Berlisconi alikuwa anawanyanyasa wakazi

lakini habari hizo zinapowafikia wanahabari, waziri Mkurutu na mkuu wa sheria Fabio wanafanya kila njia kuhakikisha kwamba wanazima habari hizo:

> Ndio… wasiliana na hiyo Mamlaka ya Ushuru, alitua Waziri Mkurutu. Fabio Mkalla sasa aligeuzwa mwanafunzi; akaambiwa kuwa ni bora kusaka taarifa kutoka huko ili kuwalazimisha wakuu wa kampuni kuiachilia ile habari. Aliambiwa kuwa hata kama italazimu watazungumza na huyo mkurugenzi wa Mamlaka ya Ushuru na kumshawishi avighushi vyeti fulani ili kuwalazimu waliokifuatilia kisa cha GB wakome kufanya hivyo (uk. 120).

### 3.2.2 Ukosefu wa Huduma za Kijamii

Hali hii ya ufisadi wa hali ya juu miongoni mwa viongozi imesababisha kudorora kwa hali ya maisha ya wananchi. Wamitila, katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, anasema kwamba miaka mingi baada ya uhuru, utoaji wa huduma za kimsingi katika jamii umebakia kuwa changamoto kuu. Tunaambiwa kwamba wananchi hawawezi kupata huduma za afya kutokana na uhaba wa wahudumu na pia madawa katika zahanati za afya. Hili, kwa mujibu wa riwaya hii, sio kwa sababu hakuna dawa lakini dawa ambazo zinatolewa na serikali zinachukuliwa na viongozi na kuanzisha biashara. Katika riwaya hii ya *Msimu wa Vipepeo*, tunaona tashtiti kuhusu ubadhirifu wa viongozi ambapo wanakunywa danga ya nchi huku wananchi wakiwachiwa makombo. Tashtiti hii kuhusu uongozi imeufumbata ujumbe katika riwaya hii ambapo viongozi wanaishi maisha ya raha mustarehe huku wananchi wakizidi kuzama katika umaskini. Katika tashtiti hii, danga inawakilisha chochote kizuri nchini ikiwemo, magari, majumba ya kifahari, huduma za kimataifa za afya na hata ziara za kujivinjari katika mataifa ya nje kinachukuliwa na viongozi.

> "Ati nini" aliuliza Melissa bado akicheka.
>
> "Watoto wanaanza kupewa ziwa la mama wiki tatu baada ya kuzaliwa?"
>
> "Ehhh! Na kwa nini?"
>
> "Kwa sababu danga katika jamii hiyo sio ya watoto!"

> "Ni ya nani?"
>
> "Wanaume. Ndio wanaonyonya…Jamii inasema kuwa danga ni ya mwanamume si mtoto mchanga!" (uk. 192).

Katika tashtiti hii, tunaweza kutafsili mwanamume kuashiria viongozi kama ilivyo katika utamaduni wa jamii nyingi ambapo wanaume ndio hupewa nafasi ya kuwa viongozi. Mama naye ni nchi, maziwa ni rasilmali za nchi huku watoto wakichukua nafasi ya wananchi. Danga ni muhimu katika uhai wa kiumbe chochote kinachokua kwani inatoa kinga kutokana na magonjwa mbali mbali. Kwa hivyo, kama mwandishi anavyosema, mwanamume huyu ambaye ndiye kiongozi anachukua chochote kilicho kizuri katika nchi huku wananchi wakiwachwa bila kinga yoyote.

Katika jamii hii, viongozi wanapata matibabu ya hali ya juu, hao ndio wanaoamua miradi itakayotolewa na serikali, wanajipatia utajiri mkubwa kwa kutumia nafasi zao kujilimbikizia mali ya umma. Wananchi kwa upande wao, hawana chakula, huduma za hospitali ni duni, wananyang'anywa hata kile kidogo wanachoweza kutumia kuchuma riziki. Katika uk. 70, Waziri Mkurutu hakustuka alipoambiwa kuwa huenda gharama ya uchunguzi wa bibi yake Julia kutokana na shida ya kutopata mtoto kuwa ilikuwa juu. Hii ni kwa sababu kama waziri ana mshahara mzuri, alikuwa na bima nzuri ya kiafya ambayo iliwaruhusu mawaziri kufanyiwa matibabu popote pale ulimwenguni kwa gharama ya serikali na pia:

> … Palikuwa na kasma kubwa iliyotengewa wizara ambayo hali ikiwa mbaya anaweza kuimega kidogo. Yeye ni kiongozi anayelitumikia taifa lake. Kwa hivyo kujitolea (kama mkewe alivyoyakinisha) kwa hayo kutakuwa na tatizo gani kama serikali yake italazimika kuichukua sehemu ndogo ya kodi zake kuhakikisha kuwa amepata mtoto? Hilo ni suala kubwa na muhimu sana; suala la kitaifa hasa (uk. 70).

Huku yeye kama kiongozi akiwa anaweza kupata haya yote, wananchi hawana hata mahitaji ya kimsingi kama vile chakula. Wanaishia kupewa chakula cha mbwa ambacho hakifai kwa wanadamu na hata wanapougua, wengi wanaishia kufa kwa sababu hakuna

dawa na wahudumu wa kutosha. Mwandishi anazua suala la ukosefu wa huduma za kimsingi licha ya ubadhirifu mkubwa wa viongozi. Hata serikali yenyewe haiwezi kuwapa wananchi chakula na badala yake inategemea nchi za nje ambazo zinatoa chakula ambacho hakifai kwa wanadamu. Chakula hiki kinachotolewa kama msaada na serikali za nje kinaishia kuwadhuru kiafya. Wanapatwa na maafa ambapo waliumwa na tumbo na kuaga dunia:

> Baadaye alianza kutoa maelezo yake kwa utulivu mara hii. Kwamba watu walipewa chakula kilichotolewa na serikali majuzi tu. Waliokula walianza kulalamika maumivu ya tumbo; wengine macho yao yakabadilika na kuwa ya manjano; matumbo yakavimbiana na hatimaye, kama majani ya mitende, miti inayokua sehemu hiyo kwa wingi, wakaanza kupukutika mmoja baada ya mwingine; kwingine hata jamaa nzima zimefutwa na mahindi hayo. Vituo vya afya vilivyokuwa karibu havikuweza kuwasaidia kwa sababu ya ukosefu wa madawa na wahudumu wenyewe (uk. 245).

Katika riwaya hii tunapata picha ya nchi iliyogawanyika pande mbili. Kuna nchi ya viongozi na matajiri wanaoshirikiana na viongozi kufuja fedha za wananchi na ambayo ni nchi ambamo watu wanakula na kusaza. Kwa upande mwingine, kuna nchi ya watu wa kawaida ambao kama mwandishi anavyotuambia wanaendelea kuzama katika lindi la umaskini ambao umewala hivi kwamba wamebaki mizoga au kiwiliwili.

> Melissa aliwazia tatizo hilo la njaa. Nchi yake imekuwa huru kwa miaka isiyopungua thelathini na tisa lakini bado inashindwa kujilisha yenyewe. “Mama mbona tunashindwa kama nchi kuwa na mipango mizuri ya kupambana na njaa? Kila wakati tunategemea misaada, hata ya chakula! “Inasikitisha kwa kweli na tunaweza kuchimba chemchemi za maji kuwasaidia watu kwenye maeneo kaufu” Na utazame ubadhirifu wa serikali yenyewe; magari wanayoyaendesha viongozi wenyewe, jinsi wanavyotota kwenye maisha ya raha; gharama si gharama hizo!” (uk. 246).

Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inaangazia suala muhimu na ambalo limeendelea kuathiri mataifa yanayoendelea hasa barani Afrika, suala la ukosefu wa chakula. Hili ni suala la kimsingi na ambalo kila taifa huru linafaa kuwa linajitosheleza. Huku wananchi wakiendelea kufa kutokana na njaa na pia ukosefu wa huduma za afya, viongozi wanaishi maisha ya kifahari kwa kutumia fedha za wananchi, fedha ambazo

zingeanzisha miradi ambayo ingetoa suluhu kwa baadhi ya matatizo ambayo wananchi wanashuhudia. Haya yanahusiana kwa karibu na ripoti ya mashirika ya *Transparency International* na *Kenya National Commission on Human Rights* (KNCHR), ambalo ni la kiserikali ambayo kwa pamoja yalitoa ripoti mwezi wa Februari mwaka wa 2006.

Katika ripoti hii, iligunduliwa kwamba kati ya mwezi Januari 2003 na Septemba 2004, serikali ya National Rainbow Coalition ilitumia takriban dola milioni 12 kununua magari kwa matumizi ya kibinafsi ya maafisa wakuu serikalini. Magari hayo yalijumuisha magari 57 aina ya *Mercedes-Benz, Land Cruiser, Nissan Patrol* na mengineo. Fedha zilizotumika zilizidi zile ambazo serikali ilitumia mwaka wa kifedha wa 2003/04 kukabiliana na malaria – "ugonjwa ambao unasababisha vifo vingi nchini".

Kwaka na Mutunga (2011) wanakubaliana na haya wakisema kuwa takriban asilimia 80 ya wakenya hutegemea sekta ya kilimo. Hata hivyo kutokana na ongezeko la joto ulimwenguni na mabadiliko ya hali ya anga, imekuwa vigumu kutegemea misimu ya mvua kwa miongo kadhaa na hivyo basi inakuwa vigumu kutegemea kilimo. Janga hilo kwa miaka mitatu lilisababisha kupoteza kwa ajira na kusababisha kukosekana kwa chakula. Matokeo yakawa ni janga la njaa, utapia mlo na hata vifo. Hata hivyo wataalam hawa wanashangaa ni kwa nini nchi hii inaendelea kutegemea mvua kwa kilimo ilhali kuna mito mingi na maziwa nchini. Kwao, hili linaonyesha uongozi duni wakisema tangu uhuru, hakuna serikali ambayo imeupa ukulima wa unyunyizaji maji kipao mbele ili kuwezesha nchi hii kuweza kujitegemea kwa chakula.

Wataalam hawa wanaendelea kusema kwamba ufisadi huchukua mabilioni ya pesa za Wakenya na huenda ukawa chanzo kikuu cha umaskini uliokithiri nchini. Kwamba fedha zinazopotelea kwa ufisadi zingetumika kujenga mahospitali, viwanda, barabara, shule, kutoa maji safi, kufadhili unyunyizaji maji miongoni mwa mengine. Kwa

kufanya hivi, wakenya wanaoaga dunia kila mwezi wangepata matibabu kwa bei watakayomudu na pia hawangekufa njaa (Kwaka na Mutunga, 2011).

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, tunaona wananchi ambao wamepoteza matumaini na ambao hawaoni matunda ya uhuru kwani licha ya kuwa na viongozi wao katika mamlaka, bado wanaendelea kushuhudia unyanyasaji chini ya serikali yao. Katika riwaya hii, tunashuhudia masaibu ya wakulima wa eneo la Mwetare ambao wanafanya kazi ngumu shambani lakini hawafaidiki na jasho lao. Ingawa serikali inachukua mengi ya mazao yao, haijawapa huduma muhimu kama vile umeme, hospitali na hata shule nzuri. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba watoto wa wakulima ndio wanaohudhuria shule ambazo si nzuri huku watoto wa mawakala wa serikali wakipelekwa shule za kifahari. Tunaona serikali ambayo inaendeleza sera zilizoachwa na wakoloni za kuwanyanyasa waafrika.

> Mtu unavuna magunia arubaini ya mchele; mwenyewe unaruhusiwa kuuza magunia manne tu! Mengine mali ya serikali! Hamna anayejali kama una jamaa; unaumwa; una ardhi…una nini! Shauri yako na maisha yako! Sasa hiyo raha ya kuvuna iko wapi kama mavuno wanafaidi hao wanaoishi huko Kitambaasie; wamejitambaza tu kwenye penu za ofisi zao kubwa kama mijusi wasijue hata hiyo sura ya mpunga! Kanda alikaa tutwe. Yule mzee alieleza jinsi walivyotaabika; jinsi eneo zima la Mwetare lilivyokosa huduma muhimu kama umeme; hospitali na hata shule nzuri – ingawa watoto wa mawakala wao wenyewe wanasomea shule za Wazungu. Jinsi walivyomenyeka kwa kazi ngumu huku wanawafaidi wengine. Na walivyopuuzwa na serikali kuu katika maamuzi yake. Mwishowe akamuuliza, Nambie mwanangu, huo uhuru tuliopata unatanda nchini kwa hatua za kinyonga au kama maji unakauka kabla ya kutufikia sisi tunaoishi vijijini? (uk. 17).

Odhiambo-Mbai (2003) anasema kuwa serikali ya kwanza nchini ilirithi mfumo wa uchumi ulioachwa na wakoloni. Katika mfumo huu, bei ya bidhaa za viwanda na kilimo kwa upande mmoja na zile za matumizi kwa upande mwingine ziliongozwa na nguvu za soko. Lakini kama ilivyokuwa katika sekta ya umma, uchumi ulisimamiwa kwa kiwango kikubwa na wazungu. Wazungu hawa walidhibiti viwanda na mashirika ya

kifedha na pia walimiliki mashamba. Wengi wa waafrika walikuwa tu wanafanya kazi katika mashamba haya kwa malipo ya chini huku wengi wakiishi kama maskwota katika mashamba hayo.

Hii ndio hali ambayo inaendelea kuwakumba wakazi wa Mwetare ambao, miaka mingi baada ya kupata uhuru, bado serikali imeendelea kudumisha sera za wakoloni ambazo ziliwanyanyasa na kuwanyima nafasi ya kujiendeleza. Hili linaeleza ni kwa nini umaskini umeendelea kukithiri kwa vile viongozi hawana nia ya kubadilisha hali iliyoko kwani inawafaidi.

### 3.2.3 Upendeleo katika Miradi ya Maendeleo

Wakitafitia kuhusu ujenzi wa barabara nchini Kenya, Burgess, Remi, Edward, Ameet, na Gerard (2015) wanasema kuwa viongozi barani huhakikisha miradi hutekelezwa katika maeneo maalum. Wanaendelea kusema kuwa rais amekuwa akitumia mamlaka yake makubwa kuingilia mipango ya barabara na kuhakikisha kwamba zimejengwa katika wilaya ambako kuna kabila lake. Mawaziri wanaosimamia wizara ya barabara pia hao wanafanya vivyo hivyo na kupendelea eneo wanalotoka. Hali hii inatokana na ubinafsi wa wanasiasa ambapo wanatumia fedha za umma kujipigia debe wakati wa kura. Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, tunaona viongozi ambao kwa vile hawana maono wanatumia fedha za umma kulingana na matakwa ya mtu mmoja badala ya nchi. Katika riwaya hii, tunaona viongozi wakitumia mamlaka waliyonayo kubadilisha mradi wa kitaifa na kuanzisha mradi mwingine ambao hata haujajadiliwa ili kuona iwapo utakuwa na manufaa yoyote kwa taifa. Kwa kufanya hivi, viongozi wanatumia fedha za umma kujipigia debe kwa kupeleka miradi hii mahali wanakotoka. Hii ni licha ya kuwa maendeleo hayo yangeifaa nchi bila kujali yamo katika eneo lipi. Pia, fedha

zinazotumika kufanya maendeleo haya zinatoka katika kila pembe ya nchi na sio sehemu ambayo kiongozi fulani anatoka na kwa hivyo zinafaa kufaidi wote.

> Wanawarsha walijadili umuhimu wa kuanzishwa kwa chuo kinachoshughulikia sayansi ya baharini Gongwa. Kwa kweli chuo chenyewe kilishaidhinishwa miaka sita iliyopita lakini waziri aliyekuwako wakati huo akakipinga kwa kuwa hakuwa mwenyeji wa eneo hilo. Ilidaiwa kuwa alibadilisha hati fulani na kuhakikisha kuwa fedha iliyotengwa kwa ajili ya kuanzishwa kwa chuo hicho imehamishwa kwenye chuo kingine kilichoanzishwa kwenye eneo bunge lake (uk. 51).

Hii ni sifa moja ya uongozi mbaya kwani aina hii ya uongozi huhusisha kulazimisha malengo ya viongozi kwa wananchi kabla ya kuwashauri na kukubaliana nao. Pia hawazingatii umuhimu wa miradi hiyo kwa muda. Hawa ndio aina ya viongozi walioko kulingana na riwaya inayoshughulikiwa ambao hawana maono bali wanafanya mambo kulingana na matakwa yao. Riwaya hii inatoa picha ya viongozi ambao wana maono finyu ambapo hawaangalii maendeleo ya nchi kwa ujumla na badala yake wanafikiria tu kuhusu maeneo yao. Hili ni jambo ambalo linaathiri mataifa mengi katika bara la Afrika ambapo viongozi hawaangazii maendeleo ya sehemu mbali mbali za nchi. Badala yake tunaona fedha za umma zikitumiwa kwa maeneo fulani nchini huku maeneo mengine yakibaguliwa. Hili linasababisha maeneo mengine kubaki nyuma na pia kuleta mafarakano kwani maeneo hayo huhisi kubaguliwa na serikali.

Viongozi hutumia mali ya umma kuwekeza katika maeneo wanayotoka ili wapate kuchaguliwa tena (Burgess na wenzake, 2015). Haya yanawiana na yale riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inayoyasimulia inaposema ya kwamba linalowasumbua si jinsi watakavyowahudumia wananchi lakini njia watakayotumia ili wachaguliwe tena na kuendelea kuifyonza nchi. Wanajua kwamba hamna lolote ambalo wamewafanyia wananchi na kwa hivyo hawana ujasiri wa kuwarudia wananchi na kuwaomba kura. Ni kutokana na uoga huu ambapo viongozi wanajilimbikizia mali ili waweze “kuwanunua” wapiga kura wakati wa uchaguzi na kuendelea kuwanyanyasa.

> Waziri alitamani angepata jambo ambalo lingemfungamanisha na raia wa eneobunge zima; likawachanja damu, kama watu wa jamii yake walivyofanya zamani, kuudumisha udugu na urafiki wao, wasiachane naye asiwe na wasiwasi wa kuukosa ubunge wake ambao ulimpa fursa adimu ya kuufyonza uhondo wa damu kwenye mwili wa nchi yake (uk. 173).

Rose-Ackerman, akinukuliwa na Jain (2001), anaeleza kuhusu aina ya uongozi unaokisia kuwa wapiga kura hawajui lolote, na kwamba wabunge wanaweza kununua kura zao. Katika mazingara haya, nia ya wabunge ni kutafuta kuchaguliwa tena na kujinufaisha kibinafsi. Kwa hivyo, uwezo wao wa kudhibiti ufisadi unategemea vyama vya kisiasa vilivyoko, asasi za kisiasa na jinsi wanavyofadhili kampeni zao. Ufisadi kwa hivyo unanawiri pale viongozi wanapotoa miradi itakayowafaidi wenyewe na wala si wananchi. Huu ndio uongozi unaozungumziwa na kazi inayoshughulikiwa ambapo wanasiasa huja inapokaribia uchaguzi na kuwadanganya wananchi na miradi ya maendeleo ambayo haina manufaa kwa wapiga kura bali kwa wanasiasa kwani inawapa nafasi ya kuendelea kujinufaisha na mali ya umma.

### 3.2.4 Umaskini

Kaiser, Padilla na Hogan (2007) wanasema kuwa athari za uongozi mbaya hujitokeza katika maisha duni wanaoyoishi watawaliwa. Katika riwaya hii, hali hii inajitokeza katika hali ya uchumi ya wananchi ambayo inasababishwa na vitendo vya viongozi. Yerli (2017) anasema kuwa wanauhistoria mpya hulenga kuielewa kazi ya kifasihi katika muktadha wake wa kihistoria. Hivyo basi ni muhimu kuitalii kazi ya kifasihi na muktadha wake wa kihistoria ili kuilewa kazi ya kifashi. Tumeona jinsi mali iliyotengewa huduma za kijamii inavyoliwa na wachache kupitia kwa ufisadi. Pia, viongozi hao hao wanashirikiana na wageni kuwanyang'anya wakazi rasilmali ambayo wanaweza kutumia kujipatia riziki. Na kwa hivyo viongozi wanachangia pakubwa hali ya umaskini inayoendelea kukithiri. Hali hii inaendelea kudhihirika wazi katika maisha

ya kiuchumi ya wakazi kama ile ya wanakisangu ambao viwanda vyao vilifilisishwa na wakuu walioteuliwa kuvisimamia:

> Kile cha njugu za macadamia kilifikwa na hatma hiyo hiyo: usimamizi mbaya. Wasimamizi wenyewe wakawa wanatamwa maisha ya raha na ureda uliokithiri, kwenda likizo na jamaa zao Afrika Kusini; kwenda mandarin huko Riviera, nchini Ufaransa, na kulipiwa gharama kwenda kufanya manunuzi yao Uingereza, wakati wafanyi kazi wao wanateseka. Mishahara ya wafanyikazi na ujira wa vibarua ukawa haulipwi (uk. 201).

Mambo haya yanaendelea kushuhudiwa katika jamii. Kwa kutumia bunilizi, Wamitila anarejelea wakati ambapo nchi hii ilishuhudia kuanguka kwa kampuni nyingi hasa zilizokuwa zinashughulikia bidhaa za kilimo na hivyo kuwaacha wakulima wengi wakiwa hawana mahala pa kupeleka bidhaa zao. Kuna viwanda kama vya sukari ambavyo mwandishi anarejelea na ambavyo vilitegemewa na wakulima wengi magharibi mwa nchi, viwanda vya pamba na vinginevyo. Kutokana na haya, wananchi waliendelea kuwa masikini jambo ambalo linaendelea hadi sasa kwani hakuna viwanda ambavyo vimefufuliwa.

Kulingana na Wanyande (2001), akizungumzia kuhusu sekta ya sukari nchini, watu walio na mamlaka huingiza sukari nchini bila kulipa ushuru na kuiuza kwa bei rahisi kuliko sukari iliyotengenezewa hapa nchini. Hili linasababisha kutouzwa kwa sukari ya hapa nchini. Tatizo hili limeongezewa na ufujaji wa fedha zilizotengwa kuimarisha sekta ya sukari. Wanyande anasema sh. milioni 700 za hazina ya maendeleo ya sukari zilifujwa na mamlaka ya sukari na wafanyi biashara wengine wa kati. Hakuna ushahidi wowote unaonyesha kuwa walichukuliwa hatua zozote.

Katika nchi ambayo, kulingana na Kwaka (2011), kiwango cha ukosefu wa ajira ni asilimia 70, riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inaonyesha jinsi uongozi duni umeendelea kuchangia hali hii. Kama anavyosema, kulikuwa na wakati ambapo watu waliweza kujiajiri kupitia kwa kilimo huku viwanda vikitoa ajira na hivyo basi viwango vya

uchumi vilikuwa juu. Hata hivyo, miaka ya uongozi duni ambapo viongozi na wasimamizi wameendelea "kufyonza damu ya nchi hadi sasa imebaki kiwiliwili," imesababisha viwango vya umaskini kuongezeka kwa kiwango kikubwa nchini.

> Kumbukumbu yake ikarudi siku za zamani katika soko la kijijini. Siku hizo watu walichinja ng'ombe waliouzwa kwa kupima kwa mikono sio mizani; watu wakawa wanakula nyama vizuri. Maendeleo yalipokua kukazuka masoko makubwa kidogo; lile dogo likawa haliwezi kuchinja ng'ombe tena wakabakia kuuza nyama ya mbuzi au kondoo…..Uwezo wa watu wa kununua nyama ukawa nao unafifia; pesa zinawachenga hadi sasa ambapo kula nyama lilibakia tukio la nadra. Nyama na pesa zikafifia, zikapeperuka na kupotea kabisa (uk. 156).

Wamitila, katika *Msimu wa Vipepeo*, anaendelea kutuonyesha jinsi uongozi duni unavyoendelea kuchangia matatizo ya jamii. Badala ya kutafuta suluhu la umaskini unaoendelea kukithiri, viongozi wanatumia hali hiyo kujifaidi. Waziri Mkurutu alitumia fedha za umma kuanzisha mradi wa vipepeo huku akisingizia eti ni mradi wa wanakisangu utakaowasaidia kujinasua kutoka kwa hali yao ya maisha.

> Wote walitamani kujinasua kutoka kwenye umaskini uliowagandama milini, ukawasimika palepale wakabakia kuvuta miguu kwa nguvu zao zote kama mtu aliyezama kwenye dongo la kinamu msimu wa mvua za Masika (uk. 200).
>
> Waziri alichukua pesa za wizara zilizotengewa wagonjwa wa ukimwi kuanzisha mradi wa kufuga vipepeo. Kwamba mradi wenyewe haukuwa wa wana-Kisangu bali wake mwenyewe (uk. 278).

Kiongozi kama huyu ndiye Lumumba (2011, uk. 53) anayemwita "kiongozi duni". Anasema kiongozi kama huyu huongozwa na matamanio ya kusifiwa. Hujisifu kuwa anashikilia maono ambayo yeye tu ndiye anaeyaelewa huku wafuasi wake wakimfuata tu kama kondoo wanaomwaabudu kama miungu. Viongozi kama hawa wana ari na haiba lakini hutumia sifa hizo kujifaidi.

### 3.2.5 Kutegemea Misaada

Kutokana na umaskini uliokithiri, tunaona kuwa kuna matatizo mengi ambayo yanawakumba wananchi. Hata hivyo, viongozi waliopo hawaoni umuhimu wa kushauriana na wananchi katika juhudi za kukuza uwezo wao ili kutoa suluhu kwa matatizo yao. Kwa hivyo wanageukia suluhisho lililo rahisi na ambalo ni kutafuta misaada kutoka kwa wafadhili wa nje. Mwandishi anatumia masaibu ya watoto omba omba kuirai jamii kuliangalia kwa undani suala la misaada kwani mingine inatumiwa kuwadhulumu wananchi. Katika riwaya hii, wananchi na hata viongozi walifurahia kwamba mgeni mmoja alijitolea kuwasaidia watoto hawa kumbe alikuwa anawadhulumu hasa wale wa kike ambao walisafirishwa hadi ng'ambo kutumiwa kama makahaba:

> Tangu kuzinduliwa kwake, shirika la *Global Foundation* lilisifiwa na wengi sio tu jijini pia nchi nzima. Huduma zake - kuwasaidia watoto waliotelekezwa na wazazi wao - zilihongerwa na watu wengi; kuuondoa udhia wa watoto waliojazana jijini; wakajizungukia huku wanawavamia wenye magari; wakiwashurutisha kuwaadhiri wasipowasaidia. Lakini kilichowapendeza wengi ni kuwa wasimamizi wa makao yenyewe walifanya mengine muhimu zaidi. Watoto wa kike waliopelekwa makaoni, ambao walikuwa wengi kuliko wenzao wa kiume, waliishia kupata udhamini wa kwenda huko Ulaya kupata mafunzo maalumu na kuandaliwa kupambana na ulimwengu wa kesho (uk. 199).
>
> *Global Foundation* ilikuwa na mawakala katika mataifa ya kimagharibi. Huko Ujerumani kulikuwa na Bordello Agencies katika mji wa Frankfurt ambako watoto wa kike, wengine wenye umri wa chini ya miaka kumi na mitatu, wanazongomewa kwenye biashara ya ukahaba (uk. 212).

Licha ya haya kufichuliwa na vyombo vya habari, viongozi hawafuatilii kutokana na kuwa wao pia walishiriki katika uundwaji wa kampuni hiyo bila kujali ni nini itawafanyia watoto wao. Badala yake, serikali inawalaumu waandishi wa habari kwa kufichua kashfa hiyo:

> Zamani Rais Kamaliza Rungu wa Kioga alisema kuwa kuna haja ya kuwadhibiti hawa waandishi wa habari watu wakalalamika sasa hasara gani hii? Matope gani haya wanayopakwa mawaziri wazima wa nchi kwa nia ya kuwafukuza wawekezaji, malalamiko yalitamkwa (uk. 212).

> Waziri Mkurutu alisema kuwa atawashawishi mawaziri wenzake kuitetea *Global Foundation* hasa kwa kuwa inawahusisha wawekezaji wa nje…. Kwamba nchi haiwezi kufanya matendo kama hayo ambayo yanaweza kuwakasirisha wafadhili wakuu wa nchi. Kwa njia hii kupunguza kasma za mikopo ambayo ilikuwa tegemeo kuu la maendeleo nchini (uk. 218).

Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inatuambia kwamba viongozi wana haja zaidi na mikopo inayotoka kwa wafadhili na kwa hivyo wanaweza kutenda lolote wanalotaka hata kuwadhulumu wananchi mradi tu mikopo iendelee kuletwa. La kusikitisha ni kuwa mikopo hii haiwafaidi wananchi bali hao viongozi wenyewe. Tunaona viongozi ambao wanawajibikia wageni na sio wananchi waliowapa mamlaka:

> Waziri akamwangalia mwandishi wa habari kisha akasema, “Sisi tuko tayari kupokea msaada kutoka kwa yeyote yule. Mtu anayepewa mbuzi wa bwerere hamchunguzi meno. Tunaikaribisha misaada ya hao na hata ya wengine” (uk. 246).

Kutokana na haya, ni wazi kwamba viongozi hawataki kukuza uwezo wa wananchi kuweza kujitegemea bali wanaendeleza ile kasumba kwamba ili nchi iweze kuendelea, ni lazima itegemee misaada ya nchi za magharibi. Haya yanatiliwa mkazo na Tseggai (2006) anaposema kuwa misaada kutoka nchi za nje haijakuwa na faida kwa muda wa nusu ya mwongo mmoja uliopita. Ikiwa msaada huu ulitumika kukabiliana na njaa, magonjwa, utapia mlo, majanga na kuzorota kwa jamii, basi lengo lake halijatimizwa na manufaa yake hayapo barani Afrika. Anasema la kusikitisha ni kwamba katika mataifa yanayoendelea hasa barani Afrika, wengi wa viongozi na pia wale wanaoongozwa huona maendeleo kuwa yanatokana na misaada kutoka nje badala ya juhudi za wananchi. Naye Brautigam (2000) anasema kwamba misaada inaweza kuwa na maendeleo ya kudumu katika nchi ambazo zina uongozi na taasisi bora. Hata hivyo, mfumo uliopo wa kutoa misaada hautoi vichocheo kwa viongozi na warasimu katika nchi zinazotegemea misaada kutekeleza mabadiliko magumu katika sekta ya umma ambayo yataimarisha asasi hizi na, hivyo basi, kuwezesha misaada kutoa mchango

chanya kwa maendeleo. Kwa hivyo, tunaona kwamba uongozi bora ni muhimu kwa misaada kuweza kuleta maendeleo.

### 3.2.6 Ukiukaji wa Sheria

Mwandishi anaonyesha kuwa kuna sheria mwafaka kuwalinda wananchi kutokana na dhuluma kutoka kwa wageni. Katika riwaya hii, tunaona kuwa katika juhudi za kuwalinda wananchi, wageni hawaruhusiwi kuanzisha miradi yoyote bila kuwepo kwa wenyeji lakini viongozi wenyewe, wakishirikiana na wakuu serikalini, wanakiuka sheria hii. Kinaya ni kwamba wanaohitajika kuzilinda sheria hizi ndio hao hao wanaozikiuka na, badala ya kuwalinda wananchi, zinatumika kuwanyanyasa. Badala ya kuilinda sheria ya nchi, viongozi wamo katika mstari wa mbele kuivunja ili kujifaidi na kuwafaidi jamii zao. Wamitila anatoa picha ya mkuu wa sheria ambaye amesomea na hata kubobea katika taaluma hiyo. Lakini badala ya kutumia ujuzi alio nao kuihudumia nchi, mwanasheria huyo anatumia ujuzi huo kuvunja sheria zinazofaa kuwalinda wananchi ili yeye na rafiki yake waziri na wawekezaji wa nje wapate kujinufaisha:

> Waziri Mkurutu alikuwa akiyacheua mazungumzo yake na rafiki yake, Fabio Mkalla. Alishamfahamisha kuwa ile mipango ya uwekezaji ya Adolf Dieter ilikuwa imefikia ngazi za juu sana. Kwamba wakati wowote atakisajilisha kituo cha kuwatunza mayatima na watoto wa mitaani. Kwamba mwanzoni palikuwa na tatizo kutokana na sheria za nchi ambazo zinamkataza raia wa kigeni kuanzisha kituo kama kile bila ya kuwepo na ushirika wa wenyeji. Kwamba sasa hali hiyo ilishakiukwa baada ya waziri kupendekeza jina la mpwa wake na Fabio naye shemeji yake. “Nchi hii unajua siasa yake ilivyo, huwezi kulitumia jina lako moja kwa moja,” alisema waziri (uk. 86).

Pia, mkuu wa sheria anatumia mamlaka yake kusitisha kesi dhidi ya Gattuso Berlusconi, licha ya kuwa amewanyang’anya wananchi wa Kisiwandeo njia zao za kujipatia riziki baada ya kuwakataza wasivue samaki kwa kuwa maji na samaki waliokuwa pale ni miliki yake. Pia, kampuni yake GB ambaye alikuwa Mmarekani ilikuwa inachafua maji katika kisiwa hicho na hivyo basi kuyaharibu mazingira. Lakini Waziri Mkurutu

alikuwa tayari kumtetea kwa vyovyote vile huku rafiki yake Fabio akitumia sheria kumsaidia Mmarekani huyo:

> Na alikuwa hata tayari kutoa machozi yake kuitetea serikali yake dhidi ya shutuma za kuiruhusu kampuni ya Kimarekani kuyachafua maji ya bahari huko Kisiwandeo. Kwani hayo madogo? Jipu la pekee lililomsumbua rafiki yake Adolf Dieter (kutiwa rumande kwa rafiki yake Gattuso Berlusconi) lilishapata ufumbuzi, likapasuliwa na kuminywa na Fabio Mkalla, kwa niaba ya serikali, aliyekatiza mashtaka dhidi yake kwa kutumia mamlaka ya kisheria ya *nolle prosequi.* Alishamfahamisha kuwa aliwasiliana na idara iliyohusika ya polisi na kuyakinisha kuwa hapakuwa na uchunguzi uliowezesha kushtakiwa kwa Gattuso; kuwa hata baadhi ya mashahidi waliokuwa tayari kuutoa ushahidi wao mahakamani (wavuvi wa Kisiwandeo) walishaghairi na kwamba ule mvuvumko uliokuwako kabla ulishanywe (uk. 146).

Wajibu mkuu wa mahakama ni kutetea haki za walioathiriwa na kutoa hukumu bila kuegemea upande wowote, lakini katika nchi hii hili halifanyiki. Riwaya hii inaonyesha hali ambapo mahakama inaegemea upande wa wenye mali hata katika suala ambalo linawaathiri wengi na ambalo ni wazi kwamba hao matajiri wamo lawamani. Kwa hivyo wananchi wanabaki bila mtetezi ama hata mahali pa kukimbilia wanapodhulumiwa.

> Chama cha wanamazingira kilijaribu kuwapeleka wenye viwanda mahakamani. Wanachafua jiji; wanayaharibu mazingira yetu, walisema. Lakini mahakama iliyohusika ilifutilia hiyo kesi mbali kwa kusema kuwa hapakuwa na ushahidi wa kisayansi wa kutosha kuwahukumu waliohusika. Wiki moja baadaye wakili mmoja wa serikali aliuliza swali la balagha: ni nani aliyewadanganya hawa jamaa kuwa wanaweza kushinda kesi ya namna ile? (uk. 109).

Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inatuonyesha kuwa ingawa ni kweli kuwa mara nyingi wageni wanawanyanyasa wenyeji, wanafanya hivyo kwa kusaidiana na walio katika mamlaka wanaovunja sheria ya nchi ili kujinufaisha wao binafsi. Na kwa hivyo wanaofaa kulaumiwa sio wale wageni lakini wanaotumia mamlaka yao vibaya kuwasaidia kuwadhulumu wananchi. Vile vile, wenyeji walio na mali wanatumia mali yao kuvunja sheria sio tu kuwadhulumu wananchi lakini nchi yenyewe. Hivyo basi, miaka mingi baada ya kupata uhuru cha kulaumiwa sio ukoloni mambo leo bali tatizo

limo miongoni mwetu kwa wale ambao tumewapa mamlaka. Hii ndio dhana ya ndani nje ambapo tunaona kuwa ni kweli kwamba wageni wanaendelea kuwanyanyasa wenyeji lakini ni wazi kwamba wanafanya hivyo kwa kushirikiana na walio mamlakani. Haya yanadhihirishwa na nadharia ya uhistoria mpya ambayo huhusisha matatizo ya kijamii na siasa kwa kuyaweka katika muktadha wa kihistoria na kitamaduni.

### 3.2.7 Ufasiri wa Uongozi katika *Msimu wa Vipepeo*

Kwa mujibu wa nadharia ya uhistoria mpya, itikadi zinazobaini fasihi lazima zitafitiwe na kuhakikiwa kwa njia za kijamii, kisiasa na kiuchumi za kipindi kinachozungumziwa (Balkaya, 2014). Kwa hivyo kazi hizi huenda zisitueleze au zitueleze ukweli wa ulimwengu lakini hutueleza mawazo kuhusu mpangilio wa jamii, dhuluma, miiko nk. Katika kazi hii tunashuhudia migawanyiko mikubwa katika jamii ambapo wenye uwezo ndio wanapata chochote wanachotaka huku wasio na uwezo wakiendelea kudhulumiwa katika jamii. Tunaona viongozi wanaoshirikiana na wageni kuwadhulumu na pia kuwanyang’anya wananchi rasilmali yao. Viongozi wanaotoa uamuzi wa kibinafsi kuhusu mali ya umma na ambao hawajali maslahi ya umma uliowachagua lakini badala yake wanatumia uongozi kujifaidi. Kwa viongozi, wadhfa wanaopewa sio wa kuwatumikia wananchi lakini unawapa nafasi ya kufikia rasilmali za umma na kuzitumia kuendeleza mahitaji yao ya kibinafsi. Ni viongozi ambao wako radhi kuwanyanyasa wananchi kwa kuvunja sheria ili iwafae wenyewe na wageni wanaoshirikiana kuendelea kuwanyanyasa wenyeji.

## 3.3 Wananchi na Uongozi

Huku viongozi wakilaumiwa kwa yanayoendelea katika jamii, wananchi pia hawajawachwa nyuma. Kwa mujibu wa Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, wananchi pia wanachangia hali iliyoko kwa kutowajibika na kuwaacha viongozi watende

wapendavyo. Huu ndio mtazamo wa ndani nje ambao waandishi wa riwaya ya kisasa wamechukua katika kuangazia tatizo la uongozi duni ambalo limeendelea kushuhudiwa katika jamii.

### 3.3.1 Kutojali kwa Watawaliwa

Kaiser na wenzake (2007;179) wanazungumzia uongozi duni kwa kutumia mfano wa pembe tatu iliyo na sumu. Kwa mujibu wao, pembe hii inahusisha watawala, watawaliwa na mazingara. Wanasema kwamba viongozi, pamoja na wanaotawaliwa na mazingira yaliyomo, huchangia katika kupata uongozi hasi au chanya. Haya tunayapata katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* tunapoangazia vitendo vya wananchi na mazingara yaliyomo katika jamii ya riwaya hii. Tunayaona mazingara ya umaskini uliowala wananchi hivi kwamba wamekosa matumaini na hivyo basi wanamfuata yeyote ambaye wanafikiria anaweza kuwatoa ktikaa hali yao. Kulingana na mwandishi, wananchi wanachangia uongozi duni kwa kutojali yanayoendelea nchini. Katika kufanya hivi, mwandishi anaonyesha kuwa wananchi hawatekelezi wajibu wao kuhakikisha kuwa kuna uongozi bora bali wanawaacha viongozi wafanye watakavyo. Wamitila anatuambia kwamba wananchi hawana ule umoja utakaowawezesha kupigania maslahi yao na, kwa hivyo, hili linafanya wao kutumiwa vibaya na viongozi. Wahenga walisema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Udhaifu huu wa wananchi unatumiwa na viongozi kuendelea kuwanyanyasa.

> Alishasoma kwenye magazeti wakati mbunge wa eneo hilo alipolalamika kuhusu watu wa eneo bunge lake kuwa watumwa wa Bodi ya Umwagiliaji maji ya Mwetare. Yeye kama raia wengi nchini hakujali; na ajali nini na ni jambo ambalo halimhusu Be wala Te? Si ndiyo falsafa ya nchi nzima hiyo? Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi? (uk. 15).

Wamitila anatoa picha ya wananchi ambao wanadanganywa na hatua ambazo si za kweli lakini wao wanaridhika tu. Hili linatoa mazingira bora kwa viongozi kutojali na

jinsi wanavyotekeleza majukumu yao. Wanajua kwamba watawadanganya wananchi kwa muda na hatimaye watasahau na kuendelea na maisha yao ya kawaida. Licha ya kupata uhuru, hali ya kujidhalilisha haikutoka kwa akili ya wakenya wengi.

> Siku nne baadaye GB alikamatwa na polisi waliosema kuwa hawangeweza kukaa bwete na kuona sheria za nchi zimekiukwa…Magazeti ya kila siku yalichapisha picha za maandamano ya wakazi wa Kisiwandeo wakihongera uamuzi wa serikali na hata kuthubutu kudai kuwa hawakuwa wametengwa kama walivyofikiria hapo kabla (uk. 124).

> Jay…Hii ni nchi ambayo imekula kuchakulo kama wasemavyo watu kijijini…haina kumbukumbu kabisa! Umma hushikwa na hisia zinazowapanda na kuwajaa akilini kisha zinanywea kama puto kubwa linalodungwa kwa sindano; hunywea na kunyong'onyea kabisa! (uk. 146).

Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inatuambia kuwa viongozi wameshawasoma wananchi na kujua kile wanahitaji kufanya ili wawapumbaze na hivyo basi kuepuka ghadhabu yao. Wamejua kwamba wananchi hawatathmini vitendo vyao. Hii ndio maana Waziri Mkurutu anapopatikana na kashfa ya uharibifu wa mazingira, analia. Kule kulia katika tamaduni ambapo mwanaume hafai kulia hadharani kunawafanya wananchi kumwamini na hata kulisahau suala lenyewe (uk. 101). Riwaya hii *Msimu wa Vipepeo* pia inatuambia kwamba hali hiyo ya kutojali kwa wananchi inawafanya viongozi kutenda lolote bila kujali kwani wanajua hakuna chochote ambacho wananchi watafanya. Wanajua kuwa hata wanapokasirika, ni kwa muda tu na hatimaye wanasahau na kuendelea na maisha kama kawaida.

> Alimweleza kuwa hisia hizo za umma zilikuwa kama nguvu ya povu, povu lenyewe linaongezeka na kuvimbiana lakini ukipuliza baada ya muda linayeyuka na kupotea kabisa - hali ikarudi kuwa kama awali (uk. 124).

Kwaka na Thuranira (2011;35) wanasema huku wapiga kura shupavu wakitarajiwa kusaka habari na kuchagua kiongozi kulingana na maisha yake, rekodi, maadili, imani, miradi yake ya maendeleo na sera zake ambazo anataka kuimarisha, wapiga kura nchini huathiriwa kwa urahisi na pesa kidogo na kabila au ukoo wa mwaniaji. Haya yote ni

matokeo ya miaka ya wananchi kunyimwa uwezo, hivi kwamba wanashikilia uaminifu usio na manufaa kwa kabila na kukubali pesa zinazotosha chakula cha siku moja ili kuamua watakavyopiga kura. Mwanasiasa anaelewa fika haya na kwa hivyo hutumia ukabila na umaskini uliokithiri kuwapa pesa na hivyo basi kuwalaghai wapiga kura. Matendo haya ya wananchi yanasaidia kuhalalisha tatizo lililopo nchini la uongozi duni.

Pia tunaona wananchi wanaokubali kutumiwa na wanasiasa kupigana vita vyao kwa sababu yeye (mwanasiasa) ni mmoja wao ilhali anapokula mali ya nchi anakula peke yake. Hii ni hali ambayo imeendelea kushuhudiwa katika nchi zetu ambapo haijalishi mwanasiasa ametenda kosa gani kwani anakimbilia jamii yake ambayo humuunga mkono. Tunaona wananchi ambao wanadanganyika kwa urahisi bila ya kuangalia kwa undani suala ambalo kiongozi wao amehusishwa nalo. Mradi tu ni kiongozi wao, wanakubali kuzama naye licha ya kuwa kitendo alichotenda kinawaathiri hata wao wenyewe. Mwandishi anawakumbusha kwamba ni lazima wajihusishe na yanayoendelea nchini na pia wasikubali kuhadaiwa na vitendo vya viongozi na hatimaye kusahau maovu wanayofanyiwa.

> Alishawasiliana na wana-eneobunge lake nao wakaitikia kilio cha kiongozi wao; ni kiongozi wao na wasemacho; chako kikioza ni chako. Wakaandamana huku wamebeba mabango kuwalaumu wapinzani wake wa kisiasa wakalalamika kuwa mbunge wao alikuwa anaonewa na watu ambao waliona gere kutokana na maendeleo yake; wakapaaza sauti kutangaza jinsi watu wa jamii yao wanavyoonewa katika nchi yao; kwamba hata hizi zilikuwa njama za nchi za Ulaya (uk. 250).

Kabeberi (2011) anasema ikiwa wananchi hawatatekeleza wajibu wao na kuweka watu wasio na maadili mamlakani, serikali itaharibika. Sheria zitatungwa, sio kwa manufaa ya umma bali ya kibinafsi. Watu wafisadi watapewa nafasi ya kutekeleza sheria zilizotungwa, mali ya umma itatumiwa kwa watu wasiofaa na haki za wananchi zitakiukwa. Kwaka (2011) anamnukuu Noah Webster, mmarekani mzalendo na mtaalam, akisema mwananchi ana wajibu muhimu kuhakikisha kwamba viongozi walio

na maadili wanachaguliwa kushikilia mamlaka. Mtalaam huyu anahusisha utungaji wa sheria nzuri na uongozi bora na jukumu ambalo wapiga kura hutekeleza katika kuwachagua viongozi.

Kutokana na kutowajibika kwa wananchi katika uongozi, inakuwa ni rahisi kwa viongozi kuwahadaa. Wanajua kuwa wananchi hawajali wanalotendewa na kwa hivyo inapokaribia uchaguzi, wanarudi nyumbani na kuwandanganya na miradi ya hapa na pale ili waweze kuchaguliwa tena. Hili linaeleza ni kwa nini viongozi hawa wanapochaguliwa hawana haja ya kuwahudumia wananchi kwani hiyo haikuwa nia yao. Wanajua kwamba jinsi ya kupata uongozi katika jamii ni kuwandanganya wananchi kwa kuanza kuwatembelea pindi tu uchaguzi unapokaribia na pia kuanzisha miradi ya kuwafunga macho na baada ya kuchaguliwa wanatoweka.

> Siku hizi alishaanza hata kurudi huko mashambani (kwa kuwa msimu wa uchaguzi haukuwa mbali) na kuwasaidia watu wa eneo Bunge Lake. Walishachimbiwa chemchemi za maji (uk. 161).

Kwaka na Thuranira (2011) wanatoa rai yao kwamba wakenya hawakuelimishwa wala kuhamasishwa wakoloni walipoenda. Kwa hivyo, kwao, tabaka la waafrika waliokuwa na elimu na waliochukua mahala pa wakoloni walichukua nafasi kuu ambayo ilikuwa ya mkoloni katika akili ya Mkenya wa kawaida. Matendo yake na tabia hazingeweza kupingwa, kwa hakika, yeyote aliyekuwa kwa mamlaka au alikuwa na utajiri mwingi kama ule wa mkoloni alienziwa bila kujali alikotoa utajiri huo. Na kwa hivyo si jambo la kustaajabu kwamba mwanasiasa Mkenya hii leo au mrasimu anaweza akawapotosha watu, aibe mali ya umma na asifanyiwe chochote huku mwananchi wa kawaida akimsifu kwa kuwa mfanyi kazi shupavu. Ni katika hali hii ya wananchi kutopewa uwezo ambapo marais wa Kenya na wenzao katika mamlaka wameweza kuwanyanyasa na kuwazamisha katika umaskini bila ya kufanyiwa chochote. Kwa hivyo, mwananchi,

wa Kenya humtambua tu mwanasiasa, wafanyi kazi wakuu serikalini na mtu tajiri kama kiongozi.

Hii ndio hali ambayo mwandishi anataka wananchi kupigana nayo ili waweze kujikomboa kutoka kwa uongozi duni. Katika riwaya hii, Wamitila anajaribu kuwazuzua wanajamii kuiangalia hali yao upya na kujikwamua kutoka kwa hali hiyo. Mwandishi, kwa kutumia mwelekeo wa ndani nje, anawarai wananchi kutokubali kudanganyika kwa urahisi wanapowachagua viongozi na badala yake kuwachunguza kwa undani badala ya kutumia kigezo cha utajiri kama sifa kuu ya kutafuta kiongozi. Katika eneo la Kisangu, tunaona kuwa kufilisishwa kwa viwanda kumechangia pakubwa kuzorota kwa hali ya uchumi katika eneo hilo. Lakini uchaguzi unapowadia, Mkurutu anakuja na kuwajengea kituo cha polisi baada ya kusikia kuwa kulikuwa na tatizo la usalama na kutokana na hilo anachaguliwa. Wakazi wa Kisangu hawaulizi fedha alizitoa wapi wala kutoa mahitaji yao kwa mbunge huyo kabla ya kumchagua. Pia, badala ya kuwachagua viongozi ambao kwa pamoja watashirikiana kutatua matatizo yao, wanangoja kufanyiwa. Hawachagui viongozi ambao watawasaidia kujikwamua kutokana na matatizo yanayowakumba lakini yeyote anayewaahidi kuwatendea jambo ndogo anakubaliwa.

### 3.3.2 Wananchi na Ufisadi

Wananchi pia wanajipata lawamani kwa kuchangia katika wizi wa rasilmali za nchi. Hii ni kwa sababu wanawasifu wanaotajirika bila ya kujali wanapotoa utajiri huo huku wakiwakashifu wanaotegemea jasho lao. Kwa hivyo ni jambo la kawaida kwa mtu kuitumia afisi kujitajirisha na yule ambaye hafanyi hivi basi hafai kupewa hata hiyo nafasi ya kuhudumu. Tunaona wananchi ambao hawaheshimu wanaotumia jasho lao kupata mali bali wale wanaotumia afisi bila ya kujali jinsi hili linavyowaathiri. Na kwa

hivyo hata hao wananchi wakipata nafasi ya kuhudumu kama viongozi watashiriki ufisadi kama tu viongozi wao. Wamitila anatuambia kuwa mfanyikazi ambaye hashiriki ufisadi na hivyo kustaafu akiwa masikini anakashifiwa. Kwa hivyo hili linachangia pakubwa ufisadi kwani wengi watafanya kila juhudi kujitajirisha ili wasije wakakumbana na fedheha wanaporudi kwa jamii baada ya kustaafu.

> Kwenda nyumbani na watu kumshangaa. Alikwenda Kitambaasie kufanya nini huyu na hana anachotushinda nacho isipokuwa huko kuja huku kutoka jijini na mikate mikubwa ya bofulo? Wengine wakamsubu, wakamkashifu kwa kuwa mwoga, mtu aliyehiari kuzamishwa chini na nanga ya madeni badala ya kuitegemea nundu ya shirika (uk. 155).

Mwandishi anawaambia wananchi kuwa, kwa vitendo vyao, wao pia wanachangia pakubwa yanayoendelea nchini. Katika kazi yake, Wamitila ameangazia mchango wa wananchi katika mchakato wa uongozi. Kwa mujibu wa riwaya hii, licha ya kuwa wananchi wanadhulumiwa na viongozi, wanakumbushwa kuwa wao pia wanachangia hali hii kwa kutojali yanayoendelea katika nchi. Kwamba mara nyingi wanadanganywa na kuhadaiwa na viongozi kwa sababu hawana umoja na pia hawatathmini vitendo vya viongozi wao.

### 3.4 Suluhisho Lililopendekezwa

Kwa mujibu wa nadharia ya uhistoria mpya, mwandishi haathiriwi tu na jamii anapoandika kazi yake bali pia anaiathiri jamii. Kwa hivyo anapoangazia matatizo yaliyomo katika jamii, vile vile anatoa suluhu ambazo kulingana naye zitasaidia kukabiliana na matatizo aliyoyazua. Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mwandishi ameyaangazia matatizo ya uongozi ambayo yanasababishwa sio tu na viongozi bali pia wananchi kama njia moja ya kuiathiri jamii. Wamitila, katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, anatoa mapendekezo ambayo kwake yeye yanaweza kuwa suluhu kwa udhaifu aliyouangazia katika kazi yake. Kama Dogan (2005, uk. 92) anavyosema, “matini kwa upande mmoja huunda mahitaji na matamanio ya jamii na kwa upande mwingine ni

wakala unaosaidia kuunda jamii upya”. Tunaona kuwa waandishi kupitia riwaya ya kisasa wanajitahidi kuunda jamii mpya kwa kurekebisha hali ya uongozi ambao ni duni. Kama Julius Nyerere, akinukuliwa na Lumumba (2011), anavyosema:

> Kwa hakika tatizo la Afrika ni uongozi duni usiokuwa na maono. Lakini kwangu mimi, siri ya maendeleo ni watu, ardhi, na siasa safi na vile vile vijana wenye malezi bora, siha njema na bongo kali. Hivi vyote lazima viambatane na uongozi bora. Kila kiongozi lazima akumbuke ya kwamba uongozi ni kama hekalu na mahali patakatifu pa kutoa huduma kwa kujinyima kwa maslahi ya umma.

Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inayatimiza haya kwa kuangazia uongozi bora ambao jamii inatarajia katika juhudi zake za kupata viongozi watakaorejesha imani ya jamii kwa uongozi na pia uongozi utakaowezesha jamii kuendelea.

Katika kuangalia suluhu iliyopendekezwa, tunaangazia sifa kadhaa ambazo tutatumia kusawiri uongozi bora ambao unapendekezwa na waandishi kama suluhu la matatizo ya uongozi yanayoangaziwa.

### 3.4.1 Uaminifu

Uaminifu ni muhimu sana katika uongozi kwani kiongozi akiwa mwaminifu, hata anaowaongoza wanakuwa na imani naye. Kiongozi mwaminifu hushikilia kile anachokiamini na maadili hata pale ambapo kuna ushawishi mkubwa wa kwenda kinyume na maadili. Uaminifu wa kiongozi hauonekani kwa kuangalia tu bali unatokana na vitendo vyake.

Mwandishi anatuambia kuwa kuna uwezekano wa kuwa na viongozi waaminifu na wanaowajali waliowachagua. Anatuonyesha kuwa inawezekana kwa viongozi kuwahudumia watu na kuwasaida kujikwamua katika hali yao ya umaskini ingawa viongozi kama hao ni wachache. Viongozi hawa wanawafanyia watu wao kazi na kujaribu wawezalo kuimarisha hali yao ya maisha. Hili linawawezesha kujiwekea bima ya kuchaguliwa tena badala ya kuwahadaa wananchi. Mwandishi anatuonyesha kuwa

kuwahudumia wananchi ni muhimu zaidi kuliko kujilimbikizia mali. Kwamba viongozi wanapoimarisha hali ya wananchi, wanakuwa na imani nao na uongozi wao na hivyo watawachagua tena na tena. Hivyo basi mwandishi anawashauri viongozi kuwa, ili waweze kufaulu katika uongozi, ni lazima uongozi wao uyaangazie matatizo ya wananchi. Katika kufanya hivyo, hawatahitaji kuiba fedha za umma ili wahongane wanapotaka kuchaguliwa tena lakini wananchi watawachagua kutokana na waliyowatendea.

> Kila alipomwangalia mbunge wa jimbo jirani la Mwetare, Kembo Ndura, alimwonea gere. Yule alishajiwekea bima ya ubunge wenyewe - kuhakikisha kuwa raia wa pale, waliokosa mashamba kwa muda mrefu, wamepata vikataa vyao; vikataa hivyo vilikuwa kama nyongeza ya damu ya uhai wao (uk. 173).

### 3.4.2 Kiongozi Anayewapa Uwezo Anaowaongoza

Huyu ni kiongozi ambaye anajitahidi kuwapa anaowaongoza uwezo kiuchumi. Kiongozi huyu hujua kuwa hafai kuwanyanyasa wengine ili yeye afaulu. Hii ndio aina ya uongozi ambao unakashifiwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo.* Uongozi ambao huwanyanyasa walio chini kwa kutumia mali yao na kuchangia pakubwa umaskini unaoendelea kushuhidiwa. Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inanuia kuyabadilisha haya kwa kutoa mfano wa mbunge Ndura. Anatuambia kuwa kuna viongozi ambao bado wana utu na ambao hawasahau walikotoka. Hata hivyo serikali haiwathamini viongozi ambao wanapigania maslahi ya wananchi na hivyo basi haiwapi motisha wengine ambao wangependa kuimarisha hali hii. Badala yake, tunaona wanaoshiriki ufisadi wakipewa kazi kubwa kubwa na wanaowajali wananchi wakiwekwa pembeni na hata kufutwa kazi. Kupitia kwa Ndura, tunaona kiongozi ambaye anaelewa matatizo ya jamii yake na wanapomchagua kama kiongozi wao, anaitumia nafasi hiyo kupigania maslahi yao. Ni kiongozi ambaye haitoroki jana yake lakini kwa kuwa amekulia katika mazingara yayo hayo, anatumia nafasi watu wake wanayompa kama mbunge kuangazia

na kutafuta suluhu ya matatizo yao. Suala la umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi na wananchi linajitokeza kwani ni kutokana na ushirikiano huu ambapo maendeleo yanapatikana.

> Mabadiliko ya eneo la Mwetare yasingepatikana kama sio kutokana na kushirikiana kwao na mbunge wao, Kembo Ndura, ambaye aliwapigania mpaka wakaishia kupata hiyo ardhi ndogo waliyokuwa nao. Si hilo tu. Kembu Ndura aliweza kuwaunganisha watu wa makabila ya Ingwari, Atiriri na Asi kwa njia nzuri sana……Ikiwa huyu Ndura wetu hakuteuliwa kuwa waziri basi sijui nchi hii inataka viongozi wa aina gani! (uk. 61).

### 3.4.3 Kiongozi Mkakamavu

Sifa nyingine ni ile ya ukakamavu. Kiongozi bora wa siasa ni yule ambaye hafichi ukweli ili aonekane mzuri mbele ya watu bali huongea ukweli jinsi ulivyo hata kama wengi hawataki kuusikia ukweli huo. Nia yake si kuwafurahisha watu na katika hali hiyo kuwapotosha. Ili kutenda haya, kiongozi anahitaji ukakamavu na ambayo ni sifa moja ya uongozi bora. Maelezo haya yanalingana na ya mwandishi anapotuelezea kuhusu Waziri Fumo. Anatwambia kuwa ni lazima kuwe na viongozi ambao ni mashujaa na ambao wataweka maslahi ya nchi mbele hata kama wanakabiliwa na tisho la kufutwa kazi. Katika riwaya hii, tunaona jinsi ufisadi umekithiri hata katika ngazi za juu serikalini, hivyo basi inahitaji kiongozi shujaa ambaye anaweza kusimama na ukweli na kwenda kinyume na hata kiongozi wa nchi. Licha ya kuwa kila kiongozi anashiriki ufisadi na ubinafsi, kuna uwezekano pia wa kuwa na viongozi wanaopigania maslahi ya umma.

> Waziri Fumo alikuwa mchapakazi, mtetezi wa haki za wakulima, na waziri wa pekee aliyejitolea kupinga baadhi ya mapendekezo ya wafadhili wakuu wa nchi kuhusu mabadiliko katika sekta ya ukulima. Alishikilia kuwa ilikuwa lazima serikali ihakikishe kuwa viwanda vya nchini havitahatarishwa na uingizaji wa bidhaa kutoka mataifa ya nje. Kwamba nchi ndogo kama yetu haiwezi kuvikubali viwanda vikubwa ambavyo vinakuja kuisonga shingo ya uchumi wa jamii. Waziri Fumo alikuwa waziri wa pekee aliyefutwa kazi katika mabadiliko hayo (uk. 154).

Wamitila anatueleza kwamba uongozi bado ni muhimu katika jamii na kwamba licha ya kuwa na viongozi wengi ambao hawajali maslahi ya umma, bado kuna matumaini kwani kuna wachache ambao wana nia njema kwa nchi.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii, imedhihirika kwamba kutokana na yale ambayo tumeyaangazia, viongozi wanachangia pakubwa hali iliyoko katika jumuiya iliyoshughulikiwa na riwaya hii. Viongozi hao wanaendelea kufuja fedha za umma badala ya kuzitumia kukabiliana na hali ya wananchi, wananyonya danga ya nchi wakiwaachia wananchi makombo. Huku wananchi wakiendelea kuishi katika umaskini uliokithiri hata kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula na afya, viongozi wanatumia fedha zao (wananchi) kuishi maisha ya ubadhirifu. Viongozi wanashirikiana na wageni kuwanyanyasa wananchi huku wakijali zaidi misaada inayotoka ng’ambo kuliko hali ya wananchi waliowachagua. Kwa upande wao, wananchi wanalaumiwa kwa hali inayowakabili. Ni wananchi ambao wanadanganywa kwa haraka na viongozi na wanasahau wanayotendewa. Hawawajibiki na kwa hivyo viongozi wanatumia hali yao kuendelea kuwanyanyasa. Hata hivyo, mwandishi anatuambia kuwa inawezekana kwa viongozi kubadilisha hali hii akitumia viongozi ambao, licha ya kukosa usaidizi kutoka kwa serikali, wanajitahidi kuchangia kuimarisha maisha ya wananchi. Anawashauri viongozi kuwahudumia wananchi kama njia kuu ya kuhakikisha wanachaguliwa tena badala ya kushiriki ufisadi kwa lengo la kuwanunua wananchi wakati wa uchaguzi.

# SURA YA NNE

# TASWIRA YA DINI KATIKA RIWAYA YA *PARADISO*

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunaangazia jukumu la asasi ya dini katika jamii. Hii ni asasi ambayo inatakiwa kukemea maonevu ya kijamii, kutetea wanyonge na hata kuwakosoa viongozi miongoni mwa wengine. Hata hivyo, ili kutimiza haya, lazima asasi hii iwe inaongozwa na watu ambao wana maadili. Hata hivyo, mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anatupa picha ya uongozi wa dini ambao umejaa ulafi, tamaa ya pesa, ufisadi na unyanyasaji wa wanyonge. Tunaangalia pia mchango wa wafuasi katika kuzorota kwa asasi hii. Mwisho, tunaangazia yale mwandishi Habwe anayoyapendekeza katika kubadilisha hali hii.

## 4.2 Umuhimu wa Dini

Dini, iwe imejikita katika tamaduni za Kiafrika au iwe ni dini ya kisasa, ina wajibu wa kuwaokoa watu kutoka kwa yale yote yanayowanyanyasa katika nyanja za kisiasa, kijamii na hata kiuchumi. Pia, jukumu la kidini la dini yoyote ile katika ujenzi wa taifa ni kuhimiza waumini wote kupendana bila kujali misingi yao ya kikabila, rangi au imani mbali mbali (Kasomo, 2010). Kutokana na haya, tunaona umuhimu ambao umepewa asasi hii tangu jadi na ndio maana asasi hii inaangaziwa kuona kama inatimiza matarajio haya ambayo imewekewa na jamii. Woodbridge na Semmelink (2013) wanasema kwamba kama vile Mungu aliliita taifa la Israeli, kuwa mashahidi wa kinabii katika mataifa, Mungu bado analiita kanisa kuwa mashahidi wa kinabii na kuleta haki katika jamii. Wanaendelea kusema kwamba kama ilivyokuwa katika taifa la Israeli wakati wa nabii Amos, unyanyasaji wa masikini bado unaendelea katika jamii yetu. Katika uk. 93, wataalam hawa wanaendelea kusema kwamba unabii wa Amos ni changamoto kwa kanisa barani Afrika leo. Kwa hivyo ni changamoto kwa viongozi wa dini kuchukua

wajibu wao kama wawakilishi wa Mungu katika jamii (kama ‘chumvi na mwanga’) na kukemea maovu ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

### 4.3 Uongozi wa Dini

Tukizingatia nadharia ya uhistoria mpya, Bhat (2014) anasema kuwa nia yake kuu ni kuangalia kazi ya kifasihi kwa kuzingatia usuli wake kihistoria na kuangazia hali ya kijamii na kiutamaduni. Wananadharia hii, huchambua matini kwa kushirikisha katika tathmini matini za kifasihi na zisizo za kifasihi ambazo huenda zilimwathiri mwandishi wakati wa kuandika kazi yake. Na hivyo basi ni muhimu kufahamu uhusiano kati ya matini, hali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Anasema kuwa kila matini ni diskosi inayoashiria hali halisi. Katika riwaya ya *Paradiso*, mwandishi anatupatia hali ya kusikitisha katika asasi ya dini ambapo viongozi wanasawiriwa kama fisi wanaowala kondoo wao. Ulafi, ulimbikizaji wa mali na kutojali maskini unaoshuhudiwa katika siasa ndio ule ule unaoshuhudiwa katika dini. Habwe anatuambia kwamba katika jamii ya kisasa, viongozi wa dini wamechukua makanisa na kuyageuza kuwa mali inayomilikiwa na mtu binafsi yaani, kiongozi anayesimamia kanisa fulani. Kwa vile ni mali yake, anatumia fedha za kanisa kadri anavyotaka huku hata sherehe za kanisa zikigeuzwa na kuwa sherehe za familia. Kwa hivyo makanisa haya yamekuwa si ya waumini tena bali ni mali ya familia huku yakimilikiwa na bwana, bibi na wana wao.

> Isitoshe, New Jerusalem lilinasibishwa na Bwana na Bi Joshua Bosire. Hili lilidhihirika wazi wakati wa siku kuu za kanisa hili. Sherehe zote zilijikita kwenye Joshua na mkewe Lona na familia yao (uk. 67).

Viongozi hawa wamejawa ubinafsi hivi kwamba wanatumia fedha za kanisa kujiwekezea mali pamoja na wanao pasi na kujali hali ya wafuasi. Wanasawiriwa kama watu ambao hawajali maisha ya wafuasi wao na badala yake mali yote ya kanisa inaelekezwa kwao. Wanaishi maisha ya raha na hata mali inayosalia wanaitumia

kuwawekezea wanao. Badala ya kuwashughulikia wale wanaohitaji, wanawekezea wanao kwa maisha ya baadaye. Watoto wa Boribori:

> … wako katika shule za nchini. Wawili wanasomea Karen Academy na wengine wawili wako katika chuo kikuu cha Kianda; kila mmoja ana gari lake. Wengine wawili wadogo walipelekwa shuleni na dereva mmoja wa pale New Jerusalem; Bwana Mwangi. Moja katika miradi ya pale kanisani ni kuwabwaga na kuwazoa kutoka shuleni wana wa mchungaji. Kila mtoto katika hawa amefunguliwa akaunti katika benki ya Baroda. Licha ya akaunti, Boribori aliwafungulia bima za maisha na za masomo katika shirika la Bima la British Assurance. Alikuwa na mtoto mvulana mmoja, Jim. Jim ashanunuliwa nyumba mbili Marekani katika mji wa New York (uk. 213).

Haya yanadhihirisha yale yanayoshikiliwa na wananadharia wa uhistoria mpya kwamba matini ya kifasihi haitokani na ombwe tupu bali huwa inatokana na hali halisi katika jamii. Kama Sharma (2014, uk. 2) anavyosema, "nadharia ya uhistoria mpya huangalia matini iwe ya kifasihi au la kwa kusisitiza umuhimu wa kuzingatia hali ya kitamaduni ya wakati ilipoandikwa, maana, athari na jinsi itakavyotafsiliwa na pia kuitathmini". Anaendelea kusema kwamba matini ya kifasihi huzalishwa na kutimizwa katika hali yake ya kitamaduni na wala si katika ombwe tupu.

Hali hii inaelezewa kwa njia ya kuhuzunisha na Agbamila na Abdulganiyu (2014) kuwa viongozi wa makanisa wanaendelea kuendesha magari makubwa, kumiliki majumba ya kifahari nchini na hata nchi za nje huku wafuasi wakiishi kwa umaskini uliokithiri. Licha ya kuwa na makanisa makubwa yaliyojengwa kwa kutumia fedha zao, wafuasi wanaendelea kuishi maisha ya uchochole huku viongozi wakimiliki mali ya mamilioni. Agbamila na Abdulganiyu (2014) walikuwa wanatafitia hali ya makanisa katika nchi ya Nigeria, lakini tunaona hali hiyo hiyo ikiwiana na yanayoendelea hapa nchini.

Ogola (2014) anaelezea hali ilivyo hapa nchini akisema kuwa utajiri umekuwa changamoto nyingine ambayo inakumba makanisa hapa nchini. Hili ni dhahiri katika vipindi vya runinga ambapo wahubiri huweka nambari za simu ili wafuasi watume pesa

kupitia M-pesa kwa miradi ambayo haijulikani. Ni kana kwamba wengi wa wahubiri hasa wa makanisa ya kipentekoste huyaanzisha ili kujitajirisha. Wako tayari hata kuwahonga wafuasi wadanganye kuwa wameponywa kupitia kwa miujiza ilhali si kweli. Naye Gathogo (2011) anasema kuwa la kushangaza ni kwamba uongozi wa makanisa haya unaamini kwamba bila pesa basi hawawezi kuihubiri injili ya Yesu Kristo katika kiwango ambacho wangetaka. Kwamba suala la fedha kama kiungo cha kimsingi katika kuhubiri injili linatiliwa mkazo katika makanisa yote yawe yanaoibuka au yale ya kitambo.

Mazingira haya ndio hali halisi ambayo inashuhudiwa si tu barani Afrika bali pia hapa nchini na yanafanana na yale mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* anasimulia anaposawiri uongozi makanisani kuwa unaoongozwa na tamaa. Kutokana na tamaa, tunashuhudia mizozo kati ya kiongozi mmoja wa kanisa na kiongozi mwingine huku kila mmoja akitaka kuwa ndiye anayeongoza kanisa lake. Habwe anatueleza kuwa hawang’ang’anii waumini kwa ajili ya kuwahubiria injili lakini kila mmoja anataka kuwa ndiye anayepata pesa na zaka kutoka kwa washiriki. Kutokana na haya, kanisa linashindwa kuleta umoja na uwiano katika jamii. Badala yake, tunashuhudia utengano kanisani huku makanisa yakiibuka kila uchao. Hii ni kinyume cha maadili ya asasi hii ambayo inafaa kuimarisha upendo na umoja katika jamii. Viongozi wa makanisa ambao wanafaa kuimarisha nguzo hizi muhimu zinazoleta utangamano katika jamii ndio wanaoongoza katika kuvunja makanisa. Tunaona Joshua na Omutele wakikosana na kila mmoja akianza kanisa lake. Wameshindwa kuvumiliana na hata kusameheana kwa sababu kila mmoja anataka kuwa ndiye anayesimamia kanisa:

> Baadaye, lakini kulitokea kutoelewana baina ya Joshua na Omutele, Joshua aliona hapakuwa na haja ya kugombea jambo lolote na kijana kama Omutele. Alimwacha na akaanzisha huduma yake na karibu nusu ya wafuasi wale (uk. 31).

Mafarakano haya yanayosababishwa na tamaa ya pesa yanaingia hata katika familia ambapo baba na mtoto wanakosana kwa sababu kila moja anataka kuwa kiongozi wa kanisa. Hii ni kwa sababu anayeongoza kanisa ndiye anayepokea fedha zinazotolewa na waumini kama zaka na pia mali ya kanisa:

> Tonje gani mwanangu? Tonje alifungua kanisa lake mwenyewe. Yeye na babake hawaonani uso kwa uso. Kila mmoja yuko na mambo yake. Zuhra alieleza. Wanagombea washirika na zaka. Pesa zimekuwa uti wa mgongo wa Injili hapa Mombasa (uk. 45).

Hendriks (2007) anasikitikia hali hii na kusema kwamba inaonekana mojawapo ya biashara zinazokua kwa kasi barani Afrika ni ujenzi wa kanisa inayomilikwa na mtu binafsi kwa mfano wa makanisa kule marekani yalio na haiba kubwa na yanayosizitiza "afya na utajiri" ambayo yanatawala vipindi vya televisheni. Mifano hii imeigwa na wengi wakubwa kwa wadogo barani Afrika. Anasema ingawa aina hii ya kanisa ndio hali halisia kijamii, kitheolojia inasikitisha.

Kutokana na tamaa hii, viongozi wa kanisa hawana kule kujitolea katika kuibadilisha jamii kupitia kwa dini. Badala yake, wamekuwa kama debe ambazo zinapiga kelele tu kwa sababu nia yao sio kuwakoleza watu katika imani lakini wanaangalia ni nini wanachoweza kupata kutoka kwa waumini. Kama wanavyosema Mwikamba na Ifedha (2015) hali hii imesababisha kukuwa kwa uongozi mbaya makanisani ambapo wahubiri huanzisha makansia sio kuokoa roho za waumini bali kujifaidi kutoka kwa jasho la wafuasi. Kwa hivyo, ni wazi kwamba viongozi hawa, sawa na wale wa kisiasa, wanawatumia wafuasi kifedha. Habwe anatuambia kuwa huduma kwa waumini imekuwa ni kazi ambapo wale viongozi wanapata mshahara wa mwisho wa mwezi. Hili ndilo linachangia pakubwa utengano kanisani huku kila mhubiri akiangalia pesa anazoweza kupata kanisani.

> Joshua kama Eli wa kale alikuwa hajasikia sauti ya Bwana kwa muda mrefu. Uaskofu uligeuka na kuwa sio huduma tena kwa Bwana lakini kazi. Kazi ya mshahara mwisho wa mwezi. Japo

> alisimama akihubiri, waumini wake na hata yeye mwenyewe alijua ni debe shinda ambalo hupiga kelele tu (uk. 67).

### 4.3.1 Uongozi wa Kanisa na Siasa

Habwe anasema kwamba kanisa pia halijaachwa nyuma katika ulingo wa kisiasa. Kwa kawaida, kanisa halifai kuegemea upande wowote kisiasa; hata hivyo, linapojiingiza katika siasa, ni matarajio ya wengi kwamba litaendesha kampeni za haki. Kampeni ambazo zitakuwa kielelezo kwa wanasiasa wengine kwa vile zinazingatia sheria na pia zitakazoshughulikia masuala ya wananchi na si ya kibinafsi. Lakini katika riwaya ya *Paradiso*, tunashuhudia siasa ya ubinafsi, na pia ya kutoa hongo kama tu siasa za mwanasiasa mwingine yeyote yule. Askofu Joshua anamtaka Gekonge aingie kwa siasa si kuwahudumia wanaomchagua lakini ili kanisa lipate misaada kutoka nchini na ng'ambo. Tumeona kwamba zaka na sadaka kanisani ni mali ya kiongozi anayesimamia kanisa, kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa kuwa hata misaada ambayo askofu Joshua anayotarajia kanisa litapata iwapo Gekonge atachaguliwa itaishia kuwa yake na familia yake. Tunahushudia waumini wakihongwa kwa kupewa pesa ili wampigie kura Gekonge. Pia kuna matumizi mabaya ya rasilmali za kanisa kwani magari ya kanisa yanatumiwa katika kampeni:

> Kampeni za kisiasa zilipita miezi kadhaa iliyopita, New Jerusalem walikuwa na mgombeaji wao. Joshua alidai kuwa haikuwa vyema kutazama mambo tu. Kanisa lilikuwa na jukumu maalum la kutekeleza. Aliyekuwa shemazi wao pale, Gekonge aligombea kiti cha ubunge pale jimbo la Lang'ata. Waumini wakahimizwa wampigie kura kwa wingi. Maana kama angeingia bunge angesaidia kanisa kwa misaada kutoka nchini na ng'ambo. Waumini wangekosaje kumuunga mkono baada ya pesa walizoruzukiwa pale kanisani wakati wa kampeni. Joshua alikuwa ni mmoja katika wasaidizi hata akawa anamwombea kura pale New Jerusalem. Moyo wa New Jerusalem wa kusaidiana ulikuwepo pia. Alipewa magari mawili ya pale kanisani yakasaidia katika mikutano ya hadhara (uk. 121).

Kanisa pia linaunga mkono chama cha kisiasa na hata kuwaruhusu wanasiasa kutoa hotuba kanisani kwani hatimaye wanawapa pesa. Suala hili limezua mjadala mkali

nchini kutokana na mamilioni ya fedha ambazo zinatolewa na wanasiasa kanisani kama harambee na ambazo zinakisiwa huenda zinatokana na ufisadi. Akiandikia gazeti la *The Elephant*, Kahura (2018) anasema kuwa makanisa yamepokea takriban sh. milioni 60 kutoka kwa mwanasiasa mkuu serikalini huku kanisa Katoliki likipokea sh. milioni 14 ambayo ni asilimia 23 ya michango hiyo. Hili linaonyesha kuwa kando na makanisa ya kipentekoste hata makanisa makubwa makubwa hayajawachwa nyuma. Makala haya yanaendelea kusema kuwa makasisi na wachungaji wanatawaliwa na kutumiwa na wanasiasa kwa sababu ya ulafi, kuegemea pande moja na ukosefu wa maadili. Kwa hivyo ni vigumu kwao kuzungumzia ufisadi kwani wao pia wanafaidika. Hili linaiweka dini katika nafasi ambapo wanasiasa wanapozozana, hamna atakayewasikiliza viongozi wake kwa sababu tayari wameshajihusisha na upande mmoja wa siasa na pia uendeshaji wao wa siasa hauna haki.

Kwa hivyo, kama tunavyoona, kanisa imekuwa mahala pa kufanyia siasa huku viongozi wakifurahia na kuwapokea wanasiasa kwa vile wanatoa pesa. Pia riwaya hii ya *Paradiso* inatupatia taswira ya dini ambayo haina mtazamo mbadala katika kuzitatua changamoto zinazoikumba jamii. Tunaambiwa kuwa wakati upepo wa vyama vingi vya kisiasa ulipovuma, kila mtu aliona hili ndilo litakuwa suluhisho kwa changamoto za nchi. Tunaona kanisa pia likichotwa na wimbi hili na hata kujitosa mara moja katika ulingo wa kisiasa kwa kupigia debe chama cha kisiasa. Hatuisikii sauti ya kanisa ikitoa mchango wake kwa kutoa suluhu mbadala ya changamoto zilizomo katika jamii lakini tunaona viongozi ambao wanaangazia manufaa watakayopata kutoka kwa wanasiasa:

> Mchakamchaka wa vyama vingi ulivuma nchini. Vyama vya Ford Asili na Ford Kenya vilisajiliwa. Wanasiasa, ndugu, mtu na mwanawe, rafiki waligawana. Kila mtu aliingia mtumbwi wake. Nairobi iliterema kwa uhuru wa vyama vingi. Magazeti yaliandika kusifia hatua hiyo iliyofikiwa. Ungefikiria matatizo chungu nzima yaliyotukereketa yatatatuliwa kwa vyama vya upinzani. Magazeti, vitabu, idhaa za kutangazia sasa vilisema kwa vinywa vipana. Kanisa

> la New Jerusalem liliunga mkono chama cha FORD Kenya. Viongozi walifika hapo kanisani wakatoa hotuba na wakaombewa na kuhimizwa kupiga mbio bila kusita. Viongozi walipiga magoti kwenye madhabahu wakatiwa mkono na watukufu wa bwana. Kama ilivyokuwa desturi walichanga pesa kwa miradi ya kanisa ya New Jerusalem (uk. 130).

Haya ni tofauti na yaliyojiri miaka ya tisini ambapo sauti ya kanisa ilisikika na kuchangia pakubwa katika kuleta mabadiliko ya kisiasa nchini. Parsitau (2011), akitafitia mchango wa viongozi wa kidini katika uongozi wa marais tofauti nchini, anataja mchango wa viongozi mbali mbali wa makanisa tofauti tofauti k.v. Henry Okullu, Timothy Njoya, David Gitari, muungano wa makanisa wa NCCK na kanisa katoliki katika kupigana na uongozi wa chama kimoja. Anasema kuwa kwa pamoja na kupitia mahubiri yao, walipinga uongozi dhalimu wa chama kimoja cha KANU na hivyo basi kufanikisha mabadiliko ya kisiasa. Hata hivyo anasema kuwa mwongo mmoja baadaye, haya yamebadilika na kwamba kanisa limepoteza sauti yake ya kinabii.

Linaloonekana ni kwamba hamna tofauti kati ya wanasiasa wa kawaida na wale wanaotoka kanisani. Nia yao ni moja - kujinufaisha na kupata mamlaka kupitia njia zozote zile. Tunaona asasi ambayo kando na kujihusisha na siasa, haiendeshi siasa hizo kwa njia ya haki na kwa njia ambayo inaweza kuimarisha asasi hiyo. Badala yake, dini inajiingiza katika siasa kutokana na manufaa itakayopata.

Parsitau (2011) anaendelea kusema kwamba hali hii imedorora hivi kwamba nchi hii ilipotumbukia katika ghasia za kisiasa za 2007/08, ambapo wengi walipoteza maisha na mali yao, kanisa lililaumiwa kwa kuegemea kabila na hata pande moja ya kisiasa. Labda kando na siasa, yanayoendelea makanisani pia huenda yakachangia hali hii ya mizozo. Kila uchao, wananchi wanashuhudia mizozo kanisani kati ya makundi tofauti ndani ya kanisa moja kama riwaya hii inavyotueleza:

> Kila uchao uhusiano baina ya Michael na Joshua uliendelea kutumbukia nyongo. Ni kama majogoo wawili yaliyokaa katika kizimba kimoja. Kila mmoja katika jogoo hao alitaka utawala. Mivutano hapo awali ilikuwa batini. Baadaye mivutano hiyo ilikuwa wazi. Kanisa la New Jerusalem liligawanyika katika makundi mawili hatimaye. Kundi moja lilimwunga mkono Joshua na lingine likamuunga mkono Michael. Kila jumapili vidoko, uvumi, udhabidhabina vilitawala. Kilele ilikuwa Jumapili ya Januari moja tarehe mosi. Makundi haya yalianza kupigana. Vitu, mbao, mawe, vilitumiwa kama silaha. Wanawake walipigana na wenzao wa kundi tofauti….Polisi walifika wakazima fujo na kutenganisha vikundi (uk. 77).

Kutokana na mivutano baina ya viongozi makanisani, tunaona kwamba inakuwa vigumu kwa viongozi hawa kudumisha umoja miongoni mwa waumini. Kutokana na tamaa, hawajali kinachotendeka mradi tu yule kiongozi amebaki mamlakani. Hili linawashangaza hata polisi ambao wanaouliza:

> "Nyinyi mnaabudu Mungu gani? Sasa mnapigania nini?" Polisi mmoja mwenye sijida kipajini alimwuliza mama mmoja aliyekuwa amevunjwa mkono kwa jiwe na kuketi chini huku huo mkono kaushikilia. Kanisa la New Jerusalem lilifungwa kwa miezi minne wakingojea uamuzi wa mahakama kuhusu nani aliyemiliki nini. Baada ya vita hivi "Ndugu na ndugu waliosalimiana kwa 'Bwana asifiwe' kila siku ndio hao hao wasiopikika katika chungu kimoja. "Kisa na maana nini? Michael aliwaza. Ushindani. Ulafi wa vitu vya dunia hii. Tamaa ambayo Bwana Yesu alisema tusiwe nayo (uk. 77).

Suala linaloibuka ni ikiwa ndugu na ndugu wanapigana makanisani, kunapotokea ghasia baina ya wananchi na kusababisha mafarakano ya kijamii, ni nani watakaoleta uwiano wa kijamii kama yayo hayo ndiyo yanayoshuhudiwa kanisani? Hii ni hali ya kusikitisha ikizingatiwa kwamba ghasia za kisiasa huzuka mara kwa mara katika mataifa mbali mbali na kwa hivyo ni muhimu kuwa na angalau viongozi watakaotegemewa kuzima joto la kisiasa linapopanda. Kutokana na yanayosimuliwa na Habwe, tunaona kwamba ni vigumu kuwategemea viongozi wa kidini kusuluhisha mizozo kwani hata wao wenyewe ni chanzo cha mizozo katika makanisa wanayoyaongoza.

### 4.3.2 Unafiki Kanisani

Katika kuangalia suala la mamlaka katika matini, wananadharia wa uhistoria mpya huangazia jinsi wananchi wa kawaida (hasa wale waliotengwa) wanavyosawiriwa wanapokabiliana na matukio makuu (Hickling, 2018). Katika riwaya hii, mwandishi ametupa taswira ya wananchi wanaoishi katika mazingara duni katika kitongoji duni cha Kibera. Wakazi hawa wanaishi kwa vibanda huku kukiwa kumejaa fujo. Ni katika mazingara haya ambapo wahubiri Joshua na Michael walianzisha kanisa lao. Parsitau (2011) anatuambia kwamba mojawapo ya sifa bainifu ya makanisa ya kipentekoste yanayoundwa kila uchao tofauti na yale ya hapo awali ni kwamba hupata wengi wa wafuasi wao kutoka kwa maeneo yalio na idadi kubwa ya watu na hasa katika vitongoji duni vilivyo katika miji mikuu nchini kama vile Nairobi, Nakuru, Eldoret, Nyeri na Kisumu. Anaendelea kusema kwamba kuna sababu kadhaa za kidini na kijamii ambazo zimechangia kuibuka kwa makanisa haya zikiwemo kuzuka kwa viongozi wasomi wa ki-injilisti kutoka vyuo vikuu na pia ukuaji wa kasi wa miji na kuporomoka kwa chumi za nchi mbali mbali barani Afrika.

Naye Kagema (2014) anaendeleza wazo hili akisema kwamba Kenya ni nchi inayokua na hivyo basi baadhi ya wananchi wake wanaishi maisha ya umaskini huku wakikabiliwa na changamoto za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Changamoto hizi zinamaanisha kwamba hawapati mahitaji ya kimsingi k.v. maji safi, chakula, elimu, huduma za kijamii, mavazi na hata makazi. Katika hali kama hizi, watu hutafuta kikundi chochote ambacho kitawapa mahitaji haya au hata kuwapa matumaini maishani. Kwa hivyo, watu katika hali hii hujipata wanakumbatia kikundi chochote kiwe cha kijamii, kidini, kiuchumi na kisiasa ambacho kitawapa matumaini. Hali hii ngumu kijamii na kiuchumi hutoa mazingira mwafaka ya kukua kwa makanisa haya.

Haya ndio tunayapata katika riwaya ya *Paradiso*. Katika riwaya hii, mwandishi anatuchorea mandhari ya kanisa ambalo limeanzishwa katika vitongoji duni vya Kibera ambapo wananchi wanaishi katika hali ya uchochole. Hata hivyo, baada ya viongozi wa kanisa hili kupata pesa ambazo zimetoka kwa waumini, wengi ambao wanaishi katika kitongoji hicho, wanahamia mitaa ya kifahari. Tunaona kwamba viongozi wa makanisa wanatumia hali ya ukosefu wa matumaini miongoni mwa wakazi wa Kibera sio kuwasaidia kutoka katika hali ile bali kuwahadaa kupata ile fedha kidogo wanayo na baadaye kuwaacha katika hali hiyo hiyo na kuhama.

> Katika kundi hili ni Michael pekee aliyekaa Kibera bado. Joshua alikaa mtaa wa Woodley. Alisema kwa kuwa Mungu alikuwa kambariki na gari la *Toyota* aliona ahamie mahali pa salama pa kuliweka hilo gari. Wanawe wawili wa kike walikuwa wanasomea Chuo Kikuu cha Daystar kwa hivyo aliona asiwadhiki sana kwa kukaa Kibera. Nyumba yake Joshua ni ya kisasa si kama kibanda alichokaa hapo Kibera. Japo hapo Kibera kibanda hicho kilionekana kama kizuri lakini hakikumstahili hasa alipopandishwa cheo na kuwa Askofu mkuu. Musa naye alikaa Buruburu. Pia yeye aliona Mungu alikuwa amejibu maombi yake kwa kumpa nyumba. Alishukuru. Musa alisema kuwa ilikuwa vizuri kukaa mahali pa usalama. Kibera kulikuwa na fujo, ilikuwa vigumu kulea watoto kwa heshima na adabu (uk. 43).

Joshua na Musa wamekuwa wakiishi Kibera mahali ambapo walianzisha kanisa lao na hata kuwalelea wanawao pale lakini kwa vile wamepata mali, wanahama kwa sababu ni mahali pa fujo. Hii ni kinaya kwa vile wao kama wahubiri wanafaa kuirekebisha hali hii na kuona kwamba kuna tabia bora katika jamii lakini badala yake wanayakwepa majukumu yao kwa vile nia yao ni kujinufaisha na wala sio kuwahudumia kiroho wakazi wa Kibera. Pia wanaendelea kudumisha makanisa yao katika eneo hilo hilo huku wakiendelea kujitajirisha kutokana na jasho la wanakibera. Riwaya hii inatuonyesha kwamba wahubiri hawa hawana nia ya kuimarisha hali ya wakazi hawa wa Kibera kutokana na hali yao duni. Kwao, wangependa hali ile ibaki vile vile ili

waendelee kufaidika. Mwandishi anauliza swali kuu kupitia kwa Michael ambaye pia ni mhubiri na aliyebaki wengine wakihama Kibera:

> Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa chake. Itakuwaje tunajitafutia starehe kubwa kubwa katika dunia? (uk. 43).

Kama wafuasi wa Mwana wa Adamu, wanafaa kufuata mfano wake na kuishi maisha ya kawaida, na kuendelea kuishi miongoni mwa wanaowahudumia badala ya kujitafutia makuu.

Tunaona viongozi wa makanisa ambao wanachukua mali yote ya kanisa na kuwa yao. Michael anapewa gari na Amuko baada ya kumwombea. Michael analitoa gari hilo kwa kanisa lakini Askofu Joshua akalichukua.

> Punde si punde aliliegesha kwake nyumbani. Gari likabadilika likawa si la kanisa bali lake la kibinafsi. Mkewe Joshua alikuwa akitembelea gari hilo hali Joshua akawa anatembelea lile jipya la Toyota, kapu nzima la zaka, sadaka, fungu la kumi na matoleo mengine alilivuna Joshua. Musa ndiye aliyeshirikiana naye kujua yatatumiwa vipi (uk. 48).

Kando na kuchukua mali ya kanisa, viongozi hawa wanajaza nafasi zilizobaki wazi kanisani na jamaa wao wa karibu labda kuhakikisha kuwa wanaendelea kuidhibiti ile mali ya kanisa. Baada ya kanisa la New Jerusalem kuvunjika na Joshua na Michael kutengana, Lona mkewe Joshua ndiye aliyechukua mahali pa Michael. Pia pengo lililoachwa na Musa linajazwa na Nyamongo aliyekuwa pia na uhusiano na Joshua. Katika kumteua Nyamongo, Joshua anamtaka mtu ambaye hatampinga badala ya kuzingatia uwezo wake wa kuhubiri.

> Lona sasa ndiye aliyepachikwa mahali pa Michael. Alikuwa mmojawapo katika makasisi wa New Jerusalem mbali na Nyamongo aliyepachikwa mahali pa Musa. Nyamongo alikuwa mhubiri. Kwanza alikuwa mpevu wa umri. Hakuwa kijana atayezulia watu zogo lisiloeleweka. Pia, alikuwa mtoto wa mbiomba wake Bosire. Joshua hakutarajia ubishi wowote kutoka kwake. Sasa Lona alipopewa cheo hicho cha ukasisi Joshua aliona kakamilika (uk. 79).

Kutokana na ulafi kanisani, tunaona kuwa suala la fedha badala ya lile la imani linatiliwa mkazo zaidi kanisani. Wahubiri wanaitisha pesa zaidi pasi na kujali hali ya kiuchumi ya wafuasi wao. Agbamila na Abdulganiyu (2014) wanasema kuwa kanuni na mahubiri yanayoshikiliwa na viongozi wa kidini ni tafsili ya kitabu kikatatifu yanayosema; *Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.* Anaendelea kusema kuwa kifungu kingine kinachotiliwa mkazo ni kile cha Malachi 3:10. *Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la.* Mnamo Agosti 16, 2016 nchi hii kupitia kwa kipindi cha Makri ya Injili katika runinga ya KTN ilishuhudia jinsi mhubiri mmoja Peter Kanyari wa kanisa la Salvation Healing Ministry alivyotumia kifungu hiki kuwahadaa wafuasi kutoa sh.310 ili wapate miujiza.

Wahubiri tayari wamehama mtaa wa Kibera baada ya kupata fedha kutoka kwa waumini lakini badala ya kuwasaidia waweze kuinua hali yao ya maisha, wanaendelea kuwanyanyasa kwa kuwaitisha fedha zaidi ili waendelee kugharamia maisha yao yaliyojaa ubadhirifu:

> Tangazo jingine ndugu na dada zangu katika Yesu ni kwamba matoleo yenu yamepungua, si zaka si fungu la kumi. Kitabu cha Malaki kinasema matoleo ni lazima kwa muumini. Matoleo haya yapaswa kuwa mazuri. Baadhi yenu mnaleta kanisani masazo ya *supermarket*, yaani *change*. Hamleti zaka za kutukuza Bwana. Si ruhusa kuleta shilingi moja kanisani au hata shilingi kumi, kwani pesa hizo zitanunua nini? Lazima mnapoleta zaka mjiulize inaweza kununua nini. Kanisa lina miradi mingi kama vile kununua vyombo vya muziki na ni haramu kucheza muziki katika vyombo hivyo ikiwa hukuchangia. Kuanzia jumapili ijayo, vifuko vya sadaka vitakuwa kule mbele na kila mmoja atapaswa kupeleka zaka yake kila mtu akimwona. Maana kuna watu huja jumapili mbili hapa wasitoe zaka (uk. 54).

Tunaona viongozi ambao wamepofushwa na tamaa yao ya fedha hivi kwamba hawaoni hali ya wafuasi wao. Ni wazi kwamba wengi wao wanahitaji msaada kutoka kwa kanisa na si wao kuutoa. Wahubiri wanaojali maslahi ya wafuasi wao wangetumia fedha wanazopata kuwapa uwezo kiuchumi wale wafuasi badala ya kuwaitisha fedha. Agbamila na Abdulganiyu (2014) wanasema kuwa viongozi wa dini hawahubiri au kuwafunza wafuasi mbinu za kukuza utajiri au kuwekeza ili waweze kujikwamua katika hali yao. Badala yake, wanatumia injili kuendelea kuwaibia wafuasi. Hili ni sawa na jinsi wanasiasa wanatumia nafasi waliopewa kuendelea kuiba mali ya umma. Ndio maana wale waumini wanalalamika kwani inaonekana kuwa viongozi hawataki kuelewa hali yao.

> "Ametuchosha huyu bwana na habari za zaka. Kila siku zaka. Asiyejua habari za zaka ni nani?" Alisema mzee mmoja pale.
>
> "Kwa nini unasema hivyo?" Mama fulani alimwuliza.
>
> "Hajui kuna wengine hawana pa kutoa hiyo zaka. Hata kula hawawezi kula. Tena hizo pesa wanazila wao. Ndio sababu." Mzee alijibu (uk. 54).

Wahubiri wanaishi maisha ya raha na hata mali inayosalia wanaitumia kuwawekezea wanao. Kwa sababu ya ulafi unaoshuhudiwa katika makanisa, wanazidi kuwaitisha wafuasi zaka bila kujali kwamba kuna wale hata chakula hawana. Licha ya kuwa wafuasi wanajitahidi kutoa, tunaona kuwa kuna malalamishi ya wafuasi kwani wanaitishwa kila uchao ilhali hata hawapati faida yoyote kutoka kwa makanisa yale. Kutokana na yanayojiri katika riwaya hii, mwandishi anatuambia kwamba wafuasi wametengwa kwani nafasi za kanisa zinawaendea wafuasi, fedha vivyo hivyo huku wao wakitakiwa tu kutoa kila uchao. Haya ni sawa na wanayotuambia Mwikamba na Ifedha (khj) kuwa wafuasi wengi wangependa wahubiri wao kuishi maisha mazuri. Hata hivyo wanachoshwa na jinsi wanavyoitishwa kila mara. Sawa na viongozi wa kisiasa, viongozi wa kidini wanaongozwa na ubinafsi ambapo wanaishi maisha ya ubadhirifu

kutoka kwa jasho la wafuasi wao wanaoendelea kuishi maisha ya umaskini. Na kwa hivyo, viongozi hawa hawawezi kuwawekemea wala kuuona uovu unaotendwa na wanasiasa kwani yayo hayo ndio wanayoyatenda.

## 4.4 Uozo Kanisani

### 4.4.1 Kuabudu Pesa

Kwa kuzingatia riwaya ya *Paradiso* tutaangazia hali ilivyo katika makanisa kwani kando na kuwa watetezi wa wanyonge viongozi wa kanisa wana jukumu la kudumisha maadili katika jamii. Nath (2015) anaorodhesha vipengele kadhaa kuhusu umuhimu wa dini katika jamii. Mawazo yake mtaalam huyu yatatuongoza katika kutalii yale yanayoendelea katika asasi ya dini. Jambo hili ni muhimu kwani ni kutokana na maadili ambapo kunaweza kuwa na haki za kijamii. Nath anasema kwamba dini hufunza maadili ya kijamii k.v ukweli, upendo na nidhamu. Mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* ameyaangazia haya na kutoa rai yake kuwa upendo, kusamehe, kuwajali wengine na kujitolea ni mambo ambayo hayapatikani kanisani. Badala yake, tunashuhudia utengano unaosababishwa na kutovumiliana na pia kukosa kusameheana. Kuna ubinafsi, uzinzi, kujitakia makuu yote haya yanayokinzana na imani ya kikristo. Habwe anatupa taswira ya makanisa ambayo nje ni kanisa lakini ndani yamejaa uozo na kuwafananisha na Mafarisayo walioshtumiwa na Yesu:

> Yesu aliwashtumu Mafarisayo kwa ajili ya unafiki. Mafarisayo walizoea kushtumu watu hali yale wanayoyapinga ndiyo wayafanyayo. Mafarisayo wale wale ndio walioshughulika kuwaleta watu kwa Mungu na ndio pia waliowatoa. Mafarisayo walijenga imani yao katika dini wala siyo imani na Yesu. Ndugu zangu, Bwana wetu Yesu aliwashtumu Mafarisayo kwa kuwaambia walikuwa na tabia kama watu walioosha vikombe kwa juu kumbe ndani vimeoza (uk. 55).

Tunaambiwa kuwa hawa viongozi wanafaa kuwa kielelezo kwa kutenda wanachohubiri. Lakini wanatenda kinyume na haya kwani wanawanyang’anya maskini badala ya

kuwasaidia na pia hawajali hali ya wanyonge. Katika riwaya hii, hatuoni viongozi wa kanisa wakichukua hatua yoyote kuyainua maisha ya wafuasi wao. Tunaona viongozi ambao badala ya kuwachunga, ndio wanaowala kondoo. Wanaishi maisha ya ubadhirifu mkubwa kutokana na jasho la wanyonge badala ya kuwasaidia walio maskini kama ambavyo imani ya kikristu inavyosema. Injili ya fedha imeshamiri kanisani hivi kwamba yanayopewa kipaombele katika dini ni fedha wala si imani. Pia kutokana na vitendo vyao, wanaishia kuwafukuza watu kanisani badala ya kuwavutia kujiunga na kanisa. Haya ndio yaliyomfika Mganga ambaye kupitia kwa Lona mkewe alimkaribisha Joshua kijana ambaye hakuwa na mahali pa kuishi lakini akaishia kuoana na Lona. Tangu wakati huo, Mganga aliwachukia sio tu wanawake bali pia dini na wakristo kwa sababu kwa mujibu wake aliona dini kama ulaghai na ujambazi wa aina fulani (uk. 71).

### 4.4.2 Ubaguzi

Riwaya ya *Paradiso* inatuambia kwamba yale imani ya kikristu inayoyakashifu ndiyo yayo hayo yanayotendwa. K.m askofu Musa anawahadaa waumini kwani anatenda kinyume na cheo chake cha uaskofu kwani amekuwa akishiriki uzinzi na sio tu na wake za watu bali pia watoto wa shule:

> Lililomhuzunisha Kyalo zaidi ni kuwa Musa hakuwa akimhadaa na kumchezea mkewe tu bali alicheza na wanawake karibu watano. Karibu wote ni wake za watu na mmoja ni binti ya mtu katika shule ya upili ya Alliance (uk. 59).

Huku imani ya kikristo ikisisitiza usawa, tunaona ubaguzi ukiendelezwa kanisani. Askofu Musa alichapwa na kuumizwa na Kyalo alipompata na mkewe Salome. Huku kanisa likimlipia Musa bili yake ya hospitali, hakuna anayemjali Salome ambaye pia ni mshiriki wa kanisa hilo na alilazwa hospitalini sawa na askofu. Huu ni wizi wa mali ya kanisa ikizingatiwa hali aliyopatikana:

> Musa alitoka hospitali. Bili yake ya shilingi elfu mia nne ililipwa na kanisa. Baadhi ya washiriki wa kanisa hilo walilalamika lakini wangefanyaje? (uk. 60).

Imani ya kikristu sio ya mtu binafsi bali ya kila mtu anayeiamini. Lakini linaloshuhudiwa makanisani ni ule ubinafsishaji wa dini ambapo kiongozi binafsi anataka kumiliki kanisa. Mwandishi anatuambia kwamba uongozi wa kanisa umejikita katika watu wachache ambao wana uhusiano na viongozi walioko mamlakani. Kwa vile wanachukulia kanisa kuwa mali yao, wao ndio huamua nani atakuwa mhubiri huku wakimiliki mali yote ya kanisa.

### 4.4.3 Uzinzi

Nath (2015) anazungumzia umuhimu wa dini katika kudhibiti tabia ya mtu binafsi. Riwaya ya *Paradiso* inatueleza kwamba uzinzi miongoni mwa viongozi wa kanisa ni jambo la kawaida. Hii ni licha ya kuwa hao ndio wanafaa kuwarekebisha wanajamii kutokana na maovu kama haya. Joshua alizini na Lona aliyekuwa mkewe Mganga, Musa na Salome na pia Michael anajipata katika mtego huo huo anapozini na Patricia ambaye ni rafiki yake mkewe Lydia. Vitendo hivi vya viongozi wa kanisa vinawafanya wengine kuichukia badala ya kuwavutia kujiunga nalo.

> Joshua alikaa kwa takriban miaka kumi na mama Lona. Joshua alipenda kumuita Dada tu kwa ambavyo waliswali pamoja. Baadaye Lona na Mganga walianza kudhaniana. Kila mmoja akawa hamwamini mwenzake. Japo kulikuja mamake Lona kuwasuluhisha haikuwezekana. Walitengana. Kumbe kwa miaka hiyo yote kumi Lona alokaa na Joshua, Joshua alikuwa mume mwenza wa Mganga (uk. 34).

Kutokana na kuhadaiwa na mkewe Lona na askofu Joshua, Mganga anajazwa na chuki moyoni mwake kwa wanawake na pia kwa dini. Na kwa hivyo tunaona vitendo vya waumini hawa vinawafukuza wengi kanisani na hata kuvunja asasi muhimu ya kijamii, ile ya familia. Tunaambiwa viongozi hawa hawajali wanalolifanya mradi tu hakuna

aliyewaona. Na kwa hivyo wanaendelea na kazi yao ya uhubiri licha ya matendo yao maovu wanayotenda.

> Michael hasumbuliwi tena na nadhiri yake kama usiku wa kwanza. Michael aliota ameanguka katika mkondo wa maji na hakuwa na mombezi. Lakini mazoea sasa yalimfanya kutojali. Michael sasa kama baba yake alikuwa na dunia mbili, dunia ya imani kwa Bwana na miujiza na dunia ya mapenzi na Patricia (uk. 152).

> Michael kulala kwa Patricia halikuwa jambo kubwa kwake. Maadam hakuonekana alifika kanisani na kuongoza ibada (uk. 160).

Maovu yanayofaa kukashifiwa kanisani kama vile kuzini yamekuwa ni kawaida kwa viongozi wa kanisa. Hawa viongozi ndio wanaofaa kuwa kielelezo kwa wafuasi na hata kwa wasioamini lakini vitendo vyao vinawafukuza hata wale wanaoamini kanisani.

Jambo lingine analolizungumzia Nath (2015) ni umuhimu wa dini katika kudumisha nidhamu. Lona ni mke wa askofu; isitoshe, yeye pia ni kasisi mwandamizi katika kanisa la New Jerusalem na pia ana umri uliokomaa. Kwa hivyo, anafaa kuwa na heshima yake kwa jinsi anavyovaa na hata anavyozungumza. Hata hivyo, mwandishi anatupatia picha ya kasisi na mama ambaye anavaa nguo ambazo ni za aibu na pia aliyejaa matusi badala ya baraka kinywani mwake:

> Michael alisema, akitazama skati ndefu ya huyu mama iliyopasuliwa kuwili hadi mapajani, kiasi cha kwamba imletee hizaya. Michael alishangaa ni kwa nini mama huyu alivaa hivyo katika umri wake wa miaka sitini. Isitoshe, atavaaje hivyo akija kumwona? (uk. 69).

Pia tunamwona Lona akitumia lugha ya matusi, ni kasisi ambaye hana Subira: "Mara wimbo wa Shari Martin ulikatika dereva fulani alipotokea kwenye Kibera Drive na kuingia barabarani. Lona akasema, Mbwa wa mkia, shenzi kabisa, *Acheni, acheni kuwabatiza wakiwa*…..Jinga. anasimama bila kuashiria" (uk. 136).

Viongozi wa kanisa wanafaa kuonyesha heshima wakiwa kanisani na hata nje. Hata hivyo, tunaona viongozi ambao hata mavazi yao ni ya aibu. Hivyo basi inakuwa vigumu kwa kiongozi kama huyu ambaye hana nidhamu kuweza kusisitiza nidhamu kwa anaowaongoza.

Nath (2015) anaendelea kusema kwamba dini huimarisha maadili miongoni mwa watu na kwa hivyo huleta utangamano wa kijamii. Utangamano huu lazima uanze kwa familia kwani hii ndio nguzo ya jamii. Callan (2014) anasema kuwa familia ni muhimu kwa utangamano wa jamii, malezi ya watoto na hata ustawi wao kibinafsi, ni nguzo ambayo kupitia kwayo, watoto kwa watu wazima hujifunza, hufanya kazi na hata kuchangia jamii. Tunaona umuhimu wa asasi hii na hivyo basi ni muhimu kwa viongozi wa dini kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa asasi hii imesimama. Hata hivyo, Riwaya ya *Paradiso* inatupa viongozi wa dini ambao kando na kushindwa kudhibiti familia zao, pia wanaharibu familia zingine na hivyo basi kuchangia katika kuyumbisha jamii. Askofu Joshua ameshindwa kuidhibiti familia yake. Alimpenda mwanawe kiasi cha kumtendekeza na hili linamfanya Nice kuwa mtoto ambaye hana maadili. Huku mwanawe Nice akiwa na tabia mbaya, Joshua hafanyi juhudi za kumrekebisha na badala ya kukabiliana na tabia hiyo anataka amwoze kwa Michael:

> "Lazima tukutafutie mwanangu kwa sababu tabia yako ni mbovu. Hatutaki utangatange kama mwehu. Mara utaenda na wazungu, mara waafrika, mara wahindi. Mimi ni mhubiri sitaki kuchafuliwa jina" Joshua alisema (uk. 73).

Joshua ana haja zaidi na watakavyofikiria watu badala ya kumshauri mwanawe. Pia huyu ni yule yule Joshua ambaye aliuhama mtaa wa Kibera kwa vile hakutaka wanawe wakulie katika mazingira yasiyokuwa na nidhamu. Joshua anakuja kujuta baada ya mwanawe kupotea kwani anaona kuwa yeye pamoja na mkewe walichangia hali hiyo kwa kutokuwa mfano mwema nyumbani.

> Kwa kweli vitendo vya mzazi huwa mfano mwema kwa wana. Yeye Joshua hakuwa mwaminifu. Wala Lona hakuwa mwaminifu. Uaminifu wao ulikuwa midomoni tu (uk. 129).

Hili linaendelea hata katika ndoa ambapo tunaona wahubiri wanaoishi katika ndoa ambazo zimevunjika au zinazoshuhudia misukosuko. Lona na Joshua walioana baada ya kuishi katika maisha ya uzinzi huku Lona akizini na Joshua akiwa bado katika ndoa

yake na Mganga. Baadaye, ndoa ya Lona na Joshua inakumbwa na misukosuko baada ya mwanawe Nice kumwambia kuwa yeye si babake. Lona anatafuta ushauri kutoka kwa waganga. Michael naye anazini na Patricia huku Askofu Musa akizini sio tu na Salome bali na wanawake wengine wakiwemo wanafunzi wa shule.

> Michael leo alihisi kitu kwa ndani. Aliona katika hali yake ile hakufaa kushauri kuhusu matatizo kama yale. Angefanyaje na ile ni kazi yake? Ilibidi ashauri hivyo hivyo. Mume alikuwa akisema mke wake amekuwa mkali hata hafurahii kwenda nyumbani tena. Michael akamweleza mke kuwa ni vyema kuwa mnyenyekevu kwa Ibrahimu. Kila wakati Michael alipokuwa akiwazia nyumba ya Ngugi na Ruth alihisi kama ni kinaya kwake (uk. 163).

Kuhubiri si tu maneno bali pia ni vitendo. Katika riwaya hii, Habwe anatuonyesha kuwa viongozi hawa si kielelezo chema katika jamii kwa kuzingatia vitendo vyao hasa katika ndoa. Tunaona wahubiri wanachangia kuzorota kwa asasi hii. Hata hivyo, mwandishi anatuambia kuwa hao viongozi ndio wafuasi wao wanawaendea kuwataka ushauri ndoa zao zinapokumbwa na matatizo. Na kwa hivyo hata ushauri wanaotoa si wa dhati lakini wa kijuujuu tu kwani hata wao dhamiri zao zinawahukumu.

Lona ni kasisi na kiongozi wa kina mama kanisani. Hivyo basi, anafaa kuwa mstari wa mbele katika kuidumisha imani ya kikristo. Kutokana na wadhfa wake katika kanisa, tungemwona akiiombea ndoa yake ilipokumbwa na misukosuko na hata kujaribu kuirudisha katika hali yake ya kawaida. Lakini baada ya kukosana na mumewe, Lona anapata nafasi ya kwenda kwa mganga ili aweze kumdhibiti mumewe. Hatumwoni mama ambaye ananyenyekea kwa mumewe; badala yake anataka kumdhibiti mumewe. Anamwendea rafiki yake Adema ambaye pia ni kiongozi wa kina mama katika kanisa la African Divine Church (ADC). Adema anampeleka kwa mganga kwa jina Angelina ambaye anampa dawa itakayompumbaza mumewe. Yeye pia ameshampumbaza mumewe na anamsaidia Lona kufanya vivyo hivyo na wanapofaulu;

> Walicheka. Wakajiona washindi. Walishukuru Mungu kwa yote (uk. 114).

Ni kinaya kwamba wanamshukuru Mungu kwa kufanikiwa kufanya yaliyo kinyume naye. Tungetarajia kuona viongozi ambao wanamgeukia Mungu na kutafuta uongozi wake katika shida zao lakini hili halifanyiki. Na kwa hivyo wanahubiri tu kwa sababu ni lazima lakini hawaamini na kuzingatia wanayoyahubiri.

Mwandishi anatuambia kwamba kutenda mambo kando na maadili ya dini imekuwa ni kawaida kwa wahubiri. Ni asasi ambayo imejaa uovu. Tunaona viongozi wanaowanyanyasa na hata kuwaibia waumini. Wanawahadaa waumini kwa miujiza ya uongo wanayotumia kwa minajili ya kuongeza wafuasi ili wapate fedha zaidi. Ni viongozi ambao kwao pesa ndio kila kitu na watafanya kila wawezalo ili wazipate. Wahubiri wenyewe wanajua kwamba wanayotenda sio ya haki na ndio maana dhamiri yao inawahukumu. Ingawa ile dhamiri inawahukumu, wanaitupilia mbali kwa sababu wengi wa wahubiri wanatenda yayo hayo:

> Kwani mimi peke yangu? Ndio wenye magari bora siku hizi. Ndio wenye nyumba za bei. Ndio wanaosomesha katika skuli za ghali. Na ndio wanaojilimbikia pesa benki (uk. 163).

Tunapata mawazo kama hayo yakiendelezwa na Lona: “NI NANI ATAKAYEKAA HEMANI MWA BWANA? Biblia ilitoa maelezo. Lona alijitathmini akaona hawezi hata chembe… Haidhuru hata kama sitakwenda sitakuwa peke yangu. Lona alijipurukusha. Ni wangapi walao rushwa? ni wangapi wauao? Ni wangapi wadanganyao?” (uk. 130).

Kutokana na uovu uliojaa makanisani, viongozi wake hawajali hata wanapotenda maovu kwa sababu kila mmoja anafanya hayo. Mwandishi anasema kuwa kutenda kinyume na maadili ni jambo la kawaida kwa viongozi wa makanisa. Viongozi kama

hawa hawawezi kutegemewa kuibadilisha jamii kwani wao wenyewe wamezama katika uovu.

### 4.4.4 Biashara Haramu

Katika juhudi za viongozi kutafuta fedha, wanajihusisha na biashara ya dawa za kulevya. Boribori aliachiwa kanisa la New Jerusalem baada ya Joshua na Lona kuaga dunia na anaitumia nafasi aliyo nayo kushiriki ulanguzi wa madawa ya kulevya. Ni viongozi ambao hawatosheki kwani hata baada kupata fedha kutoka kwa waumini, bado wanatumia kanisa kushiriki katika biashara haramu ya madawa ya kulevya ili waendelee kujitajirisha. Tunaambiwa kwamba hii haikuwa mara ya kwanza kwani Boribori alirithi biashara hii kutoka kwa Joshua na Lona:

> Jingine ni kashfa ya Boribori ya almasi na mihadarati katika kanisa la New Jerusalem. Kanisa hili limehusishwa na ulanguzi wa madawa kama vile *bangi*, *heroine* na *hashish* (uk. 193).
>
> Siku moja Boribori alipokuwa ametokea safari ya Ujerumani Polisi wakafika pale New Jerusalem. Waliomba kuwasaka. Polisi walipata mihadarati ya aina ya *hashish, heroine,* bangi na mihadarati mingine. Makanisa mengi nchini yalikuwa yamehusishwa na kashfa za aina mbalmbali. Polisi waliingia katika nyumba mbalimbali kwa fosi. Walipekuapekua chumba. Jibwa lao liliwasaidia kunusa sehemu mbalimbali za chumba kilichokuwa na mwanga hafifu. Hawakupata mihadarati tu bali pia zebaki, almasi na dhahabu (uk. 199).
>
> Mihadarati kama vile *hashish* na *heroine* ilitoka Lagos: ikaletwa New Jerusalem nao walipokwenda nje katika shughuli za kikanisa kama vile maombi, semina, kongamano na kadhalika (uk. 207).

Mwandishi anawakashifu kwa kutumia madhabahu kama nyenzo ya kutafuta mali.

Kando na ulanguzi, kanisa pia linahusishwa na ulawiti na uuzaji wa binadamu. Tunaona viongozi wa kanisa ambao hawaheshimu hata maisha ya binadamu mradi tu wanapata fedha. Watu wanaoendesha biashara hii kupitia kwa makanisa haya wanaelewa kuwa watoto hao wasichana wanaenda kutumiwa kama makahaba. Kanisa linafaa kupigana na

ukahaba na pia kuwa mstari wa mbele kuwachunga watoto lakini, badala yake, kanisa hilo hilo ndilo linalochangia kuendelezwa kwa ukahaba:

> Nchi ilikumbukushwa kadhia za miezi minane iliyopita ambapo makanisa yalikuwa na kashfa ya ulawiti na kuuza wasichana wadogo kama watumwa wa mapenzi katika nchi za ng'ambo kwa kuwahadaa wanawatafutia kazi. Watu waliokuwa makanisani waliona wanaonewa. Watu waliokuwa nje ya kanisa likadumaza harakati za injili. Kanisa lililaumiwa kwa sababu ya watu. Watu hawa ndio waliokuwa mihimili ya injili lakini wakaweka tamaa ya pesa na utukufu mbele yao (uk. 207).

Badala ya kupigana na uozo ulioko katika jamii, viongozi hawa wanachangia kuendelea kuzorota kwa hali hii. Hii ndio sababu wanajihusisha na ulanguzi wa madawa ya kulevya, jambo ambalo linachangia uozo wa jamii kwani watu wanapotumia madawa haya kuna uwezekano mkubwa kuwa wataendelea kushiriki maovu kwani zinalemaza uwezo wao wa kufikiria. Ingawa wanafaa kupigania wanyonge, wanawauza wasichana wadogo wakijua wanaenda kufanya ukahaba.

### 4.4.5 Ufisadi

Licha ya kuwa mhubiri, anaposhikwa na kufikishwa mahakamani kwa kosa la ulanguzi wa madawa ya kulevya, Boribori anajaribu kumhonga jaji ili aepuke haki. Boribori hakuwa na nia ya kubadilisha mienendo yake lakini alitaka kesi itupiliwe mbali na aendelee kama kawaida na kazi yake ya uhubiri.

> Boribori alindondoka shilingi milioni moja. Aliitoa kama chai kwa jaji Moriasi (uk. 212).

> Alinuia kushinda na baadaye kuendelea kuhudumia Bwana Mungu, Boribori na *Mercedes* (uk. 213).

Riwaya ya *Paradiso* inatuambia kwamba ufisadi unaoshuhudiwa miongoni mwa wanasiasa na hata wananchi ndio ule ule unaoshuhudiwa miongoni mwa viongozi wa makanisa. Na kwa hivyo asasi hii haiwezi kamwe kupigana na uozo huu katika jamii.

## 4.5 Mchango wa Wafuasi

Mwandishi anawasawiri wafuasi kama ambao hawaendi kanisani kutafuta maadili au imani bali kutatua matatizo yao ya kibinafsi. Ni waumini ambao hawajali kinachoendelea katika asasi hii ila kila mmoja anaenda kujitafutia yatakayomfaidi yeye binafsi.

### 4.5.1 Miujiza

Katika juhudi za kuwavutia wafuasi zaidi ili fedha ziongezeke, baadhi ya wahubiri wanawavutia waumini kwa kutenda miujiza. Mwandishi anasema haikashifu miujiza.

> Lakini Michael alitaka iandamane na wanaomwamini Yesu. Yaani watu wa kweli. Siyo warongo. Siyo wezi. Siyo wabakaji. Siyo makafiri wa namna zote. La! (uk. 57).

Katika riwaya hii, Habwe anatuambia kuwa wengi wanaenda kanisani sio kumtafuta Mungu lakini kutafuta miujiza. Katika miaka ya hivi karibuni, kumezuka 'wahubiri' wengi ambao wanawatangazia waumini utendaji wa miujiza katika makanisa hayo. Hata hivyo, tunaambiwa kuwa mingi ya miujiza hii sio ya kweli lakini ni njia moja ya kuwavutia waumini ili fedha zipate kuongezeka kanisani. Mwandishi anairai jamii kutathmini suala hili la miujiza kwani mingi ni ya kuwahadaa waumini.

> Boribori anakumbuka vijana watatu waliojifanya vilema wakashuhudia kupona kumbe ni urongo. Vijana hao walifanya ili walipwe pesa. Baada ya sarakasi hiyo vijana hao walilipwa shilingi elfu moja kila mmoja. Boribori anakumbuka mkutano aliokuwa nao Kisii mjini. Watu kumi na wanane walishuhudia kupona Ukimwi. Kumbe ni porojo lao la kupanga (uk. 215).

Mwandishi anatuambia kuwa wafuasi nao pia wanachangia katika uozo unaoendelea makanisani kutokana na sababu zinazowafanya kwenda kanisani. Kama viongozi wao, nia yao pia sio kutafuta maadili kanisani lakini ni kwa sababu zao za kibinafsi. Kuna wale wanaoenda kutafuta utajiri, kuponyeshwa magonjwa na mizozo mingine.

> "Wajua siku hizi mwanangu watu watafuta kunako miujiza. Yaani mahali ambapo matatizo yao ya kiuchumi, kijamii yanaweza kutatuliwa." Zuhra alisema (uk. 52).

Mwandishi anaendelea kutuambia kuwa "maradhi, ufukara, mizozo na ukosefu wa kanisa ni baadhi ya visababu vilivyosukuma watu kanisani" (uk. 52).

Tunaambiwa kuwa ingawa wengi wanaenda kanisani ni wachache wanaotafuta yaliyo ya kweli: "Ni wachache waliokuja ili kufuata mambo ya Maulana ya kuishi na kutembea kwa haki" (uk. 81).

Katika riwaya ya *Paradiso*, tunaona waumini ambao wanatafuta miujiza na kwa hivyo hawako tayari kukabiliana na maovu yanayoendelea makanisani; wanakwepa kukabiliana nayo kwa kumlaumu shetani. Kwa kawaida, shetani ni kiumbe ambacho hakionekani na ambacho pia kina uwezo kumshinda binadamu na kwa hivyo ni vigumu kukabiliana nacho. Hivyo basi inakuwa rahisi kumlaumu kila mara kiongozi wa kanisa anapotenda uovu. Mchungaji Musa anapopatikana akizini na Salome ambaye ni mfuasi wake, waumini wanaambiwa:

> … tumesikitika na kuvamiwa na shetani aliyemshambulia Mchungaji Musa aliyekuwa amekwenda kwa huduma. Tunajua siku hizi shetani ameanza kutuvamia na tutazidi kupambana naye hadi wakati tutakaomshinda. Ningependa tuendelee kuwaombea Mchungaji Musa na dada Salome ili waweze kushinda hali zao (uk. 53).

Wafuasi pia hawatathmini vitendo vya wahubiri wao. Boribori anaposhtakiwa kwa ulanguzi, wafuasi wa kanisa lake wanajitokeza kwa wingi kumuombea ili aweze kuachiliwa huru. Hawataki kuamini kuwa kiongozi wao anaweza kuwa ametenda kosa lile.

> Wakati huo hakimu walinuia kufanya uamuzi. Boribori na waumini wake walienda katika uwanja wa Uhuru Park. Walisoma biblia na kuswali kwa muda wa saa moja (uk. 217).

Ni wazi kwamba kando na viongozi, wafuasi pia wanafaa kulaumiwa kwa yale yanayoendelea katika asasi hii kwani wao pia hawaendi kanisani kumtafuta Mungu lakini kwa sababu zao wenyewe.

### 4.6 Suluhu Lililopendekezwa

Akizungumza kuhusu majukumu ya mwandishi, Nyamndi (2006) anasema kuwa mwandishi ni mwalimu kwa kuzingatia maana asilia ya neno hili. Kwa hivyo, kama mwalimu katika jamii, mwandishi Habwe anazua masuala yanayoiathiri jamii yake lakini wakati huo huo anatoa suluhu ambazo kwake yeye anaona zitairudishia hadhi asasi hii ya dini. Hii ni sawa na wanayoyasema wananadharia wa uhistoria mpya. Mojawapo ya mawazo ya Stephen Greenblatt, ambaye ni mwanzilishi wa nadharia hii, ni kwamba kuna dunia mpya kijamii ambayo kila mara inaundwa na kuundwa upya na matini (Hickling, 2018). Katika kutoa suluhu, tunaona mwandishi anajaribu kuiunda upya jamii yake. Katika kuangazia haya tutaongozwa na mawazo ya Stuckelberger (2007) kuhusu kiongozi mwema kwa kujikita katika kitabu cha Luka 12: 35-48.

#### 4.6.1 Kiongozi Anayewajali Wengine

Stuckelberger (2007) anasema kwamba kiongozi mwema ni yule anayejali uchumi wa watu wote wanaoishi na kufanya kazi katika jamii ile. Yeye hutambua kuwa yeye si mmiliki au mwenye hisa katika kampuni ile lakini ana wajibu wa kuitunza na kuikuza kwa niaba ya mwenyewe. Kwa upande mwingine, kiongozi mbaya huchukulia kuwa yeye ndiye mmiliki na huiona ile nyumba/ kampuni kama mali yake binafsi. Kwa mujibu wa kazi hii, tutachukua kampuni kuwa kanisa. Hivyo basi, kiongozi huyu wa kanisa ni lazima awajali wafuasi wake na pia atambue kuwa yeye si mmiliki wa lile kanisa bali anafaa kulitunza kwa niaba ya wafuasi na mmiliki wake ambaye ni Mungu. Haya ndiyo riwaya ya *Paradiso* inayoyazungumzia katika kutoa suluhu ya matatizo yanayoikumba asasi hii. Ni lazima mchungaji awe mfano mwema kwa kondoo. Katika riwaya hii, tunapata picha ya viongozi ambao wanatenda kinyume na yale yanayotarajiwa kutoka kwao. Ni viongozi ambao hawana dhamiri inayowahukumu,

wanajiendeleza kwa kutumia mali ya kanisa huku wafuasi wakisahaulika; jambo ambalo mwandishi anatuambia ni kinyume na imani ya kikristo.

> Yeye Michael alijaribu kusimama wima kama mti uliomea karibu na mto. Aliamini kasisi alipaswa kuwa mfano mwema kwa wale anaowaongoza. La sivyo atakuwa kama kiongozi aliyezungumziwa katika Ezekieli 34 anayejiendeleza bila kuwazia kondoo wake. Kiongozi kama huyo hakufaa kitu (uk. 67).

Mwandishi anawataka viongozi wa kanisa kuwaangazia wafuasi wao na kuona jinsi wanavyoweza kuwasaidia kiimani kama njia moja ya kuchangia suluhu katika jamii.

### 4.6.2 Kiongozi Anayewachunga Anaowasimamia (Kondoo)

Stuckelberg (2007) anasema kuwa mtumishi mwaminifu huchunga watu anaowasimamia. Huwapa chakula, mshahara na huwasaidia waweze kujisimamia. Yule mbaya huwadhulumu anaowasimamia. Tumeona kwamba umaskini uliokithiri umechangia pakubwa kuanzishwa kwa makanisa hasa katika vitongoji duni vya miji mikuu. Kwa hivyo, wafuasi wanatafuta kikundi chochote kile kitakachowapa matumaini ili waweze kukabiliana na hali inayowakabili. Ni wazi kwamba kando na kuhudumiwa kiroho, ni muhimu pia kwa viongozi wa dini kuona ni vipi wanaweza kuwasaidia wafuasi wao ili kukabiliana na hali yao ya kiuchumi. Na kwa hivyo badala ya kutumia hali ya wafuasi kuwadhulumu na kujifaidi kifedha wana jukumu la kuwasaidia kujikwamua kutoka kwa hali hiyo. Wazo kuu ambalo limeangaziwa katika riwaya ya *Paradiso* ni ule ubinafsi wa viongozi ambao wamewasahau wanaowahudumia na badala yake wanajiangazia wenyewe. Hili, kulingana na mwandishi, limesababisha asasi hii kukosa heshima. Kupitia kwa kasisi Michael, mwandishi anasema kuwa ni lazima asasi hii iwaangazie waumini kwa kuwasaidia walio maskini miongoni mwao na pia kutoa huduma kwa waumini. Anasema hili litairejesha heshima yake kwa waumini.

> Alitaka kanisa litakalosaidia maskini miongoni mwa waumini na kufanya miradi ya kujenga zahanati na skuli za kuhudumia umma.

> Hivi wangekuwa na kitu cha kuonyesha ulimwengu. Ulimwengu ukisadiki basi na wokovu utaheshimiwa (uk. 78).

Hata hivyo, mwandishi anasema yote hayajapotea kwani kuanguka ni kawaida kwa mwanadamu lakini la muhimu ni kuamka tena. Kasisi Micheal alimwasi Mungu kwa kuzini na Patricia huku akiendelea na huduma ya Mungu. Licha ya kuwa Michael alianguka, alimrudia Mungu na hivyo akaepuka adhabu yake na kuendelea na kazi yake ya uhubiri. Kwa hivyo bado kuna matumaini ikiwa wahubiri wataamka kutoka mahali walipoanguka na kuchukua nafasi yao katika jamii.

> Michael alikumbuka wosia wa Salome kuwa, kosa kubwa si kuanguka. kosa kubwa ni kuanguka na ukatae kusimama…Yaani kukubali kila sampuli ya mwanadamu ni mkosaji na wajibu wa wanadamu ni kusameheana. Hizo ndizo nguzo muhimu katika wokovu. Nguzo ya mwisho inayotawala hizo ni toba kwa Maulana na kufanya suluhu naye (uk. 185).

Mwandishi anawaita viongozi hawa kumrudia Mungu na kufanya yaliyo ya kweli ili waweze kujirehemu na pia kuirudishia hadhi na heshima asasi hii. Ni katika kufanya hivi ambapo asasi hii itaweza kutekeleza wajibu iliyowekewa na jamii.

### 4.6.3 Kiongozi Mfanyakazi

Kiongozi mwema, kulingana na Stuckelberger, hufanya kazi kwa bidii kwa niaba ya washiriki wake na hivyo basi huwa kielelezo kwao. Kiongozi mwovu hafanyi kazi, ni mfisadi, mlafi na mdhalimu. Udhalimu wake na unyanyasaji hudhihirisha kuwa anawachukulia anaowasimamia kuwa mali yake binafsi. Ubadhirifu unaosawiriwa na viongozi wa makanisa katika riwaya hii unawaweka viongozi hawa katika aina ya pili ya viongozi ambao ni wadhalimu. Hii ndio hali ambayo mwandishi, katika azma yake ya kuunda jamii mpya, anawarai viongozi wairekebishe. Anawaambia viongozi hawa wa makanisa kwamba hamna haja ya kujilimbikizia mali huku wakiwatenga wengine kwani, kwake, hili ni ubatili mtupu. Licha ya kuwa na nyumba kubwa huko Karen huku ikiwa na kila kitu, Joshua alikosa raha baada ya ndoa yake kukumbwa na misukosuko.

Na licha ya kuchukua mali ya kanisa huku hata wakiwawekezea watoto wao kwa siku zijazo, wanakufa na kuyaachia mali yao wengine ambao hata hawakuyatafuta:

> Pesa na magari ameachia wengine ambao hata hawatashughulika kuzitunza na wala hawajui pesa hizo zimepatikana vipi (uk. 134).

Boribori pia alijiwekea utajiri mkubwa kwa fedha alizopata kutoka kwa kanisa la New Jerusalem. Hakuwafikiria wafuasi bali yeye mwenyewe na familia yake. Lakini yote yote hayo yanaisha baada yake kufungwa jela anapopatikana na kashfa ya ulanguzi wa madawa ya kulevya.

> Nyumba yake Karen imesimama kwenye shamba la ekari mia mbili. Humo shambani mmepandwa miti ya sampuli nyingi. Katika sehemu moja ya shamba lake alifuga farasi. Sehemu iliyosalia ilipambwa kwa miti ili kupafanya mahali hapo ahera duniani. Wafanyikazi wa shamba hili walikuwa kiasi cha kumi. Kulikuwa na wafagiaji, wakulima, wachanja kuni na tarishi wa kutumwa. Nyumba yake nayo ni masimulizi. Imetamba kwenye nusu ekari. Ina matagaa sita. Walijenga waachi kutoka Israel. Vyuma vilivyoijenga viliagizwa kutoka Ujerumani. Sakafu yake imefanywa kwa vigae maalum vya kutoka Ufaransa. Milango ya nyumba yake iliagizwa mahsusi kutoka wasanii wa Pate. Imechorwa maandishi kutumia alfabeti ya Kiarabu. Maegesho yake yana magari sita. Nyumba hii Boribori ameihama sasa. Hakuihama kwa hiari, amehama kwa lazima. Ameihama kwa ajili ya hadaa. Sasa Boribori analala mto uliochanika. Chumba chake ni cha kimo cha choo kidogo. Hakuna mwanga. Hakina marashi. Hakina muziki wa kidini. Kina maji. Uchafu. Mwanga wake ni hafifu. Chakula ni cha taabu (uk. 222).

Viongozi hawa wanakumbushwa kuwa mali wanayojiwekezea haitawafaidi chochote ikiwa hawaishi kulingana na nguzo za imani. Na ndio maana wote hawakuishi kuifurahia licha ya kujilimbikizia.

Licha ya viongozi hawa wa kanisa kujilimbikizia mali, hatuoni wakifanya kazi yoyote, na kwa hivyo wao si mfano mwema kwa wanawaongoza. Badala yake, wamechukuwa injili ya utajiri kuwa ndio nguzo kuu katika mengi ya makanisa wala si kufanya kazi. Na kwa hivyo, wengi wa wafuasi wanaikimbilia dini ili wawe matajiri huku viongozi wakianzisha kanisa ili wapate utajiri wa haraka.

> Alizoea kusema, 'Mungu tunayemwabudu ni Mungu wa utajiri. Maulana hakutaka tukae katika ufukara.' Hii ndiyo injili Boribori alipata hapo New Jerusalem na akaifanya ishamiri kama mti wa ukufi uliomea katika mbolea ya samadi (uk. 213).

Mwandishi analiendeleza wazo hili akisema

> "yeyote aliyetaka utajiri wa haraka alikimbilia injili. Humo humo ndimo watu walitafuta wake na hata wanawake. Makanisa yalianzishwa kwa haraka na kugawanyika kila mmoja akitafuta riziki yake. Imekuwa ni vigumu kwa yeyote kujua ni lipi kanisa bora na ni lipi si bora. Makanisa yote yalishindana yakivutana huku yakilaumiana" (uk. 220).

Askofu Nana aliyechukua nafasi ya Boribori aliigeuza injili katika kanisa la New Jerusalem kwa kusisitiza maadili ya kimsingi ya haki na upendo na pia subira. Na kwa hivyo mwandishi anairai jamii kuzirudia nguzo za kimsingi za dini badala ya hali ilivyo sasa ambapo viongozi na waumini wanajiingiza katika maovu mengi kutokana na tamaa ya utajiri.

> Nana akiweka mkondo mpya wa injili. Injili yake ilitoka kwenye zaka, na maendeleo hadi kwenye 'kwenenda kwa haki na kupendana kwa majirani.' Injili hii haikupendeza sana pale New Jerusalem ambapo ilizoeleka kuwa usipotajirika haraka kwa kujenga nyumba na kuleta gari la bei basi wewe si muumini aliyeokoka kikamilifu. Sasa ilikubalika kuwa Muumba ndiye aliyembariki mja wake kupitia kazi za mikono yao. Subira ilikuwa muhimu ili kupata ahadi za Bwana (uk. 226).

Riwaya ya *Paradiso* inatoa kauli kuwa utajiri hautokani na miujiza bali kwa kufanya kazi na kwamba watu hawafai kutafuta utajiri wa haraka. Kwake mwandishi, utajiri ni jambo linalohitaji subira na kwamba Mola huwabariki waja wake kupitia kwa kazi za mikono yao.

### 4.6.4 Kiongozi Mwema huwa Tayari Siku Zote

Stuckelberg (2007) anaendelea kusema kwamba mtumishi mwema siku zote hufanya kazi njema kwani hujua mwajiri wake huenda akarudi wakati wowote. Maadili ya kibiashara na wajibu kwa Mungu hushirikishwa katika maisha yake ya kila siku. Anaendelea kusema kwamba meneja mjinga anaamini kuwa hawezi kudhibitiwa,

kwamba anaweza kushinda kesi yeyote kwa kuwahonga majaji, kwamba inatosha kwenda kanisani na kuanza kuomba wakati mwisho wake unakaribia ili aokelewe. Haya ndio yamekuwa yakiendelea kulingana na riwaya ya *Paradiso*. Askofu Musa alipozini, hakuomba msamaha kwa Mungu na badala yake alitoka kwa huduma na kuanza biashara kutokana na fedha alizokuwa amepata akiwa mhubiri. Kutokana na kufana kwa biashara zake, hili lilimpa kiburi ambapo aliona amejiweza kama binadamu. Mwanzo biashara zake zilifana sana lakini hatimaye zikaanza kuisha na hatimaye kuanguka.

> Masaibu mengi yalimkuba. Tapeli mmoja alimtapeli katika biashara yake ya zebaki. Alipoteza pesa nyingi katika kashifa hiyo. Baadaye mtoto wake alimwibia bumba la pesa. Leo alionekana barabarani akiyazungukia. Ameshikwa na wazimu (uk. 74).

Musa anaaga dunia baada ya kugongwa na gari. Joshua na mkewe Lona pia wanakutana na adhabu hiyo hiyo baada ya kumwasi Mungu. Joshua na Lona walimwibia Mungu kwa kuchukua mali ya kanisa wakajiwekezea. Lona akaona kwamba hata hamhitaji Mungu na kutafuta usaidizi kutoka kwa ushirikina na hata kwa siasa. Licha ya kuanguka, hawakuona haja ya kumrudia Mola na tunaona walipata ajali na kufa papo hapo. Mwandishi anatuambia kuwa ingawa wanaweza kudhibiti yote wakiwa duniani, kuna yule ambaye hawawezi kumdhibiti naye ni Mungu.

> Hakuna tena kilichomtisha Lona. Tayari amemdhibiti mumewe. Alidhibiti uchumi. Aliwadhibiti waumini. Sasa alidhibiti siasa za nchi. Maana hata rais wa nchi alimfahamu. Si muhali kumwona akitumika siku za holidei akiomba au kama amekaa na wakubwa wa serikali huku kajipamba lile joho. Hata kama Lona alidhibiti kila kitu, kuna kimoja tu hakukidhibiti nacho ni wakati na ahadi yake kwa Bwana (uk. 131).

Mwandishi anatoa onyo kali kwa viongozi wa makanisa akisema hawawezi kuepuka adhabu ya Mola. Kwamba ingawa wamepata mali, wamedhibiti kanisa na hata viongozi wa kisiasa, wao ni binadamu tu na kwa hivyo hawawezi kumdhibiti Mungu.

Mwandishi anawakumbusha viongozi hawa kwamba hao ni binadamu tu na wanaotoa huduma kwa niaba yake Mungu ambaye ndiye mwajiri wao na kwa hivyo ni lazima

watende kazi yake kwani huenda akarudi wakati wowote. Mwandishi anawataka viongozi wa makanisa kuirejesha katika hali yake ya kuwahudumia watu kwa kukemea yaliyo mabaya, kuwajali wasio na mali na kuirekebisha serikali inapokosea. Haya yatawezekana tu ikiwa asasi hii ya dini itakuwa na umoja. Mwandishi anapendekeza kuwe na uelewano kati ya dini moja na nyingine ili kuwe na umoja. Anasema hili linawezekana ikiwa dini moja itafanya juhudi kuielewa nyingine kwani, kulingana naye, hamna tofauti kubwa kati ya dini moja na nyingine. Anasema tofauti hizi katika dini husababisha vita. Na kwa hivyo kukiwa na umoja, basi dini itakuwa na nafasi nzuri ya kusuluhisha mengi ya matatizo yanayoikumba jamii na pia itaweza kuishauri hata serikali:

> Umoja wa dini utasaidia kupunguza ushindani wa kidini na pia utasaidia katika kupunguza vita ulimwenguni. Maana vita hutokea kwa sababu ya tofauti za kidini. Pia, dini katika nchi mbalimbali zitashauri serikali zao vizuri kukiwa na mwafaka huu (uk. 228).

**4.7 Hitimisho**

Kwa hivyo kwa kuzingatia riwaya ya *Paradiso* tunaona kuwa waandishi wanakuwa ndio mawakala ambao wanatusaidia kuelewa yanayoendelea katika jamii. Katika riwaya hii, tunaona jinsi uozo ulivyokithiri katika asasi hii ambayo imekuwa si paradiso tena. Viongozi wa makanisa wanashiriki ulanguzi, ulafi, utengano, vita na mengineyo. Utajiri unakuwa ndio nguzo kuu kanisani badala ya maadili. Hii ndio maana tunashuhudia utengano na maovu mengine. Na kwa hivyo, inakuwa vigumu kwa kanisa kuirekebisha jamii hata inapopoteza mweleko kwa vile wao pia wako katika mkondo ule ule. Wafuasi pia wanalaumiwa kwa kuchangia hali hii. Hii ni kwa sababu hawaendi kanisani kutafuta paradiso lakini badala yake wanaenda kutafuta miujiza kutokana na matatizo mbali mbali yanayowakumba. Mwandishi anatuambia ni lazima asasi hii iwe mahali ambapo watu wanaweza kupata paradiso, yaani palipo na haki na upendo. Mwandishi anatoa kauli kali kwa viongozi wa dini kwani kwake yeye wamekuwa ‘debe tupu zinazopiga

kelele tu'. Ili kubadilisha hali hii na kurejesha heshima ya dini, ni lazima wachukue mkondo mpya, mkondo wa kuwatetea wanyonge, kuirekebisha serikali na kusisitiza maadili ya kufanya kazi na si miujiza. Suala la umoja wa dini limetiliwa mkazo kwani kukiwa na umoja katika dini basi dini itakuwa na fursa nzuri ya kusisitiza umoja huo huo katika jamii. Anasema uelewano wa dini na umoja zitairudishia hadhi asasi hii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti na mchango wa utafiti. Pia sura hii inashughulikia mapendekezo yanayotokana na utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Kutokana na kazi zilizoshughulikiwa, ni wazi kwamba uongozi bado ni changamoto ambayo inaendelea kukumba jamii za kiafrika na ndio maana bado waandishi wanaendelea kuandika kuhusiana na suala hili. Kwa kuangazia kazi zilizoteuliwa katika utafiti huu, ni wazi kwamba changamoto hazimo tu kwa uongozi wa kisiasa na serikali bali pia katika asasi ya dini. Kama waandishi wa hapo awali, waandishi wa kisasa pia wanawalaumu viongozi kwa hali ambayo imeendelea kushuhudiwa katika bara la Afrika. Vitendo vya viongozi vinaathiri hali ya wananchi ambapo tunaona viongozi wakishiriki katika ufisadi, ubadhirifu na ukiukaji wa sheria. Kutokana na hali hii, fedha kidogo ambazo ziko nchini zinatumiwa kwa manufaa ya wachache huku wengi wakiendelea kuumia. Tunaona jinsi viwanda vinavyohudumia wakulima vinafilisishwa na wachache wanaovisimamia na kuwaacha wakulima bila njia za kujiendeleza kiuchumi.

Waandishi wa sasa wanatuambia kuwa ukoloni mamboleo bado upo lakini tofauti na wale wa hapo awali, Wamitila anatuambia kuwa ukoloni huu unaletwa na viongozi ambao tumewachagua kutuwakilisha lakini badala yake wanatetea maslahi ya wageni. Kwa mujibu wa Wamitila, viongozi wanavunja sheria iliyowekwa kuwalinda wananchi ili kuwapa wageni nafasi ya kuwanyanyasa wakazi kwa kuwanyang’anya rasilmali zao. Anaendelea kutuambia kuwa viongozi wanaochaguliwa hawana haja ya kuwahudumia wananchi bali nia yao ni kupata nafasi ya kujinufaisha. Na kwa hivyo hawana haja ya

kutatua matatizo yanayowakumba wananchi. Ndio maana licha ya kuwa nchi zimekuwa huru miaka mingi, bado hazijaweza kukabiliana na changamoto za jamii kama vile utoaji wa huduma za kimsingi kama vile chakula na afya.

Tunaona viongozi ambao hawafanyi lolote kukuza hali ya wananchi ya kujitegemea bali wanaendeleza ile kasumba ya kuendelea kutegemea misaada kutoka nchi za kigeni. Hata hivyo, misaada hiyo inaishia kuwadhulumu wananchi kv. watoto wasichana wanaodhulumiwa kimapenzi na pia chakula cha misaada kinachoishia kuwadhuru wananchi kiafya. Vitendo hivi vya viongozi vinachangia pakubwa hali ya umaskini inayoendelea kushuhudiwa katika jamii.

Bali na viongozi, riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* inatuambia kwamba wananchi pia wanachangia pakubwa hali iliyoko katika jamii. Hii ni kwa sababu hawana ule umoja utakaowawezesha kupigania maslahi yao. Tunaona dhuluma zikitekelezwa katika sehemu mbali mbali za nchi lakini ni wale wananchi ambao wanadhulumiwa wanaopigania maslahi yao huku wengine wakikosa kujishughulisha na yanayoendelea. Na hata hao wanaodhulumiwa wanateta kwa muda tu baada ya kudanganywa na viongozi kwamba matatizo yao yatatatuliwa. Hivyo, tunaona wananchi ambao hawafuatilii jambo hadi wakapata suluhu. Wananchi pia wanauenzi ufisadi kwani wanawakashifu wale wasiojitajirisha kwa kutumia nafasi zao za kazi. Hili linaonyesha kuwa wakipata nafasi pia wao watashiriki ufisadi na labda ndio maana hawawakashifu viongozi wanaposhiriki ufisadi.

Hata hivyo mwandishi anatuambia kuwa yote hayajapotea kwani kuna suluhu ambalo linatokana na ushirikiano kati ya viongozi na wananchi katika kutatua matatizo yanayowakumba wananchi.

Katika riwaya ya *Paradiso*, tunashuhudia asasi ya dini ambayo imepoteza mwelekeo na kwa hivyo haiwezi kutekeleza majukumu iliyowekewa na jamii kwani maovu yote yanatendwa kanisani na hasa na viongozi wa kanisa. Tunaona yale yanayoshuhudiwa katika uongozi wa serikali na siasa ndio yale yale yanayoshuhudiwa katika asasi ya dini. Katika asasi hii, tunashuhudia tamaa ya mali, ubadhirifu, unafiki, ghasia, ubinafsi na mengineyo. Ni wazi kwamba suala la tamaa ya pesa na si imani na maadili ndiyo masuala yanayotawala asasi hii. Kutokana na haya, asasi hii inakosa umoja, upendo na utangamano; jambo ambalo linasababisha kuvunjika kwa makanisa kila uchao. La kusikitisha ni kwamba wengi wanategemea viongozi hawa kuwapa mashauri lakini ushauri wanaotoa ni wa kijuujuu tu kwani hata wao wenyewe hawauamini. Ni wazi kuwa asasi hii haiwezi kukashifu maovu yanayoendelea katika jamii na kwa hivyo imepoteza uwezo wake wa kuirekebisha jamii.

Kazi hii pia inawalaumu waumini kwa yanayoendelea katika asasi hii. Hii ni kwa sababu waumini hawaendi kanisani kutafuta maadili bali wanatafuta miujiza itakayotoa suluhu kwa matatizo yao ya kibinafsi. Katika riwaya hii, mwandishi anaitaka asasi hii kuirudia hali yake ya awali ambapo watu waliitegemea kutoa mwelekeo ili kuirudishia heshima na hadhi yake. Umoja kati ya waumini na dini moja na nyingine utaifanya asasi hii kusikilizwa na wote wanapotoa maoni yao kuhusu yanayoendelea katika jamii.

### 5.3 Matokeo ya Utafiti

Kazi zilizoteuliwa zimedhihirisha wazi kwamba tatizo la uongozi linaendelea kuwa kero katika jamii. Hata hivyo, waandishi wanatoa mapendekezo ambayo kulingana nao yanaweza kurekebisha hali hii.

I. Utafiti huu umekisia kwamba waandishi wa sasa wamechukua mwelekeo mpya wa kuyashughulikia matatizo ya uongozi. Mwelekeo huu ni ule wa ndani nje

ambao unaangazia changamoto za uongozi kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Kwa kutumia mwelekeo huu, waandishi wa riwaya mpya wanawaangazia viongozi waliomo mamlakani na vitendo vyao na jinsi vinavyochangia hali iliyoko. Kwamba uongozi ukiwa bora nchi itashuhudia maendeleo lakini ukidhoofika nchi pia inadhoofika kwani vitendo vya viongozi vina athari ya moja kwa moja kwa jamii. Lakini ili uongozi uwe wa manufaa, wanapendekeza kuwa ni lazima viongozi wayaangazie matatizo yaliyomo katika jamii na kwa kushirikiana na wananchi watafute suluhu ya matatizo hayo. Badala ya kiongozi kuanzisha miradi ya kibinafsi, ni muhimu kushirikiana na wanaowaongoza ili kwa pamoja waweze kupata miradi itakayowafaidi wanajamii. Hivyo basi ni vyema kuwa na viongozi walio na maono ya jamii pana badala ya kuwa na maono yao ya kibinafsi ambapo miradi wanayoanzisha ni ya kuwahakikishia kuwa watazidi kukaa uongozini licha ya kuwa haina manufaa yoyote kwa jamii. Hili litakuwa pia njia moja ya kukabiliana na tatizo la ufisadi uliokithiri hasa miongoni mwa viongozi ambao hushiriki ufisadi ili wapate fedha za 'kununua' uongozi kwa kuwahonga wapiga kura ili wachaguliwe tena. Kando na kuifilisha nchi, hili sio hakikisho kuwa watachaguliwa tena. Kwa kufanya hivi, wananchi watakuwa na imani nao na hata kuwachagua tena. Pia licha yakuwa kila kiongozi anajitafutia makuu, kuna uwezekano wa kuwa na kiongozi ambaye anapigania sio maslahi ya eneo bunge lake lakini pia maslahi ya nchi kwa ujumla.

II. Haitoshi tu kushiriki katika uchaguzi lakini ni muhimu kwa wananchi kufuatilia vitendo vya viongozi wanaowachaguwa na utendakazi wao kwani hili litawafanya kuwajibika kwa wanayoyafanya. Kando na hili ni muhimu kwa wananchi kuwa na umoja na kuelewa kwamba jambo linaloathiri sehemu moja

linafaa kushughulikiwa na kila mwananchi. Na kwa hivyo ikiwa kuna dhuluma inayotendewa wananchi katika sehemu fulani, wengine wanafaa kuungana na wenzao kuona kwamba wanasaidika ili hili liwe funzo kwa viongozi. Pia wasiwe watu wa kudanganyika kwa haraka ambapo haki zao zinapogandamizwa wanadanganywa na viongozi kuwa hatua itachukuliwa ili wanyamaze. Ni lazima wafuatilie jambo hadi watakapopata suluhu na wasiwe watu wa kusahau na kungoja hadi jambo lingine lifanyike. Ili kuwe na maendeleo katika jamii, waandishi wanapendekeza kuwa ni lazima wananchi wakemee uovu kama vile ufisadi. Yaani wasichukulie nafasi wanayopata katika afisi mbali mbali kuwa nafasi ya kujitajirisha kwa kutumia mali ya umma.

III. Kwa muda mrefu nchi za kiafrika zimekuwa zikipokea misaada kutoka nchi za ughaibuni ili kufadhili miradi mbali mbali ya maendeleo na pia kukabili matatizo yaliyomo katika jamii. Hata hivyo waandishi wanatoa tahadhari kuhusu misaada hii na wanapendekeza kuwa badala ya kutegemea misaada, la muhimu kwa nchi hizi ni kukuza uwezo wa wananchi wa kujitegemea. Hii ni kwa sababu mingi ya misaada haiwasadii wananchi huku mingine ikiwa ni ya kuwadhulumu.

IV. Pia kuna haja ya kutumia rasilmali zilizoko nchini kwa njia inayofaa badala ya rasilmali hizo kuwafaidi wachache huku wengi wakiwa hawana njia za kujipatia riziki. Hili litasaidia nchi kukabiliana na matatizo ya ukosefu wa huduma za kimsingi kama vile ukosefu wa chakula na huduma za afya miongoni mwa zingine. Mnamo mwaka wa 2010, nchi hii ilipitisha katiba ambayo ilianzisha mfumo wa utawala wa ugatuzi. Kufuatia mfumo huu, fedha zinaletwa mashinani ambapo kila kaunti inafaa kuanzisha miradi kulingana na mahitaji ya wananchi. Mfumo huu kama ulivyo, unaweza kusaidia katika kutatua tatizo la rasilmali.

Hata hivyo bila wananchi kufuatilia kwa makini jinsi fedha zinavyotumiwa huenda tatizo la ugawaji mbaya wa rasilmali litaendelea.

V. Asasi ya dini bado inategemewa na jamii kuendelea kutoa mwelekeo na pia kupigana na maovu yanayoendelea katika jamii. Lakini ili ifaulu katika jukumu hili, ni lazima asasi hiyo ijisafishe kutokana na maovu yanayoiandama. Ni lazima asasi hiyo irudie hali yake ya awali kwa kurejesha umoja, upendo na maadili makanisani. Viongozi wake ambao wamejishusisha na mengi ya maovu haya wana jukumu kubwa la kubadilisha hali iliyoko. Pia kando na kuwa na umoja kati ya viongozi na waumini, ni muhimu umoja huu udhihirike kati ya dini moja na nyingine na pia miongoni mwa madhehebu mbali mbali ili wanapoongea kuhusu jambo waweze kusikilizwa. Umoja miongoni mwao utawawezesha kudumisha umoja miongoni mwa jamii.

VI. Waumini pia wanaambiwa kuwa matatizo yao ya kibinafsi na kutafuta utajiri yasiwe ndio mambo yanayowapeleka kanisani lakini wao pia wawe mstari wa mbele kuyatafuta maadili. Pia wanafaa kuichunguza mingi ya miujiza inayofanyika makanisani kwani mingi si ya kweli bali ni njia ya viongozi kuongeza idadi ya waumini ili fedha wanazopata ziongezeke.

Kwa kutumia nadharia ya uhistoria mpya, tumeweza kuangalia matini za kifasihi na zile zisizo za kifasihi. Hili ni kulingana na mihimili ya nadharia hii inayoshikilia kwamba kazi za kifasihi si zao la fikira za mwandishi lakini huzalishwa na hali halisi ya kijamii. Kwa kutumia nadharia hii tumeweza kudhibitisha kwamba yaliyoandikwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* na *Paradiso* si ubunifu tu wa mwandishi lakini na mambo halisi yanayotendeka katika jamii katika kipindi hiki maalum cha kihistoria. Pia nadharia hii inasema kwamba jinsi mwandishi anavyoathiriwa na jamii, yeye pia vile vile huiathiri

jamii kwa kutoa suluhu za matatizo ambayo anayaona katika jamii. Kwa hivyo tumeweza kuangazia suluhu ambazo zimetolewa na waandishi kuhusu matatizo ya uongozi.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unatoa mchango wa kitaaluma katika nyanja ya fasihi hasa riwaya kwani umeangazia mabadiliko yaliyoko katika kulishughulikia tatizo la uongozi katika kipindi hiki cha kihistoria. Kwamba ingawa bado kuna athari kutoka nje, tatizo kubwa limo miongoni mwetu yaani kwa viongozi tunaowachagua na vile vile wananchi. Unachangia katika kuwazuzua wananchi kujua kwamba wana jukumu na mamlaka ya kubadilisha hali yao kupitia kwa viongozi huku viongozi wakielezwa kwamba wanafaa kuwajibika kwa wananchi waliowachagua.

Pia utafiti huu unaongeza maandishi ya kitaaluma kuhusu uongozi barani Afrika hasa katika uandishi wa riwaya.

## 5.5 Hitimisho

Katika kuhitimisha, ni wazi kwamba uongozi umedhoofika katika asasi hizi muhimu katika jamii. Pia, kama waandishi wanavyotuambia, matatizo haya yanatokana na jamii yenyewe na kwa hivyo wanajamii wanafaa kujilaumu wenyewe kwa hali ambayo inawakumba. Na jinsi matatizo haya yako katika jamii, vivyo hivyo ndivyo jamii ina suluhu za matatizo yao. Waandishi hawa wanatuambia kuwa viongozi wanaakisi jamii na kwa hivyo tunapowalaumu ni vyema pia kama wananchi tujilaumu kwani sote tunachangia hali iliyoko. Huu ndio mtazamo wa ndani nje ambao unapendekezwa na waandishi wa riwaya ya kisasa.

## 5.6 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye

Utafiti huu ulishughulikia tu riwaya na kwa hivyo itakuwa ni bora kuangalia maoni ya watunzi wa aina zingine za fasihi andishi kama vile tamthilia, hadithi fupi na hata nyimbo miongoni mwa zingine wanavyoshughulikia suala hili la uongozi.

Nchi ya Kenya ilipitisha katiba ambapo kupitia ugatuzi, kila kaunti inapata mgao wa pesa zinazotokana na ushuru. Katiba hii inasisitiza kuhusishwa kwa umma katika uongozi na utawala. Ni muhimu kutafiti yale waandishi wanasema katika kipindi hiki kuona ama hili limebadilisha taasisi ya uongozi.

Utafiti huu ulishughulikia uongozi katika asasi ya dini kwa kuzingatia dini ya kikristo, kuna dini mbali mbali na hivyo basi ni muhimu kuangazia yanayojiri katika dini zingine k.v dini ya kiislamu kwani ni mojawapo ya dini kuu hapa nchini na pia barani.

**MAREJELEO**


Afegbua, S. I., & Adejuwon, K. D. (2012). The Challenges of Leadership and Governance in Africa. *International Journal of Academic Research in Business and Social Sciences*, *2*(9), 141-157.

Agbamila, O. D., & Abdulganiyu, A. I. (2014). The Role of Religion in Modern Society: Masses Opium or Tool for Development: A Case Study of Saw-Mill Area, Ilorin, Kwara State, Nigeria. *International Journal of Sociology and Anthropology*, *6*(1), 8–17.

Akech, M. (2011). Abuse of Power and Corruption in Kenya: Will the New Constitution Enhance Government Accountability? *Indiana Journal of Global Legal Studies*, *18*(1), 341-394.

Amutabi, M. N. (Ed.). (2009). *Studies in the Economic History of Kenya: Land, Water, Railways, Education, and Entrepreneurship*. New York: Edwin Mellen Press.

Balkaya, M. A. (2014). Basic Principles of New Historicism in the Light of Stephen Greenblatt's Resonance and Wonder and Invisible Bullets. *European Academic Research*, *II*(5), 7068-7078.

Bhat, A. A. (2014). A Critical Note on New Historicism. *Galaxy International Multidisciplinary Research Journal*, 3(lll), 12-18.

Bohman, J. (2016). Critical Theory. *The Stanford Encyclopeadia of Philosophy*. Retrieved May 23 1018

Brautigam, D. (2000). *Aid Dependence and Governance* (Vol. 1). New York: Expert Group on Development Issues.

Burgess, R., Remi, J., Edward, M., Ameet, M., & Gerard, P. (2015). The Value of Democracy: Evidence from Road Building in Kenya. *American Economic Review*, *105*(6): 1817-1851.

Callan, S. (2014). Building a Strong Society Requires Effective Family Policy. *DIFI Family Research and Proceedings* 2014. Retrived June 7 2107 from http://dx.dol.org/10.5339/difi

Dasylva, A. O. (2003). The Writer and Ph(f)aces of Conflicts in Africa. In L. Oyeleke and M. Olateju (Eds.), *Readings in Language and Literature.* Osun State: OAU Press.

Dogan, E. (2005). New Historicism and Renaissance Culture. *Ankara Universitesi Dil Ve Tarih-Congrafya Fakultesi Dergisi*, *45*(1), 77-95.

Edi, E. (2007). Africa and the New World Order: Voices and Ways of Liberation in Armah's Osiris Rising. *The Journal of Pan African Studies*, 1(9), 117-135.

Foucault, M. (1982). The Subject and Power. In H. Dreyfus and P. Rabinow (Eds.), *Michel Foucault: Beyond Structuralism and Henneneutics.* Chicago: University of Chicago Press.

Gardner, J. W. (1990). *On Leadership*. New York: Free Press.

Gathogo, J. (2011). The Challenge of Money and Wealth in Some East African Pentecostal Churches. *Studia Historiae Ecclesiasticae September*, *37*(2), 133-151.

Goddard, W., & Melville, S. (2005). *Research Methodology*. Landsdowne: Juta & Co Ltd.

Gromov, D. (2014). The Present State of Swahili Literature as an Artisitc and Social Phenomenon. *Journal of Language and Technology & Entrepreneurship in Africa*, *5*(1), 1-12.

Gromov, M. (2014). Visions of the Future in the 'New" Swahili Novel: Hope in Desperation? *Tydskrif Vir Letterkunde*, *51*(2), 40-51.

Habib, M. A. R. (2005). *A History of Literary Criticism, From Plato to the Present.* USA: Blackwell Publishing.

Habwe, J. H. (2000). *Maisha Kitendawili*. Nairobi: University of Nairobi.

Habwe, J. H. (2000). *Safari ya Lamu*. Nairobi: University of Nairobi.

Habwe, J. H. (2008). *Cheche za Moto.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Habwe, J. H. (2009). *Fumbo la Maisha.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Habwe, J. H. (2010). *Paradiso.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Hendriks, H. J. (2007). Evangelism in Africa. *Practical Theology in South Africa, 22*(1), 23–40.

Hickling, M. (2018). New Histocism. *Brock Education Journal*, *27*(2), 53-57.

Hooti, N., & Omrani, V. (2011). Saul Bellow's Seize the Day: A Modernist Study. *Theory and Practice in Language Studies*, *1*(3), 252-262.

Hope, K. R. (2014). Kenya's Corruption Problem: Causes and Consequences. *Commonwealth and Comparative Politics*, *52*(4), 1493-512.

http://plato.stanfordedu/acrhives/Fall2016/entries/critical_theory/

http://www.gap.ugent.be/africafocus/pdf/92-8-1-Mulokozi.pdf. 5.00pm

Izebaye, D. (1979). Issues in the Reassessemnt of the African Novel. *African Literature Today, 10*, 7-31.

Jain, A. K. (2001). Corruption: A Review. *Journal of Economic Surveys, 15*(1), 72-121

Jameson, F. (1986). Third-World Literature in the Era of Multinational Capitalism. *Social Text*, *15*, 65-88.

Kabeberi, N. (2011). Political Parties and the Quest for Good Leadership. In O. Okombo, B. Muluka and B. Sungura-Nyabuto (Eds.), *Challenging the Rulers: A Leadership Model for Good Governance* (117-135). Nairobi: East African Educational Publishers Limited in partnership with Community Aid International.

Kagema, D. N., & Maina, W. M. (2014). Causes of the New Charismatic Movements (NCMC) in Kenya. *Global Journal of Arts Humanities & Social Sciences, 2*(2), 35-44.

Kahura, D. (2018). Shaking Hands With The Devil: Kenyans' Views on the Raila-Uhuru Pact. *The Elephant,* 31 March. Retrieved April 2019 from https://www.theelephant.info/features/2018/03/31/shaking-hands-withthe-devil-kenyans-views-on-the-raila-uhuru-pact/

Kaiser, R., Padilla, A., Hogan, R. (2007). The Toxic Triangle: Destructive Leaders, Susceptible Followers and Conducive Environments. T*he Leadership Quarterly, 18,* 176-194.

Kakraba, A. D. (2011). Ayi Kwei Armah's Novels of Liberation: *African Nebula,* 3(June), 48-61.

Kareithi, P. M. (1969). *Kaburi bila Msalaba: Habithi ya vita vya Mau Mau*. Nairobi: East African Publishing House.

Kasomo, D. (2010). The Position of African Traditional Religion in Conflict. *International Journal of Sociology and Anthropology, 2*(2), 023-028.

Kehinde, A. (2004). The Tyranny of History in Contemporary African Fiction: A case Study of Meja Mwangi's "Kill me Quick". *Revista do centro de Estuds Africanos, USP S. Paulo,* 265-280.

Kehinde, A. (2005). An Aesthetics of Realism: The Image of Africa in Meja Mwangi's "Going Down River Road". *Entertext, An Interactive E-Journal for Cultural and Historical Studies and Creative Work-A Special Issue on Africa: Myths and Realities, 4*(2), 223-253.

Kehinde, A. (2008). Post-Independence Nigerian Literature and the Quest for True Political Leadership for the Nation. *Journal of Sustainable Development in Africa, 10*(2), 333-360.

Khamis, A. M. (2012). Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili. Retrieved April 6 2018 from http://www.ajol.info/index.php/kcl/article/view file/61424/59568.

Khamis, J. (2018). *Kenya: Looters and Grabbers: 54 Years of Corruption and Plunder by the Elite, 1963-2017*. Plano Texas: Jodey Book Publishers.

Krippendorff, K. (2004). *Content Analysis: An Introduction to Its Methodology*. London: Sage Publications.

Kwaka, J. (2011). Vetting and Social Audit of Leaders. In O. Okombo, B. Muluka and B. Sungura-Nyabuto (Eds.), *Challenging the Rulers: A Leadership Model for Good Governance*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited in partnership with Community Aid International.

Kwaka, J., & Mutunga, T. (2011). Contemporary Kenya and its Leadership. In O. Okombo, B. Muluka and B. Sungura-Nyabuto (Eds.), *Challenging the Rulers: A Leadership Model for Good Governance* (1-37). Nairobi: East African Educational Publishers Limited in partnership with Community Aid International.

Kwaka, J., & Thuranira, M. M. (2011). Contemporary Kenya and its Leadership. In O. Okombo, B. Muluka and B. Sungura-Nyabuto (Eds.), *Challenging the Rulers: A Leadership Model for Good Governance*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited in partnership with Community Aid International.

Lumumba, P. L.O. (2011). The Leadership Kenyans Deserve. In O. Okombo, B. Muluka and B. Sungura-Nyabuto (Eds.), *Challenging the Rulers: A Leadership Model for Good Governance* (1-37). Nairobi: East African Educational Publishers Limited in partnership with Community Aid International.

Masango, M. (2002). Leadership in the African Context. *Verbum Et Eclesia Jrg, 23*(3), 707-718.

Matz, J. (2004). *The Modern Novel: A Short Introduction.* New Jersey: Blackwell Publishing Ltd.

Mbatia, M. (2010). *Msururu wa Usaliti.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mbatia, M. (2004). *Wimbo Mpya.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mbiti, J. S. (1977). Christianity and African Culture. *Journal of Theology for Southern Africa, 20*, 26-40.

Mckee, A. (2001). Textual Analysis: A Beginner's Guide. *Metro Magazine, 127*, 139-149.

Mkangi, K. (1984). *Mafuta*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mojdegani, F. (2016). The New Histocists Reading of Arthur Muller's *The Crucible*. *Canadian Social Science, 13*(2), 13-17.

Mucee, F. M., King'ei, G. K. and Wafula, R. M. (2018). Mbinu ya ubunilizi wa kisayansi katika riwaya Bina-Adamu (K. W. Wanitila) na Babu Alipofufuka (S. A. Mohamed). *International Academic Journal of Social Sciences and Education, Special Issue* 1, 1-38.

Mulokozi, M. (2012). *A Survey of Kiswahili Literature 1970-1988*. Retrieved August 4 2019 from

Mumbo, C. K. (2019). Uchunguzi wa Kidrama wa Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Fasihi Afrika Mashariki. *Unaitwa Nani* ya K. W. Wamitila. *Mwanga wa Lugha, Toleo Maalum*, 105-120.

Mutula, S., Muna, W. K., & Koma, G. P. (2013). Leadership and Political Corruption in Kenya: Analysis of the 2010 Constitutional Provisions on the Presidency. *The Journal of Social Political and Economic Studies, 38*(3), 263-286.

Mwikamba, C., & Ifedha, S. A. (2015). Blessed are the Rich and Prosperous for theirs is the kingdom of the World: The Kenyan Challenge. *Research on Humanities and Social Sciences, 5*(14), 138-141.

Nath, S. (2015). Religion and Its Role in Society. *IOSR Journal of Humanities and Social Science (IOSR-JHSS), 20*(11), 82-85.

Ngetich, D. K. (2014). Christian Religion in John Habwe's 'Paradiso'. *International Journal of Current Research, 6*(7), 7714-7718.

Novikov, V. (1982). *Artistic Truth and Dialects of Creative Works*. Moscow: Progree Publishers.

Ntarangwi, M. (2007). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustan College.

Nyamndi, G. D. (2006). Prospective Commitment in African Literature. *Nordic Journal of African Studies, 15*(4), 566-578.

Odhiambo-Mbai, C. (2003). Public Service Accountability and Governance in Kenya Since Independence. *African Journal of Political Science, 8*(1), 113–145.

Ogola, M. (2014). The Challenges Facing Religion in the Contemporary World: The Kenya Situation. *International Journal of Humanities and Social Science, 4*, 322-328.

Oha, A. (2007). Beyond the Odds of the Red Hibiscus: A Critical Reading of Chimamanda Adichie's *Purple Hibiscus. The Journal of Pan African Studies, 1*(9), 199-211.

Olali, T. (2008). *Mafamba*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Olorunleke, O. (1999). Images of the Colonial State in African Literature: A Prolegomenon. In O. Olorunleke and L. Ladele (Eds.), *New Perspectives in Linguistics and Literature.* Lagos: Ilu Project Associates.

Olowonmi, J. A. (2008). The Writer and the Quest for Democratic Governance in Nigeria: Transcending Post-Independence Dissillusionment: *The Journal of Pan African Studies, 2*(3), 55-67.

Olowonmi, J. A. Olayiwola, A. A., & Olukayode, M. (2009). Fiction in the Era of Globalization: Challenges and Implications for Educational Reform in Nigeria. *The Journal of Pan African Studies, 2*(9), 226-244.

Pantegouh, A. S. (2005). Literary Production in Niger: The Case of the Novel. *TUDSKRIF VIR LETTERKUNDE*, *42*(2), 94-112.

Parsitau, D. S. (2011). Rethinking the Socio-Political Impact and Significance of Pentecostal Christianity in Kenya (1970-2009). In M. N. Ndarangwi (Ed.), *Jesus and Ubuntu: Exploring the Social Impact of Christianity in Africa* (123-145). Trenton, New Jersey: Africa World Press.

Pöysä, A. (2011). *The End of a Single Story? The Post-Colonial Novel and Society*. Doutoramento em Pós-colonialismos e Cidadania Global Centro de Estudos Sociais/Faculdade de Economia, Universidade de Coimbra.

Rodney, W. (1973). *How Europe underdeveloped Africa*. Trans. Joaquin Arriola. London: Bogle-L'Ouverture Publications and Dar-Es-Salaam: Tanzanian Publishing House.

Sanja, L., & Mukhwana, A. (2015). Re-Thinking the Institution of Marriage in the 21st Century and Beyond – New Historicm Approach to the Swahili Novel. *Journal of Sociology and Social Work*, *3*(1), 83-89.

Sharma, R. (2014). New Historicism: An Intensive Analysis and Appraisal. *Indian Review of World Literature in English*, *10*(2), 1-11.

Skinner, J., Edwards, A., & Gilbert, K. (2005). Towards a Critical Theory of Sports Management. *International Journal of Sports Management*, *6*(3), 233-251.

Stuckelberger, C. (2007). *Responsible Leadership: Global and Contextual Ethical Perspectives*. Paris: WCC publications.

Tarmakin, M. (1978). The Roots of Political Stability in Kenya African Affairs. *African Affairs*, *77*(308), 297–320.

Thompson, M. J. (Ed.) (2017). *The Palgrave Handbook of Critical Theory*. New York: Palgrave MacMillan.

Treisman, D. (2000). The Causes of Corruption: A Cross-National Study. *Journal of Public Economics*, 76, 399-457.

Tseggai, I. (2006). *Foreign Aid. A Posion Pill or a Panacea for Progress?* Paper pesented at the Annual Meeting of the International Studies Association, San Diego, CA, March 22.

Walibora, K. W. (2003). *Kufa Kuzikana*. Nairobi : Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (1997). *Contemptus mundi* and *Carpe Diem* in Kezilahabi's Works. *Kishwahili, 60*, 15-24.

Wamitila, K. W. (2008). Point of View in Kiswahili Narrative Fiction: Reading Shafi A Shafi's *Vuta n'kuvute*. *Kiswahili, 71*, 84-97.

Wamitila, K.W. (2007) *Msimu wa Vipepeo.* Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wanyande, P. (2001). Management Politics in Kenya's Sugar Industry. Towards an Effective Framework. *African Journal of Political Science, 6*(1), 123-140.

Wesonga, E., Ambuyo, B., & Mzungu, R. (2020). Nafasi ya Fasihi Katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule *Tikitimaji* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006) za K. W. Wamitila. *East African Journal of Swahili Studies, 2*(2), 54-64.

Woodbridge, N., & Semmelink, W. (2013). The Prophetic Witness of Amos and its Relevance for Today's Church in Africa in Promoting Social Justice, Especially in Democratic South Africa. *The Journal of the South Africa Theological Seminary Conspectus, 16*, 79-100.

Yenjela, D. W. (2017). *Narrated Histories in Selected Kenyan Novels 1963-2013*. Published Thesis, Stellenbosch University, Stellenbosch.

Yerli, K. (2017). Understanding Shakespeare's *King John* and *Magna Carta* in the Light of New Historicism. *Bilgi, 20*(1), 241-259.